
# MSINGI WA KUFANYIKA MWANAFUNZI

**Misingi yawaumini wote**

**Mathayo 28:19-20**

***Mathayo 28:19-20, Yesu akasema, "basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyo waamulu ninyi…"***



**Utangulizi wa kina kwa**
**Fundisho la mitume**
**(Matendo 2:42)**

Nakala hii ni nzuri kutumia katika ushirika wa kanisa la mahali pamoja
Na masomo ya vikundi vidogo.

**REVIVAL MINISTRIES AUSTRALIA**

# UWANAFUNZI

## MISINGI YA KILA MUAMINI

**KITABU CHA MAFUNDISHO NA MAANDALIZI YA WAUMINI WOTE**

Kitabu hiki kumeandaliwa kuwaleta wanafunzi wote katika ngazi ya ukomavu*, ‘**Katika maarifa ya Mungu na Yesu Bwana wetu” 2 Pet 1:2.***** Baada ya kujifunza kitabu cha pili, kuna vitabu vingine vingi ambavyo vinapatikana ambavyo vinamsaidia mtakatifu kuenenda katika ukomavu

**Mtiririko huu wa mafundisho umekusanywa kwa kuwafanya waumini wapya kuwa wanafunzi na kwa wale waumini ambao hawajapata nafasi ya kufundishwa Neno kikamilifu, kuanzia kwa misingi ya imani ya kibiblia.**

**Jinsi ya kutumia kitabu hiki.**

1. Kinatumika vyema kiongozi anapoelekeza kila somo
2. Kinamfaidi mtu kibinafsi, lakini chatumika vyema katika kikundi kidogo
3. Chukua wakati kutazama kila andiko lililopeanwa, endapo andiko lililopatianwa halija nukuliwa lote katika sehemu hii, na endapo haufahamu mazingira ya nukuu kikamilifu.
4. Kitabu hiki kimeandaliwa kama kitabu cha kufanyia kazi; chukua nafansi kujibu maswali katika nafasi iliyopatianwa, chukua nafasi kuchunguza jawabu [endapo kila mwafunzi hana nakala ya kitabu, uliza maswali na uwaulize wanafunzi kujibu kwa karatasi,]
5. Chukua muda kujadiri mazingira na kujibu maswali ambayo yako katika mazingira
6. Katika sehemu nyingi kuna aya ya kujikumbusha, na tunahimiza kila mwanafuzi ajaribu kujifundisha aya kwa moyo.

**Kitatu hiki** kimeandikwa kikiwa chombo cha wachungaji na viongozi wa mahali pamoja kuwafundisha waumini wapya na wengine ambao hawajafunzwa, elimu ya misingi ya Imani. Katika **Mdo 2:42** hii inaitwa ‘Mafundisho ya kitume’

**Lengo:** sisi wote tumeitwa tukue kutoka kwa mkristo mchanga, kuwa muumini aliye komaa, aliye na uwezo wa kuhudumu na kuwafundisha wengine. Kitabu hiki kitaanzisha mwelekeo huo**.**

### Mwito wetu:

- Kuwafanya wanafunzi Mathayo. 28:18-20,
- Kufunza na kuandaa watendakazi kwa ajili ya mavuno, Mathayo.9:37–10:40, Luka.10:1-20
- Kulileta Kanisa katika ukomavu, katika kuwafanya kuwa Wana, Wagalatia.4:10 & 1Kor.4:14-17

Toleo hili lapatikana kwa matumizi katika makanisa na huduma za Kikristo.

**Sheria ya Uchapishaji**

Huduma ya Ufuvio kutoka Australia ya shauri kwamba mafunzo yote na matoleo yote yanalindwa kisheria. Hatahivyo, yametolewa kwa ajili ya Mwili wa Kristo katika utiifu wa Amri ya Bwana kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi ***“na kuwafundisha kuyashika yote niliyo waamuru ninyi,”*** **Mathayo. 28:20**.

Kwa hivyo, yaweza kutolewa nakala kwa wengine kwa kusudi la mafundisho ila sio kwa fidia.

**© Revival Ministries Australia, August, 2010**

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Somo la Kwanza: | ***Wasemaje kumuhusu Yesu?*** |
| Somo la Pili: | ***Yesu ni nani? Maisha yake {sehemu ya 1}*** |
| Soms la Tatu: | ***Yesu ni nani? Maisha yake {sehemu ya 2}*** |
| Somo la Nne | ***Yesu ni nani? Kifo Chake {Sehemu ya 1}*** |
| Somo la Tano: | ***Yesu ni nani? Kifo Chake {sehemu 2}*** |
| Somo la Sita | ***Yesu ni nani? Kufufuka Kwake {sehemu 1}*** |
| Somo la Saba: | ***Yesu ni nani? Kufufuka Kwake {sehemu 2}*** |
| Somo la Nane: | ***Ukweli Umefunuliwa*** |
| Somo la Tisa | ***Naenda Wapi Kutoka Hapa?*** |
| Somo la Kumi: | ***Bibiliani nini?*** |
| Somo la Kumi na moja | ***Kuzaliwa mara ya pili*** |
| Somo la Kumi na Mbili | ***Nifanye nini nipate kuokoka?*** |
| Somo la Kumi na Tatu: | ***Kuzitubia kazi ziszso na uhai*** |
| Somo la Kumi na Nne: | ***Kuwa na imani kwa Mungu*** |
| Somo la Kumi na Tano | ***Mafundisho ya mabatizo*** |
| Somo la Kumi na Sita: | ***Kuwekea mikono*** |
| Somo la Kumi na Saba: | ***Kufufuliwa wafu {Sehemu 1}*** |
| Somo la Kumi na Nane: | ***Kufufuliwa wafu {sehemu 2}*** |
| Somo la Kumi na Tisa | ***Hukumu ya milele*** |
| Somo la Ishirini: | ***Tukaze mwendo tuufikilie utimilifu {sehemu 1}*** |
| Somo la Ishirini na Moja: | ***Tukaze mwendo tuufikilie utimilifu {sehemu 2}*** |
| Somo la Ishirini tna Mbili: | ***Matendo ya Kwanza ya Kanisa*** |
| Somo la Ishirini na Tatu: | ***Kuumega Mkate*** |
| Somo la Ishirini na Nne: | ***Maombi ni nini?*** |
| Somo la Ishirini na Tano: | ***Sala ya Bwana {sehemu 1}*** |
| Somo la Ishirini na Sita: | ***Sala ya Bwana {sehemu 2}*** |
| Somo la Ishirini na Saba: | ***Roho Mtakatifu ni Nani {sehemu 1}*** |
| Somo la Ishirini na Nane: | ***Roho Mtakatifu ni Nani {sehemu 2}*** |
| Somo la Ishirini naTisa: | ***Roho Mtakatifu Anakuja – jinsi ya kujazwa*** |
| Somo la Thelathini: | ***Mungu huongoza vipi?*** |

**SOMO LA KWANZA**

# UNASEMA NINI KUMHUSU YESU?

### Yapo maoni mengi

Watu wana maoni mengi kuhusu Yesu Kristo ni nani.
Wengine wanasema Yesu alikuwa:

- Mtu mzuri
- Nabii
- Mwalimu wa maandili mema
- Mtenda muujiza
- Mtu mashuhuli katika historia
- Kiongozi wa dini
- Mtu aliyefufuka kutoka wafu
- Muamuzi wa waliohai na waliokufa
- Mungu katika mwili
- Mwana wa Mungu
- Masihi ama Kristo
- Mwokozi aliyetoka mbiguni
- *Unaweza kufikiria maoni mengine ama vichwa vya Yesu kuongezea orotha hii*
- ……………………………………………………………………………………………
- ……………………………………………………………………………………………

Hebu tufahamu **Yesu ni nani** kwa kujifundisha toka kwa ushuhuda wa waliomjua alipotembea hapa ulimwenguni.

### Huwa unasema Yesu ni nani?

Hata katika siku za Yesu kulikuwa na kutatanikiwa kwingi. Aliwauliza wanafunzi wake "***Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani"?*** **(Mathayo 16: 13-14).** Wakajibu kwa aina yote ya jawabu wakikisia kwamba alikuwa nabii kutoka kitambo aliye fufuka kutoka kwa wafu. Lakini akawauliza moja kwa moja," ***Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?*** **(Aya ya 15)**
*Andika kwa maneno yako yale unayo yanena kumhusu*

……………………………………………………………………………………………

......................................................................................................................................

### Kumfahamu Yesu ni nani inakubadirisha!

Kwa wakati huu, yule mtume aliyeitwa Petro aliupokea ufunuo. Yesu akasema kuwa ufunuo kama huu hujafundishwa na wanadamu lakini umetoka mbiguni, toka kwa Mungu **(Mt16: 17).** Kwa ghafla ulimuangazia Petro kuwa Yesu ni nani. Alisema "***wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai!"*** alimwona jinsi Yesu alivyo na hii ikambadirisha milele – kwa kweli Yesu alikuwa amembadirishia Jina kutoka kwa Simioni akampa "Petro", inayomaanisha "jiwe" alipokutana na Petro mara ya kwanza (**Yohana 1:42**). Sasa palikuwa na jambo alilolifahamu sana katika maisha yake? Alijua ukweli wa Yesu!

*Umeshapata ufunuo kuhusu Yesu ni nani? Tafadhali shiriki ……………………………………………*

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

## Kuna ushuhuda wa waliomwona Yesu unaotutaalifu habari za maisha yake duniani

Katika Biblia kuna vitabu vinne vinaitwa INJILI ambazo zinatupasha habari ya maisha ya Yesu, huduma, kifo na kufufuka kwa wafu. Mbili kati ya vitabu hivyo, Mathayo na Yohana kimsingi ni chanzo.

Hii inamaanisha kwamba walikuwa na Yesu. Walikuwa watu wa karibu katika kikundi cha Yesu. Mariko na Luka, wenyewe wakiwa hawakua katika kikundi cha Yesu, walikuwa katika kikundi cha wale waliokuwa na Yesu na walipatiana ambacho walikuwa wameambiwa na kufundishwa na mitume wa kwanza.

> *Ni vyema kusoma injil. Ni vyema kuanza na Mariko kwa kuwa kina hadithi za kusisimua, anza kujisomea injili wewe mwenyewe: angalao sura moja kila siku, na pia sura nyingi ukiweza.*

## Kumfahamu Yesu ni jambo la muhimu sana kwa kila mtu.

Kufahamu "Yesu ni nani" ni ya muhimu sana kwa kila mmoja katika uso wa dunia. Nyakati zijazo na hatima ya nafsi yako inategemea unaamini kuwa Yesu ni nani. Hakuwa mtu wa kawaida! Unapotambua yeye ni nani na aliyoyatenda, kama mtume Petro, maisha yako yatabadirishwa kwa ghafla!

Mtume Yohana alinakili ambaco Yohana mbatizaji alicho kisema kumhusu Yesu, "***yeye ajaye kutoka juu, huyo yu juu ya yote. Yeye aliye wa dunia, asili yake ni ya dunia, naye anena mambo ya duniani. Yeye jaye kutoka mbinguni yu juu ya yote. Yale aliyoyaona na kuyasikia ndiyo anayoshuhudia, wala hakuna anayeukubali ushuhuda wake. Yeye alieukubali ushuhuda wake ametia muhuri ya kwamba Mungu ni kweli."*** **Yohana 3:31-33.**

### Yesu alishuka kutoka mbinguni kushuhudia juu ya yale aliokuwa amesikia ya Mungu! Ikiwa unaupokea ushuhuda wa Yesu unakubaliana na Mungu aliye kweli!

Mtume Paulo anatuambia katika waraka wake kwa Warumi yakuwa kuna mambo mawili yenye umuhimu mkubwa mno ambayo tunapaswa kuyajua kwa njia ya ufunuo.
Paulo anasema "***kwa sababu ukimkiri yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako kuwa Mungu aliwafufua katika wafu, utaokoka"*** **Warumi 10:9**

Mambo hayo mawili muhimu ni yapi?

1) Yesu ni Bwana: Hii inamaanisha kwamba tumeyapatiana maisha yetu kwake na kwa hivyo yeye ni Bwana wetu. Hiyo inamaanisha kwamba yesu ndiye aliye na maisha yetu sasa.
2) Yesu alifufuka toka kwa wafu: hii inadhihirisha kwamba Yesu ni Mungu, na tukiamini hivyo tunaokolewa kwa Imani.

Unaamini Yesu alifufuka toka kwa wafu? ……………………..........................

Umemfanya Yesu Bwana kwa maisha yako?........................................................

Tunakuuliza uombe ombi lifuatalo: *Bwana Yesu, ninaamini ulishuka toka mbinguni; ninaamini ulikufa kwa sababu ya dhambi zangu; ninaamini ulifufuka kutoka kwa wafu, sasa nakuomba unisamehe dhambi zangu, uje kwa maisha yangu na uwe Bwana wa maisha yangu.*

Aya ya kukalili: ***"kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka"***
**Warumi 10:9**

**SOMO LA PILI**

# Yesu ni nani? maisha yake
## (sehemu ya kwanza)

**YESU ALIKUWA MTU MWENYE DAMU NA MWILI NA ALIKUWA NA MAMA.**

- **Yesu alizaliwa na mwanamke.**

“kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Miriamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu***”*** ***Mathayo 1:18***

***“***Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye alizaliwa na mwanamke***” Wagara 4:4***

- **Mtu huyu alikuwa hana baba wa hapa duniani. hakupatikana kwa njia ya kiasiri.**

“Malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto (Yesufu), akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu,” ***Mathayo 1:20***

**Yesu alikuwa aitwe Mwana wa Mungu tangu kuzaliwa kwake.**

**Anaitwa Mwana wa Mungu kwa sababu Roho wa Mungu alimpata katika tumbo ya Mariamu.**

**Mungu alifanyika kuwa mtu, akazaliwa kama mtoto.**

***“***Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu***” Luka 1:35***

**Mwana wa Mungu inamaanisha kwamba Yesu ni Mungu katika mwili**

**“Na bila shaka siri ya utaua ni kuu; Mungu alidhihiriswa katika mwili” 1Tim 3:16**

**MAMBO MATATU YA KIUNABII YA YESU HATA AKIWA MTOTO**

1. **YESU NI MUNGU AKITUOKOA!**

**Jina Yesu lilichaguliwa kwake kwa maana linamfunua: atakaye tuokoa kwa dhambi**.

“Naye Mariamu atamzaa mwana, nawe utamuita jina lake YESU, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao” ***Mathayo 1:21***

**Yesu ndilo jina la Mungu na ni kwa jina hilo tu ambapo unaweza kuokolewa na dhambi na adhabu!** Jina “Yesu” linamaanisha yeye ndiye mwokozi – kwamba yeye ni “wokovu wa Mungu” kwetu. Unapoliitia jina la Yesu, unamuita Mungu ambaye anaweza kuokoa!

**“**Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye, yote, kwa maana hapana **jina jingine** chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi **kuokolewa** kwalo”. ***Mdo 4:12***

2. **YESU NI MUNGU PAMOJA NASI!**

**Yesu alitimiza mambo yalioandikwa mamia ya miaka kabla aje ambayo ilituambia angekuwa "Mungu pamoja nasi"**

**"**hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamuita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi." ***Mathayo 1: 22-23***

3. **YESU NI MFALME!**

**Mamajuzi walikuja kutoka mbali kumtafuta Yesu. Waliona nyota mawinguni ambayo walijua ilikuwa ishara kwamba mfalme mkuu alikuwa amezaliwa, hata viumbe walikuwa wakionyesha matokeo haya ya ajabu ya huyu mfalme mkuu aliyekuja duniani.**

**"**Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia" ***Mathayo 2:2***

**Walipokuwa wakimtafuta mfalme huyu wakaulizia kwa viongozi wa wayahudi na wakawaambia mambo yaliokuwa yameandikwa na wazee wa zamani ambapo angezaliwa.**

**"**Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo iliyoandikwa na manabii, Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda; Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda, Kwa kuwa kwako atatoka mtawala Atakaye wachunga watu wangu Israeli" ***Mathayo 2:5*****-6**

**Kama mtoto, Yesu aliabudiwa nan a watu hawa walipompata! hii ni ya muhimu sana kwa maana tunapaswa kumuabudu Mungu pekee, sio mwanadamu.**

"Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia." ***Mathayo 2:11***

**Miaka mingi baadaye Yesu alimuambia shetani alipokua akimjaribu kwampa utamsujudia Mungu peke yake, Yesu alisujudiwa kwa kuwa ni Mungu.**

"Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake" ***Mathayo 4:10***

**Mfalme wakati wa Yesu' miaka ya kwanza ya utoto wake, aliyeitwa Herode, alitaka kumuua kwa maana alihofu kupoteza nguvu. Lakini Mungu alimlinda Yesu kumpa Yusufu (Baba mlezi wa Yesu) ndoto.**

"… Malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Msiri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amuangamize." ***Mathayo 2:13***

**Yesu alikua katika jamii katika Pahali palipoitwa Nazarethi ambayo ipo mpaka sasa.**

**"**Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti" ***Mathayo 2: 23***

## Maswali kutoka kwa Yesu katika maisha yake

**Je Yesu alikuwa ni mtu mwenye mwili na damu? Maandiko gani yanatangaza hivyo?**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**Kwa nini Yesu anaitwa Mwana wa Mungu? Onyesha andiko.**

…………………………………………………………………………..............................................

..........................................................................................................................

**Je ni halali kumsujudia Yesu? Je alisujudiwa wakati wa maisha yake duniani? Onyesha andiko.**

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

SOMO LA TATU

# Yesu ni Nani? - Maisha Yake

## (sehemu ya pili)

### YESU ALIKUA KAMA KIJANA KATIKA JAMII!

➔ **Yesu kama mtoto alikuwa mwenye nguvu katika tabia na roho.**

"Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake" ***Luka 2:40***

➔ **Katika umri wa miaka kumi na miwili, mabadiliko yalitokea!**

Yesu alitimiza kiwango kingine cha kukua ambapo alitaka kufahamu zaidi kumhusu Baba yake, Mungu!

Katika umri wa miaka kumi na miwili yesu alienda hekaluni (Mahali ambapo Wayahudi walikuwa wakiabudia Mungu) na akaanza kuuliza maswali mengi na kujibu maswali mengi kumhusu Mungu. Watu walishangazwa naye kwa sababu ya ufahamu wake uliokomaa. "***Nao wote waliomsikia walistaajabia fahamu zake na majibu yake"*** **Luka 2:47.**

Wakati Yesu alikuwa hekluni mama yake na Yusufu walienda nyumbani, walifikilia Yesu alikuwa nao. Mara wakatambua kuwa Yesu alikuwa hapatikani, na wakawa na hofu, walipompata hekaluni kwa masubuko wakamuuliza alikuwa akifanya nini. Hawakutambua hakika yeye alikuwa nani na akawajibu, "***Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa ilinipasa kuwemo katika nyumba ya Baba yangu? Nao hawakuelewa na neno hilo alilowaambia"*** **Luka 2: 49-50**

➔ **Baada ya hayo Yesu aliendelea kukua**

Kama kijana, Yesu alinyenyekea kwa Yusufu na miriamu. "Akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii… Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." ***Luka 2: 51-52***

➔ **Alikuwa pia na ndugu zake na dada zake na pia alikuwa ni seremala**

**"**Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu na ndugu yao Yakobo, na Yose, na Yuda, na Simoni? Na maumbu yake hawapo hapa petu?" ***Mariko 6: 3.***

### HATA HIVYO, YESU HAKUWA MTU WA KAWAIDA!

Alipofikisha umri wa miaka therathini Akaja kwa ubatizo katika mto wa Yordani na mbingu zikamfungukia alipokuwa hapa duniani! (***Mathayo 3:16)***

Hii ilimaanisha, kama mwanadamu, alikuwa amefikia kiwango cha ukomavu ambapo utimilifu wa Roho wa Mungu angaachiliwa kwake! Sasa alikuwa tayari kutembea katika uwajibikaji wote kama Mwana wa Mungu, akiwa na uwezo wa kumwakilisha babaye, Mungu, kikamilifu.

Kuanzia wakati huo ungemuona Yesu, unamuona Mungu katika utimilifu wake. Hiyo ndiyo sababu alitangazwa kuwa yeye ndiye MWANA WA MUNGU!

## Ubatizo wa Yesu

Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbigu zakamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.” ***Mathayo 3:16-17***

## Jukumu lake la kwanza lilikuwa ni kuyashinda majaribu ya shetani hapa duniani kama mtu

“Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi” ***Mathayo 4:1*** na pia ***Luka 4:1***

Yesu hakutenda dhambi! Alimshinda shetani kikamilifu kwa kuyashinda majaribu. Hii inatuonyesha kwamba sisi twaweza pia kupata ushindi juu ya ibilisi kwa msaada wa Mungu katika Kristo

## Adamu na hawa walishindwa kumshinda ibilisi

Pale mwanzo Adamu na Hawa walishindwa kuyashinda majaribu ya ibilisi lakini sasa kuna mtu aliyeshinda yote ambayo ibilisi alimrushia! Hakumuasi Mungu!

1. Alijaribiwa kwa vyakula baada ya kutokula kwa siku arubaine (40) – Jawabu Yake, “Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu” ***Mathayo 4:4***
2. Alijaribiwa kumjaribu Mungu kwa njia ya kiburi – Jawabu Yake, “Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako” ***Mathayo 4:7***
3. Alijaribiwa kwa kuahidiwa kupewa nguvu zote za ulimwengu endapo atamuabudu Ibilisi – Jawabu Yake, “Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake” ***Mathayo 4:10***

**“*Kisha Ibilisi akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia”* Mathayo 4:11**

## Yesu anaweza kuhusiana nasi katika udhaifu wetu na majaribu kwa kuwa alifanyika mwanadamu na amejaribiwa kama nasi pia.

“Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu” ***Waebrania 4:15***

## HUDUMA YA YESU

Akiisha jazwa Roho mtakatifu katika ubatizo wake na akiisha upokea ushindi dhidi ya ibilisi, Yesu alitoka jangwani na nguvu nyingi za kuwasaidia wengine – na pia wewe! ***“Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akaenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando”*** **Luka 4:14**

### i. Alipakwa na Roho wa Mungu

Upako huu ulimwezesha Yesu kuwasaidia watu wawe huru katika maisha yao, kushinda dhambi, kuwa na ushindi dhidi ya ibilisi na kuponywa magonjwa yote. Yesu alizungumza kuhusu upako aliokuwa nao katika Sunagogi zao katika Nazareti, ambao ulikuwa mji wake. ***“Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.***

***Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa"*** **Luka 4:18-19**

**ii. Alifundisha na mamlaka**

"Wakashangaa mno kwa mafundisho yake, kwa kuwa neno lake lilikuwa na uwezo" ***Luka 4:32***

**iii. Alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi**

**"**Naye Yesu alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako" ***Mariko 2:5***

**iv. Aliamuru pepo wachafu kuwatoka watu ambao walikuwa wameteswa.**

**"**Maana awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka" ***Luka 4:36***

**v. Aliwaponya watu aina yote ya magonjwa**

**"…**Na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu" ***Mathayo 4:23***

**vi. Alikuwa na mamlaka juu ya kifo**

"…Akalia kwa sauti kuu, Lazaro njoo huku nje! Akatoka nje yule aliyekufa…." ***Yohana 11:43-44*** na pia ***Luka 7: 11-17***

**vii. Aliabudiwa na watu**

"Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia…" ***Mathayo 8:2***

"Kisha [mtu aliyekuwa ameponywa upofu] akasema, Naamini Bwana! Akamsujudia." ***Yohana 9:38***

**viii. Alihubiri ufalme wa Mungu.**

"Naye alikuwa akizunguka Galilaya yote….na kuihubiri injiri njema ya ufalme" ***Matahyo 4:23***

## Huyu ni yesu katika maisha yake!

**Maswali kutoka kwa Yesu katika maisha yake:**

**Majina ya ndugu zake yesu ni yapi?**

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

**Ni nini kilicho tendeka mara tu Yesu alibatizwa? Mathayo 4:1**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Nguvu za Yesu zilitoka wapi? Luka 4:14**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Taja maeneo manane ya huduma ya Yesu:**

i. …………………………………………………………………………………………
ii. …………………………………………………………………………………………
iii. …………………………………………………………………………………………
iv. …………………………………………………………………………………………
v. …………………………………………………………………………………………
vi. …………………………………………………………………………………………
vii. …………………………………………………………………………………………
viii. …………………………………………………………………………………………

Aya ya kukariri**: "*Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akaenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando" Luka 4:14***

**SOMA LA NNE**

# Yesu ni nani? - Kifo chake (Sehemu ya kwanza)

## MUNGU ALIKUWA NA YESU!

- **Daima Yesu alitenda mema kwa watu**

**"…**jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu; naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye." ***Mdo.10:38***

- **Alikuja kuwahudumia watu na kuwasaidia**

"Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika…" ***Mariko 10:45***

- **Haya mambo yalikuwa thibitisho alikuwa mwana wa Mungu**

Hii ilikuwa kwa sababu alikuwa akitenda ambacho Mungu Baba yake alitenda. Yesu alisema, "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambaio amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo atendayo Mwana vile vile" ***Yohana 5:19***

## MUNGU ANA MPANGO KWETU KUPITIA YESU!

i. **Kuweka lawama ya dhambi za dunia juu ya Yesu.**

Yesu alikuja duniani kufa, kuchukua adhabu ya dhambi juu yake. Ilimpasa Yesu afe ili atuokoe kutokana na hukumu ya dhambi. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." ***Yohana 3:16.***

"Yohana amwona Yesu anakuja kwake, akasema, 'Tazama! Mwana - kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu" ***Yohana 1:29***

"Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki." ***Warumi 4:25***

ii. **Yalikuwa ni mapenzi ya Mungu Yesu afe mikononi mwa watu waovu**

"Mtu huyu (Yesu), alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi makamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua" ***Mdo 2:23***

Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake wakati wa huduma yake kwamba lazima angeuwawa, na ateseke mambo mengi.

"Imempasa Mwana wa adamu kupata mateso mengi, na kukataliwa na wazee na wakuu wa makuhani na waandishi, na kuuawa na siku ya tatu kufufuka" ***Luka 9:22***

"Tazameni, tunapanda kwenda Yerusalemu, na mambo yote yatatimizwa, Mwana wa Adamu aliyoandikiwa na manabii. Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa Mataifa, atafanyiwa dhihaka; atatendwa jeuri, na kutemewa mate; nao watampiga mijeledi, kisha watamwua; na siku ya tatu atafufuka" ***Luka 18:31 33***

## YESU ALISALITIWA!

### Mmoja wa wale thenashara

Yesu alikuwa ametumia miaka kumi na miwili na wanafunzi wake, akiwafundisha, akiwaandaa na akiwa Baba kwao, lakini kisha akasalitiwa na mmoja wa wale kumi na wawili

ambao walikuwa karibu naye. "Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti… Yeye aliyetia mkono wake pamoja name katika kombe, ndiye atakayenisaliti…Yuda, yule mwenye kumsaliti, akajibu, akasema, Ni mimi, Rabi? Akamwambia, Wewe umesema" ***Mathayo 26: 21-25***

## Wanafunzi wake walimwacha

Walimwacha kuteseka peke yake. Haya yaliandikwa katika maandiko mda mrefu kabla ya kutendeka. Lakini aliwaachia matumaini kwamba hatabaki akiwa amekufa! "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajiri yangu usiku huu; kwa kuwa imeandikwa, nitampiga mchungaji, na kondoo wa kundi watatawanyika. Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya" ***Mathayo 26:31-32***

## Hata Petro alimkana

Miongoni mwa wale watatu wa Yesu Petro alikuwa wa karibu sana; Yesu alikuwa ametangulia kusema kwamba atamkana mara tatu usiku huo. "Petro akajibu akamwambia, Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe. Yesu akamwambia, Amin, nakuambia wewe, usiku huu kabla ya kuwika jogoo, utanikana mara tatu" ***Mathayo 26:33-34***

## Haya yalitimia

Baadaye usiku huo wakati Petro alitambua aliyoyatenda akalia kwa uchungu. Alipoulizwa kama anamfahamu Yesu alijibu:

1. "Ee, mwanamke, simjui" ***Luka 22:57***
2. "Baadaye kitambo mtu mwingine alimwona akasema, Wewe nawe u mmoja wao. Petro akasema, Ee mtu, si mimi" ***Luka 22:58***
3. "Halafu, yapata saa moja, mtu mwingine alikaza kusema, Hakika na huyu alikuwa pamoja naye, kwa kuwa yeye pia ni Mgalilaya, Petro akasema, Ee mtu, sijui usemalo. Na papo hapo alipokuwa katika kusema, jogoo aliwika" ***Luka 22:59-60***

"Bwana akageuka akamtazama Petro. Petro akalikumbuka lile neno la Bwana jinsi alivyomwambia, Leo kabla hajawika jogoo utanikana mara tatu. Akatoka nje akalia kwa majonzi" ***Luka 22:61-62***

# YESU ALICHAGUA KUFA KUFUATA MPANGO WA MUNGU.

**Hakustahili kufa; alifanya hivyo kwa ajili yako!**

### Yesu alisumbuka kuhusu kulitimiza kusudi la Mungu

Yesu alichagua kulitimiza kusudi la Mungu, baada ya kusumbuka katika moyo wake. Alichagua kwenda kwa msalaba

Mungu akayajibu maombi yake kwa sauti kutoka mbinguni ikisema Mungu atatukuzwa [kufunuliwa] kwa mauti yake! "Sasa roho yangu imefadhaika; nami nisemeje? Baba, uniokoe katika sa hii? Lakini ni kwa ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii. Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, Nimelitukuza, Nami nitalitukuza tena" ***Yohana 12: 27-28***

### Yesu alijipatiana kwa mapenzi ya Mungu

Usiku kabla ya Yesu kuuawa aliomba na akajipatiana kwa kupitia mpango wa Mungu. Hapakuwa na njia nyingine ya kumwokoa mwanadamu! "Ee Baba, ikiwa ni mapenzi yako, uniondolee kikombe hiki; walakini sii mapenzi yangu, bali yako yatendeke" ***Luka 22:42***

### Mungu, kama mtu, alijinyenyekesha kufa msalabani!

Hakustahili kufa, alichagua. “Alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba” ***Wafilipi 2:8***

### YESU ALIKUWA MTU WA KAWAIDA

Ulipofika wakati wa kumshika Yesu, walihitaji ishara kumjulisha kando na wanafunzi wake. Hakuwa mtu spesheli wakutazamwa! Alikuwa mtu wa kawaida!
Hakuyavaa mavazi ya kifalme, wala hakuwa mtu wakipekee katika viwango vya dunia. “Yeye hana umbo wala uzuri; Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani” ***Isaya 53:2-3***
Yesu alisalitiwa kwa busu kwa kuwa hangetofautishwa na wanafunzi wake. Ilikuwa ni ishara kwa wale waliomkamata. “Na yule mwenye kumsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema, Nitakayembusu, huyo ndiye, mkamateni.” ***Mathayo 26:48***

## YESU ALIKAMATWA

### Walikuja na panga na marungu

Alikamatwa na watu wengi waliokuwa na panga na marungu. Mmoja wa wanafuzi wake alijaribu kumtetea, akilikata sikio la mmoja wao. **“**Basi, alipokuwa katika kusema, tazama, Yuda, mmoja wa wale Thenashara akaja, na pamoja naye kundi kubwa wenye panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani na wazee wa watu...Na tazama, mmoja wao waliokuwa na Yesu akanyosha mkono wake, ukaufuta upanga wake, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio” ***Mathayo 26: 47, 51***

### Yesu alimponya yule mtu ambaye sikio lake lilikuwa limekatwa!

Yesu hakuhofia maisha yake Zaidi lakini alifikiria kuwasaidia adui zake! Na Yesu alimkemea mwanafunzi wake kwa kufanya hivyo. “Akamgusasikio, akamponya” ***Luka 22:51***. “Ndipo Yesu akmwambia, Rudisha upanga wako mahali pake; maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga.” ***Mathayo 26:52***

### Angaliwaita malaika wengi waje wamsaidie

Yesu alijipatiana kwa mapenzi ya Mungu. Hakuzitumia nguvu zake zishizo za kawaida, lakini alitaka kubaki katika mapenzi ya Mungu. “Ama wadhani ya kuwa mimi siwezi kumsihi Baba yangu, naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? Yatatimizwaje basi maandiko, ya kwamba ndivyo vilivyopasa kujiri?” ***Mathato 26:53-54***

### Wanafunzi walimwacha

“Ndipo wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia” ***Mathayo 26:56***

### Siri ya Kristo kutufia

Yesu, aliyekuwa yuna namna ya Mungu kabla hajafanyika mwanadamu, kwa kukusudia alijinyenyekesha kushuka toka mbinguni na azaliwe duniani kama mwanadamu. Alikuwa Mungu lakini akawa mwanadamu, na kama mwanadamu hata kifo cha msalaba kwa watu wote. Uhakika wa kukamatwa kwake, majaribu na kusulibishwa zilikuwa za kutisha, lakini alitenda haya kwa kukusudia kwa sababu yetu sisi sote.

**Maswali kutoka kwa Yesu katika kifo chake:**

Yesu alipakwa na nini? ......................................................................

Ni nani alimsaliti Yesu? ……………………………………………..

Ni nani alimwacha alipo kamatwa? ……………………………………...

Ni nani alimkana mara tatu? ……………………………………………

Yalikuwa ni maamuzi ya Yesu kuruhusu auwawe? ……………………………

Ilikuwa vyepesi yeye kuamua? ……………………………………………..

Ni nini Yesu aliomba mara tatu katika shamba la Gethsemane?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**"Aya *ya kukariri: Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."* Yohana 3:16**

**SOMO LA TANO**

# Yesu ni nani? – Kifo Chake (Sehemu ya pili)

## YESU ALISINGIZIWA

### Viongozi wa watu walitafuta sababu za kumwua Yesu

"Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushahidi wa uongo juu ya Yesu, wapate kumwua" ***Mthayo 26:59***

### Aliletwa mbele ya kuhani Mkuu

Kuhani mkuu alikuwa ndiye mkuu wa ndini ya Kiyahudi kwa wakati huo na alikuwa na sehemu ya mamlaka kubwa. Mashahidi wa uongo walishuhudia juu ya Yesu, lakini Yesu alibaki kimya na hakujibu maswali yao.

"Wasiuone wangawa walitokea mashahidi wa uongo wengi. Hata baadaye wawili wakatokea, wakasema, Huyu alisema, naweza kulivunja hekalu la Mungu, na kulijenga kwa siku tatu. Kisha kuhani mkuu akasimama akamwambia, Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini? Lakini, Yesu akanyamaza." ***Mathayo 26: 60-63***

## YESU ALISHUHUDIA MBELE YA KUHANI MKUU

### Kuwa Kristo na Mwana wa Mungu

**"**Kuhani Mkuu akamwambia, Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu. Yesu akamwambia, Wewe umesema" ***Mathayo 26: 63-64***

### Ameketi katika enzi ya Mungu

Yesu alimwambia Kuhani Mkuu kwamba baadaye atamuona Yesu ameketi kwenye enzi ya Mungu. Hivyo ndivyo inamaanisha "**kuwa katika mkono wa kuume wa Nguvu"**

**"**Lakini nawaambieni, Tangu sasa mtamwona <u>Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume</u> wa <u>nguvu</u>, akija juu ya mawingu ya mbinguni" Mathayo 26:63

### Alisingiziwa kukufuru

Alipigwa na wakuu wa Wayahudi na walimkasirikia. "Amekufuru; mwaonaje ninyi? Wakajibu, wakasema, imempasa kuuawa. Ndipo wakamtemea mate ya uso, wakampiga Makonde; wengine wakampiga makofi." ***Mathayo 26:65-67***

## YESU KATIKA KOTI/MAHAKAMA YA PILATO

### 1. Yesu alinena na kiongozi wa Rumi, Pintius pilato

Yesu alimwambia Pilato kuwa yeye ni mfame. "Yesu akajibu, Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu…Wewe umesema, kwa kuwa mimi ni mfalme" ***Yohana 18:36-37***

### 2. Desturi wa kuwachilia mfungwa

Wakati wa sikukuu ya Pasaka ya Wayahudi, kulikuwa na desturi ya kumuachilia mfungwa kwa Wayahudi. Pilato akauliza umati wa wayahudini mfungwa yupi wangependa aachiliwe huru: Yesu ama Baraba. "Lakini kwenu kuna desturi ya mimi kuwafugulia mtu mmoja wakati wa pasaka; basi, mwapenda niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?" ***Yohana 18:39***

### 3. Umati ukamchagua Baraba

Baraba, mufungwa shugu aliyekuwa muasi, muuaji, mnyang'anyi ndiye aliyechaguliwa na umati afunguliwe. (**Yohana 18:39-40)**

### 4. Mateso ya Yesu

Pilato akampiga mijeledi na askari wa Kirumi wakamdhihaki na kumpiga pia. "Basi ndipo Pilato alipomtwaa Yesu, akampika mijeledi. Nao askari wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani, wakamvika vazi la zambarau. Wakawa wakimwendea, wakisema, Salamu! Mfalme wa Wayahudi! wakampiga makofi" ***Yohana 19:1-3***

### 5. Pilato hakuyaona makosa ya Yesu

Wayahudi walipiga kelele wakisema, "Musulibishe! Musulibishe! Pilato akawaambia, Mtwaeni ninyi basi, mkamsulibishe; kwa maana mimi sioni hatia kwake." ***Yohana 19:6***

### 6. Pilato aliogopa

Wayahudi wakamwambia Pilato kwamba Yesu alisema kuwa yeye ni Mwana wa Mungu. Hii ilimwogofya sana. Kisha akamuuliza Yesu maswali zaidi lakini Yesu aliendelea kunyamaza.
"Wayahudi wakamjibu, Sisi tunayo sheria, na kwa sheria hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu." ***Yohana 19:7***

### 7. Mamlaka ya Pilato yalikuwa yametoka kwa Mungu

Pilato alijaribu kuonyesha mamlaka yake lakini Yesu akafunua kwamba **mamlaka yote yako chini ya mamlaka ya Mungu. "**Basi Pilato akamwambia, Husemi nami? Hujui ya kuwa mimi nina mamlaka ya kukufungua, name nina mamlaka ya kukusulibisha? Yesu akamjibu, Wewe hungekuwa na mamlaka yo yote juu yangu, kama usingepewa kutoka juu." ***Yohana 19:10-11***

## YESU ALISULIBISHWA

### Pilato akampatiana Yesu asulibishwe

Hatimaye pilato akashawishiwa na Wayahudi wamsulibishe Yesu hata kama alikuwa hajaona makossa kwake. "Basi ndipo alipomtia mikononi mwao ili asulibiwe, nao wakampokea Yesu" ***Yohana 19: 16***

### Yesu akaubeba msalaba [mti wa hukumu]

Pahali pa kusulibiwa paliitwa "Golgotha", na hapo akasulibiwa. "Na walipofika mahali paitwapo Golgotha, yaani, Fuvu la Kichwa…Wakamsulibisha" ***Mathayo 27:33,35***

### Mashitaka yake yaliandikwa juu ya kichwa chake

**"**Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaka yake, yaliyoandikwa HUYU NI YESU, MFALME WA WAYAHUDI." ***Mathayo 27:37***

### Alisulibishwa katikati ya wahalifu wawili

Yesu aliomba msamaha wa wale waliomtesa na kumuudhi. Aliwapenda wanadamu mpaka mwisho! "Na walipofika mahali paitapwo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume, na mmoja upande wa kushoto. Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." ***Luka 23:33-34***

### Yesu akapaza sauti

Kwa kuwa Yesu alikuwa na uzito wa dhambi za ulimwengu juu yake, Mungu akamuacha afe, ili abebe hukumu kwaniaba yetu. “Mungu wangu Mungu wangu, mbona umenia?” ***Mathayo 27:46***

### Imekwisha!

Kazi aliyokuja kufanya Yesu ilikwisha! Hii ilikuwa kazi ya ukombozi, ambayo ingekamilishwa tu kwa kumwagika kwa damu. “Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema imekwisha!” ***Yohana 19:30***

## YESU ALIKUFA

### Yesu alifanyika dhambi kwa niamba Yetu

Ili Mungu aweze kuupatanisha ulimwengu na yeye, ilimbidi Yesu afe kwa niamba Yetu. Mungu anafanya amani nasi kupitia damu, iliyomwagwa na Yesu msalabani.

“Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makossa yao…Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye” ***2 wakorintho 5: 19,21***

“Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake…kwa damu ya msalaba wake.” ***Wakolosai 1:19-20***

### Yesu aliitoa roho yake kwa Mungu

“Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake.” ***Mathayo 27:50***

“Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu. Alipokwisha kusema hayo alikata roho.” ***Luka 23:46-47***

### Alikufa kwa sababu ya dhambi zetu

**“**Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko.” ***1 Wakorintho 15:3***

### Isaya alitabiri haya miaka mia saba kabla

Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, aijuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hakutumhesabu kuwa kitu. **Isaya 53:3**

### Ameyachukua masikitiko Yetu, huhuni na akafa kwa ajili ya dhambi zetu

“Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa Yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.” **Isaya 53: 4-5**

### Kupitia kifo cha Yesu sisi tunaweza kumrudia Mungu

“Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na BWANA ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote…Utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi.” ***Isaya 53:6, 10***.

- **Mungu alikuwa na Yesu**
- **Mpango wa Mungu ulikuwa Yesu afe mikononi mwa watu waovu**
- **Yeye hana umbo wala uzuri**
- **Alisalitiwa na akakanwa na wale waliokuwa karibu sana naye**

- **Hakustahili kufa lakini alichagua**
- **Alishuhudia mbela za wayahudi na Warumi**
- **Alisingiziwa**
- **Alipigwa, kuteswa na kusulibiwa.**
- **Alipaza sauti**
- **Alikufa**
- **Alijeruhiwa kwa dhambi zetu**
- **Nafsi yake ilikuwa ni dhabihu ya kutuletea amani na Mungu**

## Huyu ni Yesu katika kifo chake!

### Maswali kutoka kwa Yesu katika kifo chake

**Ni nini Yesu alifanya kwa yule mtu alikuwa akimkamata? Hii inaonyesha nini kuhusu Yesu?**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………..

**Pilato alipata kosa lolote kwa Yesu?**

……………………………………………………………………………

**Watu walitamani kuona nini ikimtendekea Yesu**?...................................................................

**Unafikiria Yesu alimaanisha nini aliposema,**

***imekwisha***?..........................................................................................................................

...................................................................................................................................

**Maneno ya Yesu ya mwisho kabla yeye kufa yalikuwa**

**yapi**?...............................................................................................................................

.............................................................................................................................

**Aya ya kukariri:** ***"Na walipofika mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, ndipo walipomsulibisha yeye, na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume, na mmoja upande wa kushoto. Yesu akasema, Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." Luka 23: 33-34***

SOMO LA SITA

# Yesu ni nani? Kufufuka kwake

**(Sehemu ya kwanza)**

## YESU, KAMA MWANADAMU, ALIKUFA NA AKAZIKWA!

- **Yesu alilazwa kaburini na mtu mmoja tajiri aliyemwamini Yesu**

“Hata ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu…Yusufu akautwaa mwili, akauzonga- zonga katika sanda ya kitani safi, akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akavingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi.” ***Mathato 27:57-60***

- **Haya yalikuwa yametabiriwa na nabii isaya pia**

“Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya- Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.” ***Isaya 53:9***

- **Wale waliokubaliana na kufa kwake, walihofia yakuwa atafufuka kutoka kwa wafu!**

Viongozi wa dini aliogopa aliyokuwa ameyasema Yesu kuhusu kufufuka toka kwa wafu. “Hata siku ya pili, ndiyo iliyo baada ya Maandalio, wakuu wa makuhani, na Mafarisayo wakamkusanyikia Pilato, wakisema, Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, baada ya siku tatu nitafufuka.” ***Mathayo 27: 62-63***

- **Waliomba walinzi wawekwe kwenye kaburi**

Walitaka kuhakikisha hapana mtu atauiba mwili wa Yesu. Pilato aliwauliza wafanye vyovyote wawezavyo kuulinda. “Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu. Pilato akawaambia… nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo. Wakaenda, wakalilinda kaburi salama, kwa kulitia lili jiwe muhuri, pamoja na wale askari walinzi.” ***Mathayo 27:64-66***

- **Yesu kama mwanadamu alikuwa kaburini siku tatu usiku na mchana**

Hii ilionyeshwa kiunabii kupitia mfano wa maisha ya Yona ambaye aliishi mamia ya miaka kabla ya Yesu. Yona ndiye aliyekuwa amemezwa na samaki mkubwa. Kitabu katika agano la kale kiitwaccho Yona kinasimulia hadithi hii.

“Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndiyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.” ***Mathayo 12:40***

- **Wanawake wawili walikuja kuiona kaburi siku ya tatu baada ya kifo chake**

**“**Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.” ***Mathayo 28:1***

- **Kifu hakingemshika Yesu!**

Lile jiwe lililowekwa kaburini lilivingirishwa! “Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jiwe, akalikalia.” ***Mathayo 28: 2***

## YESU AMEFUFUKA!

### i) kaburi lilikuwa tupu

Malaika waliongea na wanawake ambao walienda kuuangalia mwili wa Yesu. “Wakaingia, **wasiuone mwili wa Bwana Yesu**. Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajiri ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta; nao walipoingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hata nchi, hao waliwaambia, ‘**Kwanini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka!”** ***Luka 24:3-6***

### ii) Yesu alionekana na mashahidi!

**Mariamu Magdalene** alikuwa wa kwanza kumwona Yesu baada ya kufufuka. “Naye alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.” ***Mariko 16:9***

Wanafunzi hawakumuamini Mariamu. “Huyu akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia. Walakini hao waliposikia kama yu hai, naye amemuona, hawakusadiki.” ***Mariko 16:10-11***

**Yesu aliwatokea wengine wawili** wakitembea njiani. “Baada ya hayo akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.” ***Mariko 16:12***. Wanafunza hawakuwaamini hao wawili pia! “Na hao wakaenda zao wakawapa habari wale wengine; wala hao hawakuwasadiki.” ***Mariko 16:13***

### iii) Yesu aliwatokea wanafunzi!

Yesu aliingia chumbani pasina kutumia mlango! Walitishika na wakadhania kuwa ni roho. “Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho.” ***Luka 24:36-37***

### iv) Yesu alikuwa mtu wa kawaida, sio roho!

Yesu **aliwaonyesha arama** katika mwili wake na akawauliza wamguze kuona kwamba ndiye! “Akawaambia, mbona mnafadhaika! na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo.” ***Luka 24:38-39***

Yesu **alikula chakula nao,** akiwaonyesa kuwa mwili wake ulikuwa wa kawaida! “Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, Mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao.” ***Luka 24:41-43***

### v) Yesu aliwatokea wengi

Yesu alifufuka katika wafu na alionekana na watu wengi. Katika tukio moja alionekana na kikundi cha watu mia tano kwa wakati mmoja!

“Na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; na kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenashara; baadaye **aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja;** katika hao

wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote. Na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi (Paulo)…" ***1Wakorintho 15:4-8***

## YESU ALIFUFULIWA KATIKA WAFU

### Kutufanya wenye haki kama watu ambao walikuwa wawajatenda dhambi!

Alifufuliwa kwa sababu ya kufanywa haki kwetu, akitufanya huru na dhambi ili tuishi maisha mapya. "Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki." ***Warumi 4:25***

### Kutupa maisha mapya!

Kupitia kuamini na kubatizwa katika jina la Yesu tunapokea maisha yale yale na nguvu zile zile zilizomfufua katika wafu! Tunaishi kwa maisha yake! "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima!" ***Warumi 6:4***

### Maswali kuhusu Yesu katika kufufuka kwake

**Yesu kama mwanadamu alikufa?**.....................................................................................

**Alizikwa wapi?**...........................................................................................................................

**Kwa nini watu walitaka walinzi wawekwe katika kaburi ya Yesu?**

..........................................................................................................................

**Wakati wanawake walienda kuona mwili wa Yesu, walitambua nini? Onyesha kwa maandiko**…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**Ni nani alikuwa wa kwanza kumwona Yesu alipofufuka katika wafu**?

......................................

**Baada ya kufufuka, Yesu alifanya nini kuonyesha ya kwamba alikuwa na mwili halisi?**

..................................................................................................................................................

.........................................................................................................................

**Ni idadi ipi ya watu wengi ambao Yesu aliwatokea mara moja? 1 Wakorintho 15:6**

……………………………….

**Aya ya kukariri: "*Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki" Warumi 4:25***

**SOMO LA SABA**

# Yesu ni Nani? Kufufuka Kwake

**(Sehemu ya pili)**

## YESU YU HAI LEO! YUKO WAPI SASA?

**Yesu ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu mbinguni.**

Hapa ndipo Pahali pa mamlaka kamili juu ya vitu vyote mbinguni na duniani! “Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.” ***Mariko 16: 19***

“kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu…” ***Waefeso 1:19-21***

### YESU ANAFANYA NINI SASA?

1. **Yesu anatawala kama mfalme juu ya mbingu yote na dunia yote.**

Hii inamaanisha kwamba Maraisi wote, mawaziri wakuu, wafalme na maliwali wote wanawajibika kwake. Yeye ni Mfalme!

“Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia” ***Ufunuo 1:5***

“Mungu sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu…Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.” ***Matendo 17: 30-31***

“Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.” ***Mathayo 28:18***

2. **Yesu yuko pamoja na wale wanaohubiri habari njema**

Wanafunzi wa Yesu wanatakiwa kuhubiri habari njema ya maisha yake, kifo, kuzikwa na kufufuka. Anafanya kazi nao kwa kufanya ishara kubwa kuthibitisha ukweli wa neno lake. “Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amen!” ***Mariko 16:20***

“Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amen!” ***Mathayo 28:19-20***

3. **Yesu alimtuma Roho wake**

Yesu alimtuma Roho wake akae na wale wote wanaoamini na kumtii. Unaweza kupokea Roho Mtakatifu na ujazwe na maisha yake na nguvu leo! “Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.” ***Luka 24:49***

“Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kwajilia juu yenu Roho Mtakatifu.” ***Matendo 1:4-5, 8.***

“Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio.” ***Matendo 5:32***

4. **Yesu anapokelewa Mbinguni.**

Yesu anaendelea kupokelewa mbinguni mpaka vitu vyote virejeshwe kulingana na mpango wa kwanza wa Mungu. "apate (Mungu) kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu." ***Mdo 3: 20-21***

5. **Yesu anangojea mpaka adui zake zote watakapokuwa chini ya miguu yake.**

Adui wa mwisho kuangamizwa atakuwa ni mauti yenyewe. Mungu atakuwa na watu wake wakamilifu ambao adui zake zote hawatawaharibu wala kuwadhuru tena. "Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti."***1 Wakorintho15: 25-26***

"Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake." ***Waebrania 10: 12-13***

"Hawatadhuru wala kuwataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari." ***Isaya 11:9***

## MATOKEO YA MWISHO YATAKUWA KILA MMOJA ATAJUA NI NANI ANAYEHUSIKA

"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba." ***Wafilipi 2:9-11***

**Mungu anataka uamini kwamba alimfufua Yesu katika wafu!**

- **Ukiamini, utaokoka**
- **Unaweza kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Wake**
- **Unaweza kupokea nguvu za Roho Mtakatifu**
- **Unaweza kuishi maisha mapya, kwa nguvu za kufufuka kwa Yesu**

- **Yesu alikufa akazikwa**
- **Kifo hakingemshika**
- **Amefufuka katika wafu**
- **Alioneka na mashahidi waliomwona**
- **Aliwatokea wanafunzi wake**
- **Alifufuka na mwili wa kweli – hakuwa roho tu**
- **Aliwatokea wengi**
- **Yuko mkono wa kuume wa Mungu**
- **Anatawala mbinguni na duniani**
- **Anafanya kazi na wale wanahubiri injili**
- **Anamtuma Roho wake kuishi ndani ya wale wanaomuamini na kumtii**
- **Anangonjea mpaka maadui wake washindwe**

## Huyu ni Yesu aliyehai kutoka kwa wafu!

## Maswali kutoka kwa Yesu Aliyefufuka – Sehemu ya pili

**Anathibitisha injili inayohubiriwa kwa jinsi gani? Mariko 16:20**

……………………………………………………………………………………………………

**Ni kipawa gani ambacho Yesu huwapatia wale wanaomuamini na kumtii? Matendo 1:4-8**

……………………………………………………………………………………………………

**Ni adui yupi atakayeharibiwa wa mwisho? 1wakorintho 15:26**

……………………………………………

**Yesu anafanya nini sasa? Andika mambo matano anayoyafanya**

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………………………
5. ………………………………………………………………………………………

***Aya ya kukariri. "Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake." Waebrania 10: 12-13***

**SOMO LA NANE**

# Ukweli Uliofunuliwa

## UKWELI KUHUSU YESU

### 1. Yesu hakuwa mtu wa kawaida

Hata kama Yesu alikuwa mtu, hakuwa mtu wa kawaida. Alikuwa "***mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote*"** *na* ***mfano wa Mungu asiyeonekana" Wakolosai 1: 15.*** Mtume Paulo alisema ya kuwa huyu Yesu ni "***Bwana kutoka mbiguni." 1 Wakorintho 15:47***

### 2. Yesu ni Mungu katika mwanadamu

Kuna siri kubwa ya kufunuliwa katika Yesu.Ukweli ni kwamba mimba yake ilipatikana kwa njia ya kiungu kwa Roho Mtakatifu, akaishi maisha makamilifu katika uhusiano wake na Mungu na wakati wote alikuwa mtiifu kwa Mungu inatuonyesha ya kwamba Alikuwa wa asili tofauti na mwanadamu wa kawaida. Yesu ni Mungu katika mwanadamu!

*"**Na bila shaka siri ya utaua ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili."*** **1 Tim.3:16**

Siri ni kuwa Mungu alifanyika mwanadamu! Hii ndio inamaanisha kumuita Yesu "Mwana wa Mungu". Yesu alikuja kumfunua Mungu ni nani. Kumfahamu Yesu ni kumfahamu Mungu!

### 3. Ukimwona Yesu, umemwona Mungu!

Ukimwona Yesu kuwa ni nani, umemwona Mungu! Yesu alisema kwa mmoja wa wanafunzi wake, Filipo***, "Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Fillipo? Alieniona mimi amemwona Baba…"*** **Yohana 14:9**

### 4. Mungu alifanyika mwanadamu azichukue dhambi zetu

Mtume Yohana pia anasema kwamba "***Yeye [Mungu] alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake" 1Yohana 3:5*** Mungu alifanyika mwanadamu kusudi aziondoe dhambi zetu. Alifanya haya kwa kujitoa kama sadaka msalabani. Aliamua kuchukua dhambi zetu, uasi, maumivi, chuki, uchungu, hukumu na aibu juu Yake na kubeba hukumu iliyotupasa. Alikufa kwa niaba yetu.

***"Bali Mungu aonyesha pendo lake mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."*** **Warumi 5:8**

### 5. Yesu aliangamiza nguvu za kifo kwa kufufuka katika wafu!

Sio kwamba Yesu alikufa tu, alifufuka katika wafu, akituonyesha ushindi Wake dhidi ya kifo kwa maana hangebaki mtu aliyekufa. Kifo kinawashinda tu wale wanaotenda dhambi "***kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" Warumi 6:23,*** lakini Yesu alikuwa hana dhambi. Siku tatu baadaye alikuja na akawa ameketi mkono wa kuume akiwa juu ya yote. Na ***"aliyabatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile injili"*** **2Timotheo 1:10**

### 6. Ni wakati wakubadirisha jinsi unavyofikiria kumhusu Yesu!

Mungu sasa ***"anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu [wayageuze mawazo], kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu."*** **Matendo 17:30-31**

7. **Ni wakati wa kujua ukweli kumhusu Yesu ni nani na kumwamini Yeye**

Watu wana mawazo tofauti kumhusu Yesu. Ukweli ni kwamba Yeye ni Mungu katika mwili na kwamba Yeye ni mfalme ambaye anatawala yote: ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Hakika alikuja ulimwenguni na akaonekana, akasikika na akapapaswapapaswa (**1Yohana 1:1**). Yohana anasema ukiamini Yesu ni Kristo [Mfalme], Mwana wa Mungu, [Mungu katika mwili] kisha utapata UZIMA katika Jina Lake.

**Ukitaka uzima kamili, unahitaji Yesu!**
**Mwamini Yeye!**
**Uamini ushuhuda ambao amepatiana wa Mungu!**
**UZIMA utainia ndani yako!**

**Maswali**

**Siri ya utauwa ni ipi? 1Timotheo 3:16** andika mambo sita:

**1)** ………………………………………………………………………………………

**2)** ………………………………………………………………………………………

**3)** ……………………………………………………………………..........................

**4)** ………………………………………………………………………………………

**5)** ………………………………………………………………………………………

**6)** ………………………………………………………………………………………

**Yesu alisema "ukiniona mimi, umemwona** ………………………………………………

**Ni kwa nini Mungu alifanyika mwanadamu? 1Yohana 3:5** …………………………………..

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

**Ni nini Mungu anaamuru kila mtu ulimwenguni kufanya sasa kwa maana Yesu alikufa na akafufuka? Matendo 17: 30-31**

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

***Aya ya kukariri: "Yesu akamwambia, mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?" Yohana 14:9***

**SOMA LA TISA**

# Nitaenda wapi kutoka hapa?

***Yesu anataka kuingia katika maisha yako!***
***Ni wakati wa kupokea ufunuo wa Yesu!***
***Ni wakati wa kukutana na yeye kwa hakika!***

### Yesu ni hakika, sio wazo

- Yesu sio wazo ama maungamo ya mapokezi ya dini **(Waefeso 2:20)**
- Yesu ni mtu anayeishi hakika ambaye yuko hai leo **(1Wakorintho 15:45)**
- Yesu ni hakika na Yeye ni Mungu **(Yohana 20:28)**
- Unapokuja kwake haujiungi na idara, muungano ama kikundi cha kibinadamu **(1Petro 2:4-5)**
- Unakuja kwa Mungu aliyekufanya na kukuumba na kukufanya kwa mfano wake **(Mwanzo 1:26-27)**

### Hauwezi kujificha kutoka kwa Mungu

Haina maana kujaribu kujificha kutoka kwa Mungu. Yeye ni hakika na kama unamwamini ama la Yeye anabaki vile; habadiriki **(Waebrania 13:8).** Anakuona, anakujua na anakupenda kiundani (**Yeremia 31:3),** na anataka kuingia ndani yako **(Wagalatia 2:20).**

### Tumaini la kweli na utosherevu zimo ndani ya Yesu, Mungu wa upendo na nguvu.

Watu wote wanajijaza na kitu. Wengine wanajijaza na madawa, pombe, filamu, mahaba, ndini za uongo, uzushi, mapokezi na filosofia. Vitu hivi vinaweza kutosheresha tamaa yako kwa mda lakini mwisho wake ni uharibifu, kuvunjika kwa mahusiano, majeraha na upweke. Vinatokana na ubinafsi na kupenda tu kujifurahisha wenyewe. Hazipatiani tumaini ambalo liko katika injili.

- ***Tumaini la injili ni kwamba unaweza kuishi <u>maisha tofauti</u>.***
- ***Ni maisha ambayo <u>yana nguvu zile zilizo</u>mfufua Yesu katika wafu.***
- ***Uhakika wa injili ni kuwa unaweza kuingia katika maisha mapya ambayo <u>yanadumu milele.</u>***
- ***<u>Upendo na nguvu zinaachiliwa</u> katika maisha yako unapompokea Mungu ambaye ni upendo na Nguvu.***

## SAULI – MUUAJI WA WAKRISTO, KWA PAULO – MTUME WA YESU

### Sauli, mtu aliyechukia wakristo

Mda Fulani baada ya Yesu kufufuka katika wafu, palikuwa na mtu aliyeitwa Sauli ambaye kabisa aliwachukia wale waliomwamini Yesu. Sauli alihusika kumuua Stefano, mfia Imani wa kwanza wa Yesu **(Matendo 7:58).** Alianza kuwashika waumini na kuwaweka gerezani **(Matendo 8:3).** Alikuwa mtu wa dini aliyefikiria ya kuwa anamjua Mungu na akajipatiana katika kuwashika na kuwaua watu waliomgeukia Yesu kwa mioyo yao.

### Sauli "ghafla" alikutana na ukweli – Matendo 9:3-5

Siku moja alikuwa na wakati wa mabadiriko. Huu ndio wakati ambapo kitu kwa "ghafla" kinatendeka cha kugeuza hatima yako yote. Alikuwa njiani akienda kuwakamata watu katika mji walioamini Yesu wakati, GHAFLA, NURU KUTOKA MBINGUNI ILIMGONGA! Ilimgonga mpaka chini na mara akakutana na uhakika wa Mungu. Akasema, ***"U nani wewe, Bwana?"***

### "Mimi ndimi Yesu" – Matendo 9:5

Sauti ikajibu, "***mimi ndimi Yesu".*** Mtu huyu aliwachukia watu waliomwamini Yesu. Hakuami kwamba Yesu ni Mungu lakini kwa GHAFLA alikutana na uhakika na ukweli. Alijua kwamba ukweli huu ulitokana na Mungu kwa kuwa alisema, "***U nani, wewe Bwana?"***. Alimwita Bwana, lakini hakumjua alikuwa nani. Alimwamini Mungu, lakini alikuwa hajajua Mungu ni nani.

### Sauli mtu aliebadirika – Matendo 9:6 -18

Lakini sasa ulimwengu wake wote ulikuwa umebadirika. Alipofuka katika asili kwa siku tatu kutokana na tukio hilo lakini kwa mara ya kwanza katika maisha yake aliona uhakika kabisa.

### Aliona kwamba Yesu ni Mungu! – Matendo 9:20

Kama matokeo ya ufunuo huo, aliacha kupenda kuwaua Wakristo; alijazwa na Roho wa Mungu na akabatizwa katika jina la Yesu kuoshwa dhambi zake zote – kuoshwa uasi wake kinyume cha Mungu (Matendo 22:16). na si hivyo tu, Mungu alimtumia kufanya Yesu ajulikane katika dunia. Alijulikana kama Paulo na akawa Mtume wa Yesu, akitumwa kwa watu wengi kutangaza uhakika wa Mungu.

***YESU ALIINGIA NDANI YA PAULO! YESU ANATAKA KUINGIA NDANI YAKO!***

- **Yesu amechua ushukani**

Ukweli ni kwamba Yesu ni Mfalme – amechukuwa ushukani. Sio wewe! Yeye ni mkuu kuliko wewe na aliviumba vyote.

- **Anapatiana msamaha**

Atakupatia msamaha kama utampokea lakini ukimkataa unajihukumu kwa kuziweka dhambi zako.

- **Unamhitaji Yesu!**

Sio wakati wa kuendelea kuyachezea maisha yako. Ni wakati wa kumaanisha na maisha yako**. Unamhitaji Yesu!** Unamhitaji akuokoe kutokana na kujiangamiza mwenyewe. Unamhitaji akuokoe kutokana na kujindanganya katika maisha na kuishi maisha ya ubinafsi ukijifurahisha. Iwapo wewe ni tajiri ama maskini, mzima au mgonjwa, unahitaji ufunuo wa Yesu ili uone uhakika wa maisha.

### NI WAKATI WA KUPOKEA MAISHA MAPYA

- Ni wakati wako wa kuzaliwa mara ya pili; kuzaliwa kutoka mbinguni na kupokea ufunuo wa Yesu.
- Liitie jina la Bwana Yesu na utaokoka; Mungu atakuokoa na uasi na kutomtambua.
- Atakupa maisha mapya na Yesu atakuja na kuishi katika maisha yako kwa Roho Mtakatifu.

### Anza na kuongea na Mungu

Anza kuongea na Mungu na uwe wazi kwake. Unaweza kuona kama ni vingumu kwa maana utatambua kuwa yeye ni mwema sana na kwa kulinganisha wewe ni mchafu ndani. Unapotambua jinsi Mungu alivyo mwema akilinganishwa nawe, usihofu lakini muombe akusamehe. Ndiposa Yesu alikufa: ili Mungu ayasamehe maovu uliyoyatenda kwa maisha yako na aanze kukubadirisha na kukupa Roho Mtakatifu.

### Kisha tii maagizo yake na ubatizwe

Usikawie! Baada ya Sauli kukutana na Yesu na kuamini kuwa ni Mungu, alipata kubatizwa kwa Jina la Kristo Yesu. Sauli aliambiwa, "***basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako ukuliitia jina lake."*** **(Matendo 22:16)**

Kubatizwa ni kuyapitia ambayo Yesu aliyapitia– kifo, kuzikwa na kufufuka! Tunapaswa kuingia ndani ya maji kuunganishwa na Yesu katika kifo na kuzikwa na kutoka kwa maji kuunganishwa na Yesu katika maisha ya kufufuka! Ni kuchagua kufa katika maisha ya kale na kufufuka katika maisha mapya! Hii itakusaidia kuishi katika maisha mapya, maisha ya Yesu! **(Warumi 6: 3-14)**

### Kuwa kama Yesu

Wakati Yesu alibatizwa **mbingu zilifunguka** na **Roho wa Mungu akashuka** na akakaa juu yake na **sauti ikasikika** ikimtangaza kuwa Mwana wa Mungu

### Wakati unabatizwa

- Dhambi yako inaondolewa kabisa
- Mbigu zitakufungukia;
- Utapokea nguvu za Roho wa Mungu
- Utapata kuisikia sauti yake kukufariji na kukuelekeza katika maisha yako!

**Maswali:** tafadhari jibu maswali haya kwa kushiriki ushuhuda wako:

a) Ulikuja aje kumjua Yesu wewe binafsi?

b) Unaweza kuongea na jamii yako na marafika zako juu ya Yesu? Shiriki ushuhuda.

c) Umeshabatizwa tangu uamini? Shiriki ushuhuda wa ubatizo wako.

d) Baathi ya watu hubatizwa kabla ya kumuamini Yesu. Kama ndivyo mambo yalivyo huyu mtu anatakiwa kubatizwa tena baada ya kuja katika imani ndani ya Yesu. Haya yalitendeka katika Biblia katika Matendo 19:1-7. Tafadhari sema kitu kuhusu haya.

**Ninaomba kwamba uone uhakika wa Mungu katika Yesu!**
**Ninaomba upate ujuzi wake katika uhakika**
**na uzaliwe mara ya pili katika maisha mapya ya kufufuka kwake!**
**Naomba upate ujuzi na furaha ya kuwa umesamehewa dhambi zako**
**na kutembea katika maisha mapya na Yesu!**

**SOMO LA KUMI**

# Biblia ni nini?

## Biblia ni:

- Neno la Mungu kwa mwanadamu

- Mkusanyiko wa vitabu 66 kitabu kikubwa kikiwa Zaburi – sura 150 ndefu [hakika mkusanyiko wa nyimbo] – na vitabu vinne (Filemoni, 2 Yohana, 3 Yohana, Yuda) zikiwa kurasa moja.

- Mkusanyiko wa maandiko matakatifu yanayopatianwa na Mungu kupitia Roho wake kwa watu watakatifu wa zamani. "***Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu"*** **2 Petro 1:21**

- Inaitwa maandiko na maandiko yote yamepeanwa kwa pumzi ya Mungu "***Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu"*** **2Timotheo 3:16**

### Ni nani aliandika Biblia?

- **Muandishi wa kwanza** wa Biblia alikuwa Musa, nabii mkubwa wa Mungu aliyewaongoza waisraeli kutoka utumwa katika Misri katika Karne ya 15 Kabla ya Yesu.
- **Musa** aliviandika vitabu vitano vya Biblia ***[Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu***, ***Kumbukumbu la torati***] baada ya kutumia siku arobaini mchana na usiku katika uwepo wenye utukufu wa Mungu kibinafsi katika mlima mtakatifu. Hakula wala kunywa kwa hizo siku arobaini kwa sababu alitwaliwa kabisa na Roho.
  **"*Naye alikuwa huko pamoja na BWANA siku arobaini na masiku yake; hakula chakula, wala hakunywa maji. Naye akaandika katika hizo mbao, hayo maneno ya maagano, hizo amri kumi." Kutoka 34:28***

### Kitabu cha mwanzo ni kitabu cha mianzo

Ulikuwa ni wakati ambapo Musa alikuwa na Mungu ambapo Mungu alimfunulia Musa kitabu cha mwanzo.
Inashughulikia:

- Uumbaji wa dunia, jua, mwezi na nyota;
- Historia ya mwanadamu kama 4000 kabla ya Yesu wakati ambapo Mungu aliumba wazazi wetu Adamu na Hawa
- Inamalizia karne ya 19 kabla ya Yesu wakati Yakobo, baba ya makabila kumi na mawili wa Israeli walienda Misri kwa sababu ya njaa katika nchi.

Baada ya Musa, Manabii wengine, makuhani, na wafalme kama wawili na maliwali waliandika sehemu hiyo ingine ya Agano la kale, ***lakini kwa uhakika Mungu ndiye muandishi wa vitabu vyote vya Biblia!***

Kuna vitabu 39 katika agano la kale na vitabu hivyo vilikuwa vimeandikwa mnamo 400 Kabla ya Kristo.
Kuna taklibani ya watu 44 ambao waliandika vitabu bali bali za Biblia kwa aidi ya miaka 1500. Yashangaza, vitabu vyote vya Biblia vyatiririka pamoja, zikitupa ufahamu wa Mungu wa ndani.

## AGANO JIPYA

### Injili

Agano la kale linabeba vitabu 27: vitabu vinne vya **Injili, Mathayo, Mariko, Luka, Yohana,** ambazo ni ushuhuda wa yale Yesu alisema na kutenda ikihusisha ***uhakika wake usio wa kawaida kuhusu kuzaliwa kwake na kufufuka kwake katika wafu.***

### Matendo ya Mitume

Injili inafuatwa na kitabu cha **"Matendo ya mitume"** ambayo ni historia ya kusisimua ya mwanzo wa kanisa: jinsi watu maelfu walibadirishwa kwa kuamini ujumbe wa injili iliyohubiriwa na mitume ambao walikuwa wamechaguliwa na kufunwa na Yesu.

Katika **Injili** na **Matendo** ***kuna ishara za kiungu, maajabu ya kupita kawaida, uponyaji na miujiza na ukombozi kutoka kwa roho wachafu.***

### Nyaraka

Kisha pama **"nyaraka**" 21 ama **"barua"** zilizoandikwa na Mitume wa Yesu. Nyaraka zinaeleza imani ya Mkristo na kanisa. ***Ni ya kushangaza jinsi kanisa la Agano Jipya lilikuwa tofauti na "Makanisa" tunayoyaona katika mataifa leo.***

### Ufunuo

Kitabu cha mwisho cha Biblia ni "**Ufunuo wa Yesu Krito [Masihi]". Ufunuo 1:1**

Kitabu cha ufunuo ndicho kingumu sana katika Biblia kwa maana ni msururu wa maono ambayo Yohana aliyaona kutoka mbinguni.

### Ya Kale na Jipya pamoja

- ***Agano Jipya inapatikana katika agano la kale***
- ***Agano la Kale limetimizwa katika Agano Jipya***
- ***Agano la Kale na Agano Jipya zinapatana vyema, zikifanya moja iliyo kamili.***

### Biblia ni kitabu cha Ufunuo

Biblia inazungumza na mamlaka ambayo haina kitabu kingine. vipo vitabu vingine nyigi vya kiungu ambavyo vinafundisha kitu cha Mungu na himaya ya Rohoni. Lakini Biblia ni kitabu cha ufunuo waliopatiwa wanadamu na Mungu ili tupate "**Kumjua Yeye aliye tangu mwanzo" (1Yohana 2:12-14),** hivyo ni, Yeye aliye muumba wa vitu vyote na ametuumba ili tuwe kama Yeye.

- ***Biblia ni kitabu wazi;***
- ***Kila mtu anaweza kusoma Biblia***
- ***Mungu atasema nawe kupitia Biblia kwa Roho Wake. Huu ndio muujiza wa Biblia.***
- ***Unaweza kumjua Mungu kupitia neno lake lililoandikwa katika Biblia.***

### Maswali

**a)** Umeshawahi kusoma Biblia yote?

**b)** Huwa unafuata mpango uliowekwa wa kusoma? Sema kitu

**c)** Unatumia nakala gani ya Biblia?

**d)** Unalo swali lolote kuhusu Biblia?

*Anza kusoma Biblia wewe mwenyewe. BIBLIA imeandikwa kwa kila mtu.*
*Ni kitabu cha Mugu kilichoandikwa kwa sababu yako, kwako.*
*Anza kusoma Agano Jipya, ukianzia injili ya Mathayo.*
*Soma hata kama ni sura moja kwa kila siku, na uzidishe unavyowezeshwa.*
*Mara unapoimarika katika injili, utapenda kusoma Biblia yote.*
*Tunafuata mpangilio mwepesi unaokusaidia kusoma Biblia yote kwa kila Mwaka.*

***BIBLIA haijapoteza nguvu zake, siri yake;***
***Biblia ni ya kipekee katika kufanya MUNGU ajulikane kwetu.***

**SOMA LA KUMI NA MOJA**

# KUZALIWA MARA YA PILI

### Hadithi ya Nikodemo, Yohana 3:1-9

Palikuwa na mtu wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi. Huyu alimjia Yesu usiku akamwambia, "*Rabi, twajua ya kuwa u Mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*"

*Yesu akajibu akamwambia, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu."*

Nikodemo akamwambia, "*Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya lili akazaliwa?"*

Yesu akajibu, *"Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa na Roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, Hamna budi kazaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho."*

Nikodemo akajibu akamwambia, "***Yawezaje kuwa mambo haya"?***

### KWA NINI NIZALIWE MARA YAPILI?

Yesu anasema usipozaliwa mara ya pili:

- "***Huwezi <u>kuuona</u> ufalme wa Mungu" aya 3***
- ***"Huwezi <u>kuuingia</u> ufame wa Mungu" aya 5***

### Inamaanishaje kuzaliwa mara ya pili?

#### 1) Kuzaliwa kutoka juu

Maneno haya "kuzaliwa mara ya pili inamaanisha **"kuzaliwa kutoka <u>juu</u>".** Yesu anaweka tofauti wazi kati ya

- Kuzaliwa kwa kawaida – "***kilichozaliwa kwa mwili ni mwili" Yohana 3:6***
- Kuzaliwa kiroho **– *"Kilichozaliwa kwa Roho ni roho" Yohana 3:6***

#### 2) Tunazaliwa mara ya pili kwa kumpokea Yesu

Mtume Yahana anatuambia **"*Bali wote waliompokea aliwapa uweza wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake" Yohana 1:12.***

Masharti ya haki hii kufanyika watoto wa Mungu ni kumpokea Yesu kwa Roho wake katika maisha yetu. Katika msingi wa kuamini, kisha tunaweza kumpokea Yesu na hivyo kuzaliwa mara ya pili.

#### 3) Tunazaliwa kwa Mungu

**"*waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya* mtu, bali *kwa Mungu"* Yohana 1:13.** Hivyo ni, **tumezaliwa kutoka juu au tumezaliwa mara ya pili.**

### NI NINI KINATENDEKA WAKATI NIMEZALIWA MARA YA PILI?

Wakati nimezaliwa “mara ya pili” hivyo ni “kuzakiwa kutoka juu”, mimi:

- Siko katika giza tena: ***“Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake”*** **Wakolosai 1:13.**

- Sio mimi niishiye, ninafanyika kiumbe kipya; Kristo yuhai ndani Yangu (**Wagalatia 2:20).**

- Sitendi dhambi kwa sababu: ***“Nimezaliwa kutokana na Mungu”*** **1Yohana 3: 9,** na uzao wake wakaa ndani yangu **(1Yohana 3:9).** Ninajilinda kutokana na dhambi na yule mwovu hawezi kunigusa. “***Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi”*** **1 Yohana 5:18.**

- Ninawapenda wengine kwa sababu ninamjua Mungu. “***kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu”*** **1Yohane 4:7.**

- Ninaishi katika ushindi. ***“Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu” 1 Yohana 5:4***

- Mimi ni kiumbe cha kiroho. Yesu alisema ***“Kilichozaliwa kwa Roho ni roho” Yohana 3:6.***

- Sasa ninaishi katika himaya ya roho (**Waefeso 1).** Nina:
  - ✓ Kila Baraka ya rohoni kutoka kwa Mungu **aya 3**
  - ✓ Nimechaghuliwa ndani ya Kristo **aya 4**
  - ✓ Nimefanyika mwana **aya 5**
  - ✓ Nimepoke kila neema **aya 6**
  - ✓ Ukombozi kupitia damu yake, msamaha wa dhambi **aya 7**
  - ✓ Nimepokea hekima na ufahamu **aya 8**
  - ✓ Nimepokea maarifa ya ufunuo wa siri **aya 9**
  - ✓ Nimepokea urithi wa kiungu **aya 11**
  - ✓ Nimetiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye mtakatifu **aya 13**
  - ✓ Hekima ya kiungu na ufunuo katika kumjua Mungu **aya 17**
  - ✓ Nimepata kujua tumaini la mwito Wake **aya 18**
  - ✓ Nimeketishwa pamoja na kristo katika ulimwengu wa Roho **Waefeso 2:6**
  - ✓ Tumepata njia ya kumkalibia Baba katika kupitia Yesu Kristo aliye Mwana **Waefeso 2:18**

- Mimi ni huru kwa sababu nimezaliwa kulingana na Roho. “***Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana” Wagalatia 4:31.***

- Nimefanyika mwana wa Mungu. “***Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu”*** **yohana 1:12.**

Tayari tumeona kwamba kuzaliwa mara ya pili inamaanisha kwamba tumezaliwa kutoka juu. Nimezaliwa mara ya pili kwa sababu Mungu anatamani haya. “***Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama libuko la viumbe vyake”*** **Yakobo 1:18.**

"***Mungu hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli"*** **1Timotheo 2:4.** Tumezaliwa kwa mapenzi ya Baba **(Yohana 1:13)**

### NIFANYE NINI ILI NIZALIWE MARA YA PILI?

- **Amini:** Ninaamini katika jina la Yesu Kristo **(Yohana 1:12)**
- **Pokea:** Ninapokea Yesu ndani ya maisha yangu **(Yohana 1:12)**

Hakuna kitu ambacho kinaweza kuuharibu uhusiano wangu wa 'kuzaliwa mara ya pili' kwa maana msingi wake ni katika neno (Mbegu isio haribika) ya Mungu ambayo ni ya kutegemewa kikamilifu. Kwa imani ninapokea ahadi ya Neno la Mungu (Mbegu) na kumpokea Yesu (Mbegu) katika maisha yangu. "***Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele"*** **1Petro 1:23.**

Mungu alikuwa ameahidi mbegu hii na ushidi atakaoupata, katika bustabi ya Edeni. "***Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino"*** **Mwanzo 3:15.** Huu ni unabii wazi kuhusu kuja kwa Masihi Yesu na kile atakachomtendea adui.

**Kuzaliwa mara ya pili inamaanisha kwamba nimeipokea mbegu hii ya ushindi (Yesu) katika maisha yangu na kuishi maisha yangu katika ushindi ambao ameupokea juu ya dhambi na mauti.**

***Aya ya kukariri: Yesu akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu. Yohana 3:5***

**Maswali:**
Nawezaje kuzaliwa mara ya pili? Kulingana na Yohane 1:12 kuna hatua mbili muhimu:

1. ……………………………………………………………………………………

2. ……………………………………………………………………………………

Ni kuzaliwa kwa aina gani – kuzaliwa mara ya pili?...............................................................

Taja Baraka tano zinazotufikia tunapozaliwa mara ya pili.

i. ……………………………………………………………………………………
ii. ……………………………………………………………………………………
iii. ……………………………………………………………………………………
iv. ……………………………………………………………………………………
v. ……………………………………………………………………………………

### SOMO LA KUMI NA MBILI

# TUTAFANYA NINI TUPATE KUOKOKA?

### Petro akihubiri siku ya pentekosti

Katika **Matendo 2** katika siku ya pentekosti, Petro aliwahubiria wale wote waliokusanyika wakati walisikia na kuona Roho Mtakatifu akiwashukia wanafunzi. {Tafadhari **soma Matendo 2**}

Alipohubiri, wote waliokusanyika walipokea ufunuo na ufahamu kumhusu Yesu Kristo:

- Kifo chake, "***Ninyi mkamsulibisha mkamwua"*** **Matendo 2:23.**
- Kufufuka kwake ***"Ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao"*** **Matendo 2:24.**
- Kuinuliwa kwake [kuenenda mbinguni awe mfalme]. "***BWANA alimwambia Bwana wangu, keti upande wa mkono wangu wa kuume. Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako"*** **Matendo 2: 34-35.** Petro alinukuu aya hii kutoka **Zaburi 110** katika agano la kale. Petro anasema Yesu alipokwenda mbinguni, aliketi kwenye enzi ya Mungu.
- Na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu***. "Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia"*** **Matendo 2: 33.** Wakati Yesu alienda mbinguni, alimtuma Roho Mtakatifu.
- Yesu ni Bwana na Kristo. Petro alitangaza kwa Wayahudi- - walikuwako maelfu mengi wakimsikiza akihubiri katika Yerusalemu. "***Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo"*** **Matendo 2:36.** Wakati waliyasikia hayo walichomwa mioyo yao, kwa maana walitambua ya kwamba walikuwa wamemwua yule wa pekee waliomngojea na kumtarajia.

### Tufanye nini tuokolewe? – Matendo 2:38

Petro akawaambia

- Tubuni – hii inamaanisha kubadirisha mawazo kumhusu Mungu
- Mkabatizwe kila mmoja – hii ni kubatizwa kwa maji kwa kuzamishwa
- Kwa jina lake Yesu Kristo – tunatakiwa kubatizwa kwa jina lililofunuliwa la Mungu
- Kwa ondoleo la dhambi zenu – ubatizo wa kweli huziondoa dhambi zetu
- Mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu – RohoMtakatifu anapewa kila muamini

Watu elfu tatu walijiunga na waumini siku hiyo wakabatizwa, na kanisa likapatikana watu waliposikia na kuelewa elimu ya msingi ya injili **(Matendo 2:42)**

**Waebrania 6: 1-2** inasema kwamba elimu ya misingi ya imani ni**:**

1. Msingi wa **kuzitubia** kazi zisizo na uhai,
2. Na imani kwa Mungu,
3. Mafundisho ya **mabatizo,**
4. **Kuwekea mkikono,**
5. **Kufufuliwa** wafu,
6. Na **hukumu ya milele**.

Katika **Waebrania 6:1** tunahimizwa "***tuenende katika ukomavu",*** ambao ni ukomavu katika Kristo. ***"Na haya tutafanya Mungu akitujalia" (Aya 3).*** Lengo la Mungu ni kwamba kanisa likue hata kuufikia utimilifu katika kila njia. Mungu ataturuhusu tuenende katika utimilifu wakati misingi imewekwa vizuri. Mungu ndiye mjenzi mkuu, na ndiye anayepatiana kibali cha kuenenda katika utimilifu. Yesu analijenga kanisa lake, "***Nitalijenga kanisa langu" Mathayo 16:18.***

### Imani ya Biblia ni kuyatenda ambayo Yesu anasema

- Tunapaswa kuwa na ujuzi wa uhakika wa toba na uhakika wa imani katika maisha Yetu.
- Tunatakiwa kubatizwa ndani ya jina la Yesu na kupokea Roho Mtakatifu katika maisha yetu;
- Tunapaswa kutembea katika maarifa ya kufufuliwa wafu na uhakika wa hukumu ya milele.

Misingi nne ya kwanza inatakiwa ijulikane wakati tunakuja katika imani ndani ya Yesu Kristo. Misingi hii inaweza kutamatishwa kwa njia ifuatayo:

***Tubu na uamini, ubatizwe na upokee Roho Mtakatifu!***

### Ufahamu zaidi wa misingi:

1. Msingi wa kina sana ni **neno la Mungu;** neno linachimba ndani ya mioyo yetu, likituamuru tuwe na mawazo yaliyobadirika na kumgeukia Mungu – hii ndiyo **toba.** Neno la Mungu ni kama kioo: inatuwezesha kumwona Mungu ni nani na sisi ni nani (**Yakobo1: 23-25)**
2. Mungu hupatiana njia. **Yesu ndiye njia (Yohana 14:6)**. Imani ni kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Msingi wa **imani** hujengwa juu ya msingi wa toba.
3. Tunatamani **ubatizo,** hii ni, **kuzamishwa katika maji** kuziosha dhambi zetu kuvunja nguvu za dhambi katika maisha yetu, kutuweka katika maisha ya kufufuka kwa Yesu Kristo. Haya ni maisha ya ushindi, bila kutawaliwa na dhambi tena.
4. **Roho Mtakatifu anapokelewa** kupitia **kuwekewa mikono.** Kupitia Roho Wake, Mungu hutupa nguvu zake kumshuhudia Yesu Kristo na kuyaishi maisha ya ushindi.
5. Msingi mwingine ni kuwa na ujuzi wa **maisha ya kufufuka** – tunabatizwa katika kufufuka kwa Yesu **(Warumi 6:5) –** na kufahamu kufufuliwa wafu**.** Siku moja kila mtu atafufuliwa **(Yohana 5: 28-29).**
6. **Hukumu ya milele** ndio msingi wa mwisho ambao tunahitajika kufahamu kabla ya kuenenda katika utimilifu. Hukumu ya milele **inazungumzia hali ya umilele**: kuishi na Mungu milele katika ufalme wake au kuishi milele katika kutenganishwa na Mungu.

Kanisa ambalo lina msingi uliowekwa kulingana na neno la Mungu na utiifu wa neno la Mungu litakuwa na mazao katika huduma.

### YESU ANAFUNDISHA JUU YA KUJENGA KWENYE MWAMBA

Biblia inazungumza habari ya maisha yetu kama majengo; "***sisi ni nyumba Yake"*** **Waebrania 3:6** na "***sisi ni jengo lake*"** **1 Wakorintho 3:9.** Tunapaswa kujenga kulingana na mafundisho ya Yesu kuwa na msingi bora, na kujenga nyumba [maisha] ambayo yatasimama.

***Luka 6:46 "Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamuyatendi nisemayo?"***
Hatuwezi kusema 'Laa" kwa Yesu kama kweli yeye ni Bwana wa maisha yetu.

***:47 "Kila mtu ajaye kwangu, na kuyasikia maneno Yangu na kuyatenda, nitawaonyesha mfano wake".*** Tunapaswa tuje; tusikie na kutii.

**:48 "*Mfano wake ni mtu ajengaye nyumba, na kuchimba chini sana, na kuweka msingi juu ya mwamba".*** Tunatakiwa kuondoa kila kizuizi kati yetu sisi na Mwamba, ambaye ni Kristo. Hii inahusisha kutubu – kuwa na imani kwa Yesu, Mwamba wa wokovu wetu.
***"Na kulipokuja gharika, mto uliishukia nyumba ile kwa nguvu, usiweze kuitikisa; kwa kuwa imejengwa vizuri."*** Maisha yaliyo na msingi katika imani ndani ya Yesu Kristo hayawezi kuharibiwa na majaribio ya maisha.

**:49 "*Lakini yule aliyesikia ila hakutenda, mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu, ikaanguka mara; na maangamizi yake nyumba ile yakawa makubwa."***

Yesu anataka tuyajenge maisha yetu na kanisa katika msingi imara

Orodhesha misingi sita iliyoelezwa katika **Waebrania 6:1-2**

1. ……………………………………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………………………………
3. ……………………………………………………………………………………………
4. ……………………………………………………………………………………………
5. ……………………………………………………………………………………………
6. ……………………………………………………………………………………………

***Aya ya kukariri: Matendo 2:38***

**"*Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"***

*Unaweza kukumbuka hadithi ambayo Yesu alisimulia juu ya kujenga juu ya mwamba? Ni yapi mambo makubwa?*

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………………**

**SOMO LA KUMI NA TATU**

# KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI

### Kutubu ni nini?

- Kutubu ni kugeuka na kuachana na dhambi, uasi na kutotii na kugeuka kumtazama Mungu.
- Kutubu inamaanisha: kubadirisha mawazo, ikihusisha hisia ile hali ya kuhisi majuto kwa asbabu ya tabia za kale ambazo hazikuwa nzuri (dhambi)
- Dhambi hakika yamaanisha "kupoteza alama"
- Ni nani tumemtendea dhambi? ***"Nimekutenda dhambi wewe peke yako"*** **Zaburi 51: 4**

### 1. Kila mtu anatakiwa kutubu?

***"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, ka kupungukiwa na utukufu wa Mungu"*** **Warumi 3:23.** Mtume Paulo anasema; ***"Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu"*** **Matendo 17:30**

### 2. Kutubu ni mapenzi ya Mungu kwa kila mtu

Tunajua kwamba ni mapenzi ya Mungu kila mtu kutubu. "***Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."*** **2Petro 3:9**

### 3. Ni lazima toba ihubiriwe

Yohana mbatizaji alitengeneza njia kwa kuja kwake Masihi. "***Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."*** **Mathayo 3:2**

**Yesu alianza huduma yake akiamuru toba. "*Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"* Mathayo 4: 17.**

Wanafuni walienda wakihubiri toba. "***Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu"*** **Mariko 6:12.**

Yesu aliwatuma wanafunzi wake wahubiri ujumbe wa toba kwa mataifa yote.
***"Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba"*** **Luka 24:46-47.**

Siku ya Pentekosti, Petro alihubiri toba kama masharti ya kubatizwa na kupokea Roho Mtakatifu. "***Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** **Matendo2:38.**

### 4. Wakristo wanapaswa kutubu?

Soma **1Yohana 1: 8-10 "*Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu"*** **aya 8*.*** ***"Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu"*** **aya 10.**

**Aya 9** inatwambia jinsi ya kufanya tukitenda dhambi, ***"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni Mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."***

### 5. Kila kutotii kwa maagizo ya Mungu ni dhambi

Dhambi inatutenga na Mungu. "***Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote"*** **Yakobo 2:10.** Yesu anatufunza kuhusu ambalo latoka "***ndani ya moyo wa mwanadamu"*** na mambo hayo maovu "***yamtia mtu unajisi"***

- ❖ **Mariko 7: 21-23** ni mambo yapi yanamtia mtu unajisi?

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

- ❖ **Warumi 1: 29-32** ni yapi yanayotendeka wakati mtu anaazimu kupuuza sheria za Mungu?

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

- ❖ **Ufunuo 22:14-15** ni nini kitatuzuia kuingia katika ufalme wa Mungu?

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………

## Dhambi zinatudhuru kwa njia ipi?

- Huzuni ya dunia – tunajiletea hukumu wenyewe na wengine mara kwa mara wanaadhiriwa, pia
- Huzuni ya Mungu – tunazikubari dhambi zetu naye Mungu anatusamehe. **1 Yohana 1:9.**

**"*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia huleta mauti"* 2 Wakorintho 7:10.**

## Toba inahusisha kuyabadilisha mawazo

Toba inahusisha kubadilisha mawazo ambapo tunageuka kabisa kutoka kwa yale tumekuwa tukitenda na kugeukia yale ambayo Mungu angetaka tutende.

### i. Zakayo ni mfano mzuri

Wakati alipompokea Yesu, alibadilisha njia yake ya maisha, na akarudisha vitu vyote alivyokuwa ameiba na hata Zaidi **(Luka 19:8)**

### ii. Mwana mpotevu – Luka 15:11-24

Hadithi ya mwana mpotevu ni mfano wa mtu ambaye alikuwa amepoteza mali yake na alikuwa anaishi maisha ya kikahaba. Alitubu na akabadilika kabisa [akageuka].

Mwana:

- "***Alizingatia moyoni mwake"* (aya 17),** jawabu kutokana na huzuni ya dunia
- Akafanya maamuzi bora **(aya 18-19),** toba katika mawazo yake
- Alitenda kulingana na maazimio **(aya 20),** alibadilika – akageuka

### Ni yapi matokeo ya toba ya kweli?

- ➢ Upendo mpya kwa Mungu na mapenzi ya kumpendeza
- ➢ Tunaitoa miili yetu kila siku kuyafanya mapenzi yake, **Warumi 12:1-2**
- ➢ Uhuru kutokana na hukumu na haibu, **Warumi 8:1**
- ➢ Yesu ametuahidi amani, **Yohana 14:27**

### Toba huelekea ubatizo

- ❖ Yesu alisema: Tubuni na muamini katika injili, **Mariko 1:15**
- ❖ Petro alisema: Tubuni na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, **Matendo2:38**
- ❖ Paulo alisema: Tubuni, mgeukie Mungu na mzifanye kazi zinazolingana na toba, **Matendo 26:20**
- ❖ Toba ni kipawa cha Mungu ambacho tunapokea kwa imani.

Aya ya kukariri**: "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."* 2 Petro 3:9**

**Ni jambo gani kuu umejifunza kuhusu toba?**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

**SOMO LA KUMI NA NNE**

# IMANI KWA MUNGU

### IMANI NI NINI?

- Imani ni ushawishi unaotokana na kusikia.
- Inaambatana na **kutumaini** na **kuamini**

Katika Biblia neno "imani" linatumika likiongea habari za Mungu ama Yesu Kristo ama mambo ya kiroho.

Tunapoona na kutambua dhambi zetu tunapata ujuzi wa hofu ya kiungu na tunatubu. Lakini tusipoamini tumesamehewa, toba yetu ni bure.

Tusipoamini kwamba Yesu ameziondoa dhambi zetu, hukumu yetu na haibu ama jitihada kuwa huru kutoka kwa dhambi itakuwa tu bure.

***Kutubu ni kugeuka kuachana na dhambi na imani ni kugeukia Mungu.***

Kwa imani:

- Tunampokea Yesu Kristo haswa kama alivyo katika injili
- Tunamtumaini na kujipatiana kwake
- Tunakubali ahadi za Mungu kwetu kupitia Yesu

### Biblia inaelezaje imani?

**"Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, *ni bayana ya mambo yesioonekana*" Waebrania 11:1.** Yatarajiwayo na yasioonekana yanakuwa hakika kwa maana tunamtumaini Mungu.

### Imani kwa Mungu

- Tunaamini kwamba Mungu anaweka ahadi zake. "***Lakini Bwana ni mwaminifu*" 2Wathesalonike 3:3.**
- Tunaamini kwamba Mungu anaweza kutenda yale alioahidi atatenda "***Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi*" Warumi 4:21.**

### Mtu hawezi kuokolewa pasipo imani.

**i)** ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa"* Mariko 16:16**

**ii)** **Wokovu ni kipawa kinachopokelewa kwa imani. *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu"* Waefeso 2:8**

### Mtu hawezi kumpendeza Mungu pasipo imani

***"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao"* Waebrania 11:6**

## Tunapokeaje imani?

***"Basi Imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"* Warumi 10:17.** Neno la Mungu ni yale Mungu anasema, hivyo ni, Biblia inatakiwa kusomwa na kuaminiwa kama ilivyoandikwa. Mungu anaendelea kusema nasi kupitia Mwana, ambaye ni Neno liishilo (**Wabrania 1:2, Yohana 1:1**), na Yesu alisema: "***Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"* Mathayo 4:4**

- Tunamsikia Mungu akisema nasi binafsi tunaposoma Biblia.
- Tunapokea imani ya kufanya yale tumesikia.
- Yesu anakuwa hakika kwetu. Yeye ni "**Neno alifanyika mwili'' Yohana 1:14.**

Kwa wepesi ni kwamba kuwa na habari hakuhakikishi wokovu! "***Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka"* Yakobo 2:19**

## Imani ni:

- ➔ Maamuzi ya kupokea neno tulilolisikia
- ➔ Kupokea kwa kuamini yule ambaye amelinena katika mioyo yetu
- ➔ Kumgeukia Mungu na kubadilika tunapomtumaini atimize neno lake
- ➔ Kudhawabiwa kwa kutambua ya kuwa Mungu ni mwaminifu na anaweka ahadi zake.

## IBRAHIMU – BABA WA WOTE WANAOAMINI

Katika **Warumi 4,** Paulo anaonyesha kutembea kwa imani kwa mfano wa Ibrahimu:

- ❖ Mungu alimhesabu Ibrahimu kama mtu mwenye haki kwa sababu alimwamini Mungu **(aya 3).**
- ❖ Ibrahimu alisikia na kupokea neno kutoka kwa Mungu **(aya 13, 21)**
- ❖ Ibrahim aligeuka kwa imani kutoka kwa hali yake isiokuwa na matumaini **(aya 18-20)**
- ❖ Ibrahimu aliamini na akashikilia ahadi ambayo Mungu alimpa katika **Mwazo 15:3-6 (18)**
- ❖ **"*Hakusita kwa kutokuamini"* (aya 20)**
- ❖ **"Alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu" (aya 20)**

**Wabrania 11:8-9**

- ❖ **"*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako".***
- ❖ **"*Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi".***

## Watu wengine wa imani

**Waebrania 11** inatuambia kuhusu watu wengine wa imani. Hawa wote walikufa katika imani, bila kuipokea ahadi, lakini wakiziona kwa mbali, walihakikishiwa, wakazikumbatia na wakakili kuwa walikua wageni na wapitaji hapa duniani **(aya 13).**

**"*Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi; kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi."* aya 39-40.**

## YESU NDIYE UTIMILIFU WA "kitu kilicho bora"

Wakati Yesu alianza huduma yake na muujiza katika sherehe za harusi katika Kana, tunasoma kwamba *"**Wanafunzi wake wakamwamini***" **Yohana 2:11.**

Wanafunzi walimuuliza Yesu watafanya nini kuzifanya kazi za Mungu. Yesu akawajibu: ***"Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini Yeye aliyetumwa na Yeye."*** **Yohana 6.:29**

### Aliyyanena Yesu kuhusu kuamini na kutumaini (imani)

- **"*Yesu akamwambia, Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki"* Yohana 20:29**
- ***"Jipe moyo mkuu, binti yangu; imani yako imekuponya"* Mathayo 9:22**
- Kwa wale vipofu: ***"Kwa kadiri ya imani yenu mpate"* Mathayo 9:29**
- Yesu alisema kwa yule akida: "***Nenda zako; na iwe kwako kama ulivyoamini"* Mathayo 8:13**

### Anachokisema paulo kuhusu imani

- ***"Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu"* I Wakorintho 2:5**
- ***"Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu"* 1 Wakorintho 15:17**
- ***"Kwa imani yenu mnasimama"* 2 Wakorintho 1:24**

### Aliyosema Yakobo kuhusu imani

- ***"Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote"* Yakobo 1:6**

### Kwa imani ndani ya Yesu Kristo tunapokea:

- Ahadi ya Roho Mtakatifu **Wagalati 3:14**
- Uwana **Wagalatia 3:26**
- Wokovu **Waefeso 2:8**
- Kumfikia Baba **Waefeso 3:11-12**

### Kwa imani ndani ya Yesu Kristo

- Tumefanyika haki **Warumi 5:1**
- Tuna amani na Mungu **Warumi 5:1**
- Tunaifikia neema ya Mungu **Warumi 5:2**
- Tunafurahia katika tumaini la utukufu wa Mungu **Warumi 5:2**

Mara tunapoweka msingi wa kutubu katika maisha yetu, tunafanywa haki na Mungu kwa kuamini kwetu. Mungu anahitaji kwamba sasa tuishi kama Ibrahimu alivyoishi: "***Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi"* Warumi 4:21.**

***Ukweli wa imani yetu unaweza kujaribiwa,***
***lakini tukibaki waaminifu, matokeo ni yapi****?*

**Aya ya kukariri: "*Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani, wokovu wa <u>roho zenu.</u>" 1 Petro 1:8-9***

***Andida maelezo ya imani kutoka kwa yale umejifundisha:***

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

SOMO LA KUMI NA TANO

# MAFUNDISHO YA MABATIZO

Maandiko yanaongea habari ya baadhi ya mabatizo:

- Ubatizo wa maji – ubatizo wa Yohana, Yesu, na ubatizo wa waumini
- Kubatizwa ndani ama kwa Roho Mtakatifu
- Ubatizo wa moto
- Utatizo ndani ya mwili wa Kristo
- Ubatizo wa mateso.

Mafundisho ya mabatizo katika **Waebrania 6:2** inazungumzia ubatizo wa maji, hivyo ni, kuoshwa kwa maji.

**Kimsingi ubatizo unamaanisha kuzamishwa; kubatiza ni kuzamisha**

## UBATIZO WA YOHANA

Ubatizo wa Yohana ulikuwa wa kuwaita watu wa siku zake kubadilisha njia zao za maisha katika kujiandaa kwa Masihi. Ulikuwa ni **ubatizo wa toba;** ulikuwa ni ubatizo wa ishara ukiwaonyesha watu kutamani kumpokea Masihi.

Kitendo cha ubatizo hakikuwa kipya wakati Yohana alikuja, lakini kilikuwa kipya kwa Wayahudi kubatizwa kama ishara ya toba. Walidhania kuwa watu wa mataifa ndio walihitaji kutubu na kumwamini Mungu wa kweli.

Yohana alikuja akisema: "***Tubuni; kwa maana ufalme wa mbiguni umekaribia"*** **Mathayo 3:2.**

Mara tu Yohana alipombatiza Yesu, huduma ya Yohana ilianza kupungua na huduma ya Yesu ikaanza kuongezeka. (**Yohana 4:1-2).** Yohana alimtabulisha Masihi kwa Waisraeli.

## UBATIZO WA YESU

Yesu hakuhitaji kutubu. Alikuwa mtu asiye na dhambi.

Alibatizwa kwa nini? Yesu alisema. "***Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kutimiza haki yote."*** **Mathayo 3:15**

Yesu alibatizwa kulingana na mapenzi ya Mungu kutimiza sheria ya Mungu: hii ilikuwa ni kutimiza sheria ambayo ilihitaji kuhani kupia sherehe ya kuoshwa katika umri wa miaka therathini.

Ni nini kilifanyika Yesu alipotoka kwa maji? Mara tu kilichofuata ubatizo Yesu alipakwa kwa njia kuu na Roho Mtakatifu.

**Mathayo 3: 16-17**

- ***"Mara akapanda kutoka majini;***
- ***Mbingu zilimfungukia***
- ***Na akamwona Roho wa Mungu akishuka***
- ***Kama hua akija juu yake."***

***"Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanagu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye."*** Mungu alitambua Yesu kuwa Mwanawe. Sasa Yesu alifunuliwa kama

Mungu katika mwili. Kuanzia wakati wa kubatizwa kwake, Yesu alitembea kama Mungu duniani.

Tunapaswa kuamini maagizo ya Yesu kubatizwa kwa imani, na kama matokeo ya ubatizo wetu tutatembea na Kristo ndani yetu, hapa duniani.

### MAAGIZO YA UBATIZO

Yesu mwenyewe alipatiana maagizo ya ubatizo baada yake kufufuka katika wafu. Aliwaelekeza wanafunzi wake: "***Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu."*** **Mathayo 28:19**

Yesu anaweka wazi kuwa ubatizo huu unafwata:

- **Toba** – **"*Mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi"* Luka 24:47**
- **Kuamini, hiyo ni imani** – **"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka." Mariko 16:15-16**

Toba ya kweli (mabadiliko) huja kabla ya imani ya kuokoa. Mtu anayebatizwa lazima awe ni mtu aliyetubu (kubadilika) na kuanini kwanza. Mtoto mchanga hawezi kutubu wala kuamini.

## ZOEZI LA UBATIZO KATIKA KITABU CHA MATENDO

### (1) Siku ya Pentekosti – matendo 2: 14-41

- Petro alihubiri **(aya 14-36)**
- Watu walishawishika '**tutendeje, ndugu zetu?" (aya 37)**
- Petro akajibu '***Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo" (aya 38)***
- Watu walitii na nafsi elfu tatu 3000 wakaongezeka siku hiyo **(aya 41)**

**Elewa:**

- Ubatizo ulikuwa siku hiyo
- Ubatizo ndiyo uliokuwa kiingilio cha kanisa- mwili wa Kristo
- Ubatizo ulikuwa katika jina la Yesu Kristo

### (2) Katika Samaria – Matendo 8:5-17

- Filipo alihubiri
- Watu walioamini walibatizwa katika jina la Bwana Yesu (**aya 12,16)**
- Mitume walifika na kuwawekea mikono ili wapokee Roho Mtakatifu **(aya 17)**

### (3) Mtu kutoka kushi -Matendo 8:35-38

- Mtu wa kushi alikuwa akisoma neno la Mungu **(aya 30-33)**
- Filipo alimhubiria habari za Yesu (**aya 35)**
- Alimwamini Yesu na akataka kubatizwa **(aya36)**
- Alibatizwa katika msingi wa kukiri kwake imani katika Kristo Mwana wa Mungu **(aya 37-38)**

### (4) Sauli katika Dameski- Matendo 9:5-18

- Sauli alipokea ufunuo wa Yesu Kristo **(aya 5-6)**
- Anania alimbatiza Sauli **(aya 18)**

### (5) Mataifa wanabatizwa – Matendo 10:34-48

- Petro alihubiri **(aya 34-43)**
- Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia neno **(aya 44)**
- Wale waliokusanyika walinena kwa ndimi wakimtukuza Mungu **(aya 46)**
- Petro aliwabatiza katika jina la Bwana **(aya 47-48)**

### (6) Kubatizwa tena katika Efeso – (Matendo 19: 1-7)

- Paulo alikutana na baadhi ya wanafunzi katika Efeso **(aya.1)**
- Wanafunzi hawa tayari walikuwa wamebatizwa kwa ubatizo wa Yohana, hivyo ni ubatizo wa toba (**aya 3)**
- Paulo alihubiri kuhusu kumwamini Yesu Kristo **(aya.4)**
- Wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu Kristo **(aya.5),** katika maji
- Kisha wakapokea kipawa cha Roho Mtakatifu **(aya 6)** kupitia kuwekewa mikono.

## UBATIZO WA WAKRISTO ama WA WAUMINI

Agizo la kubatiza lilipeanwa:

- Na Yesu **(Mariko 16:16, Mathayo 28:19)**
- Baada ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwake **(Mariko 16:14, Mathayo 28:18)**
- Baada ya kupaa kwake na kutukuzwa, mitume na wanafunzi walifanya ubatizo **(Matendo 2:38, 41)**
- Katika jina la Yesu Kristo (**Matendo 2:38);** walilifahamu jina lililofunuliwa la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

Ubatizo wa waumini huja baada ya toba na msingi wake uko katika toba.
Huja baada ya mtu kuzaliwa mara ya pili kwa imani katika Kristo.

**Toba + imani → ubatizo**

### Ni damu ya Yesu Kristo ambayo inafanya ubatizo wa mkristo uwe wa kweli

Mabatizo yote ya kale na sherehe za kuoshwa zilikuwa mfano ikihusisha ubatizo wa Yohana. Haingeweza kuosha dhambi za mtu. Pasina kumwagika kwa damu hakuna msamaha wa dhambi (**Waebrani 9:22).**
Ubatizo wa wakristo unaonyesha kuoshwa kwa dhambi kwa maana yule anayebatizwa tayari amekwisha kusamehewa kupitia damu ya Yesu Kristo.

### Kutambulishwa na Yesu kupitia ubatizo

Paulo anaongea na waumini na kuwakumbusha kilichotendeka katika ubatizo wao.
**Warumi 6:1-12**

- **:3** Tunabatizwa katika mauti ya Kristo Yesu
- **:4** Tunazikwa pamoja naye
- **:4** Tunainuliwa katika upya wa uzima pamoja naye
- **:5** Tunaunganishwa naye katika mauti yake na katika kufufuka kwake
- **:6** Utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye – dhambi zimeondolewa
- **:7** Tuko huru kutokana na dhambi
- **:8** Tulikufa pamoja na Kristo: tunaishi pamoja na Kristo
- **:9** Yesu Kristo ameshinda kifo
- **:10** Alikufa kwa dhambi mara moja kwa wote: anaishi kwa Mungu

- **:11** Tunajihesabu kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mugu katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Yesu alisema, ***"Aaminiye na kubatizwa* ataokoka"** **Mariko 16:16**

*Aya ya kukariri: "**Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" Mathayo 28: 19.***

***Ni nini kinakuja kabala ya ubatizo***

*Luka 24:47…………………………………*

*Mariko 16:16……………………………………………………………….*

*Ni kwajia zipi tatu ambazo tunajitambulisha na Yesu katika ubatizo? Tazama,* **Warumi 6:3-5**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….…..

**SOMO LA KUMI NA SITA**

# KUWEKEA MIKONO

Mwamini anatubu na kumgeukia Mungu kupitia imani katika Kristo Yesu na anabatizwa. Hatua inayofuata kuelekea ukomavu **ni kujazwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu.** Fundisho la kuwekea mikono kimsingi linazungumzia habari za kujazwa na Roho Mtakatifu kwa waamini wapya. Kipawa cha Roho Mtakatifu kinapokelewa kwa kuwekea mikono, hata kama wakati mwigine Mungu kwa njia zake za kiungu anamjaza mtu na Roho Mtakatifu pasina kuwekea mikono.

### Wayahudi katika siku ya pentekosti

Kule kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya pentekosti kama ilivyonakiliwa katika **Matendo 2** ilikuja kwa njia ya nguvu kutoka mbinguni na wale waumini 120 katika chumba cha juu wote walipokea Roho Mtakatifu kwa pamoja.

### Kulikuwa na ishara kadhaa:

- **i.** Uvumi wa upepo,
- **ii.** Kama ndimi za moto;
- **iii.** Wakasema kwa lugha nyingine.

Lakini ishara iliyoonekana ya kupokea Roho Mtakatifu inayodumu hata leo, ilikuwa kwamba **waamini walisema kwa lugha nyingine kama Roho alivyo wajalia kutamka** (**Matendo 2:1-4).** Huku kumwagwa kulikuwa juu ya wanfunzi Wayahudi wa Yesu.

### Juuya Mataifa

Kulikuwa na kumwagwa kwingine kwa Roho Mtakatifu kulikonakiliwa katika **Matendo 10.** Kikundi cha watu wa mataifa walikuwa wamekusanyika katika nyumba ya Kornelio kumsikia mtume Petro akiongea habari za Yesu.

- **i.** Walimwamini Petro akihubiri
- **ii.** Wakati alipokuwa akiongea, walipokea Roho Mtakatifu
- **iii.** Walianza kusema katika lugha nyingine.

  Mataifa walipokea Roho Mtakatifu jinsi Wayahudi walipokea hapo mwanzo.

  Katika ishara hizi mbili za kiungu hakukuwa na kuwekea mikono, lakini ishara zingine zilizonakiliwa za kupokea Roho Mtakatifu katika kitabu cha matendo ni kupitia kuwekea mikono.

Hivyo msingi wa nne ni kupokea Roho Mtakatifu kwa njia ya kuwekea mikono, lakini hata siku ya leo Mungu anachagua wakati mwingine kumwaga Roho wake Mtakatifu kwa Nguvu juu ya watu binafsi au kwa vikundi wanaomtafuta.

### Roho mtakatifu ni "*Ahadi ya Baba*" Luka 24:49

Yesu aliwaambia w anafunzi wangojee mpaka watakapovikwa na nguvu kutoka juu

***"Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu" Luka 24:49.***

Yesu aliwaamuru wanafunzi wasitoke Yerusalemu, "***Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake***

***kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache"*** **Matendo 1:4-5**

Yohana mbatizaji aliongea juu ya ubatizo huu ambao ungekuja na yesu kristo.

"***Yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto"*** **Luka 3:16**

Kipawa cha Roho Mtakatifu sanasana kinaachiliwa kwa mwamini kwa njia ya kuwekea mikono. Mwamini anapokea Roho Mtakatifu, na vipawa vya Roho Mtakatifu vinakuwa wazi kwa mwamini. Hata hivyo, karama tofauti zinaachiliwa kwa kuwekea mikono.

## KUWEKEA MIKONO KATIKA AGANO LA KALE

### Kuachilia Baraka

Yakobo aliwabariki wana wa Yusufu kwa kuwawekea mikono na akanena maneno ya kiunabii kuhusu hatima ya mataifa **(Mwanzo 48:14-16)**

### Kuwaweka watu wakfu kwa sababu ya huduma fulani

Musa alimuuliza Mungu kumweka mtu juu ya watu alipojua wakati wake wa kufa umefika **(Hesabu 27:15-23).** Mungu alitoa maagizo: "***Mtwae Yoshua, mwana wa Nuni, mtu mwenye roho ndni yake, ukamwekee mkono wako"*** **aya18.** ***"Nawe utaweka juu yake sehemu ya heshima yako"*** **aya 20.**

Musa alitii maagizo ya Mungu. "***Musa akafanya kama BWANA alivyomwamuru"*** **aya 22.** Musa aliyafanya haya mbele ya makuhani na watu. "***kisha akaweka mikono yake juu yake; akampa mausia, kama BWANA alivyosema kwa mkono wa Musa"*** **aya 23**

***"Na Yoshua mwana wa Nuni, alikuwa amejaa roho wa hekima; maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake"*** **Kumbukumbu la tolati 34:9.**

## KUWEKEA MIKONO KATIKA AGANO JIPYA

### Yesu

- Yesu aliwafufua wafu. Katika **Mathayo 9:18** jumbe mmoja alitarajia Yesu amrejeshe binti yake kwa uhai. "***Binti yangu sasa hivi amekufa; lakini njoo, uweke mkono wako njuu yake, naye ataishi".***
- Aliwaponya wagonjwa. "***Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake, akaweka mikono juu ya kila mmoja akawaponya"*** **Luka 4:40.** Tazama pia **Luka 13:13.**
- Aliwabariki watoto. "***Ndipo akaletewa watoto wandogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea".*** **Mathayo 19:13**

### Yesu aliwatuma wanafunzi wake kuwawekea watu mikono

Yesu alisema baadhi ya ishara zingewafuata waaminio. "***Na ishara hizi hizi zitafuatana na hao waaminio; … kwa jina langu… wataweka mikono yao juu ya wagonjwa; nao watapata afya"*** **Mariko 16:17-18**

Yesu ameahidi kuwatia nguvu waamini kutimiza ahadi hii.

"***Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi"*** **Matendo 1:8**

### Kuwekea mikono ili kopokea Roho Mtakatifu

- Petro na Yohana walikuja kwa wanafunzi katika Samaria. “***Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakapokea Roho Mtakatifu.”*** **Matendo 8:17.** Yule mchawi**, *Simioni alipoona ya kuwa wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono”*** **Matendo 8:18.**
- Paulo alipokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono na Anania (**Matendo 9:17)**
- Paulo aliwawekea waumini waliobatizwa mara ya pili kule Efeso nao wakapokea Roho Mtakatifu, wakasema kwa lugha na kutabiri **(Matendo 19:4-6)**

### Waamini wanawekwa wakfu na kutakaswa kwa sababu ya huduma

1. **Matendo 6:2-7 –** watu saba walichaguliwa wawasaidie mitume katika huduma; baada ya kuomba, wakawawekea mikono.
2. Wahuduma walitumwa kuhudumu katika kutii Roho Mtakatifu (**Matendo 13:2-3)** walipohudumu mbele ya Bwana na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, “***Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia”*** kisha wakiisha kufunga na kuomba, wakawekea mikona juu yao.
3. Mungu aliweka karama ndani ya Timotheo kwa njia ya kuwekewa mikona na Paulo. “***Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu”*** **2Timotheo1:6.** Anamkumbusha Timotheo asiache kuchochea karama iliyo ndani yake kwa kuwekewa mikono na wazee, “***Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani mwako, uliyopewa kwa unabii na kuwekewa mikono ya wazee”*** **1Timotheo 4:14**

### Waumini waliwaponya wengine kwa Jina la Yesu kwa kuwawekea mikono

- Waumini waliwawekea wagonjwa mikono katika kutii maagizo ya Yesu
- Paulo alipokea kuona kwake alipo wekewa mikono na Anania **(Matendo 9:17-18)**
- paulo alimwekea baba yake publio na akapokea uponyaji **Matendo 28:8-9**

***Mitume, wanafunzi na waumini wanatakiwa wahudumu kwa njia ya kuwekea mikono.***

*Aya ya kukariri*: ***“Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.” Luka 24:49***

**Maswali:**

Waumini wapya wa Samaria walipokea Roho Mtakatifu walipobatizwa?

……………………………………………………………………………………..

Walipokea Roho Mtakatifu kwa njia ipi? ………………………………………………………

…………..........................................................................................................................

.........................................................................................................................

Umepokea Roho Mtakatifu?. ………………………………………………………………..

Ulipokea kipawa cha kunena na lugha nyingine?.....................................................................

**SOMO LA KUMI NA SABA**

# KUFUFULIWA WAFU [Sehemu ya kwanza]

### Kufufuka kwa Yesu Kristo kuna umuhimu mkubwa sana katika imani yetu

- Kufufuliwa wafu kunategemea kufufuliwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo.
- Pasina kufufuka kwake, hakuna ufufuo wa wafu na hivyo hakuna tumaini kwa waumini.

Mtume Paulo anasema: "***Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka. Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu."*** **1Wakorintho 15:16-17**

### Kufufuka ni nini?

Hali ya kuinuliwa; kuinuliwa kutoka kwa wafu; kurejelea uhai.

### Yapo mambo matatu ya muhimu katika mafundisho ya kufufuliwa wafu

- Kufufuka kwa Yesu Kristo
- Kufufuliwa kiroho kwa waumini ndani ya Yesu Kristo
- Kufufuka katika siku ya mwisho ***"watu* wote *walio makaburini"*** **Yohana 5:28-29**

## KUFUFUKA KWA YESU KRISTO

Wakati wamama walikuja kuiona kaburi baada ya Yesu kufa, malaika aliwazungumzia. "***Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa".*** **Mathayo 28:6**

Yesu ndiye wa kwanza kufufuka katika wafu. "***Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala."*** **1 Wakorintho 15:20**

Kifo hakingemzuia Yesu. "***Ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao"*** **Matendo 2:24**

### Kuna uhakika gani ya kwamba Yesu alifufuka katika wafu?

Alizungumza na mitume. "***Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea mda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliouhusu ufalme wa Mungu"*** **Matendo 1:3.**

#### Yesu alionekana na watu wengi

- Kefa: "***Na ya kuwa alimtokea Kefa; tena wale Thenashara".*** **1 Wakorintho 15:5**
- Watu wengine mia tano: "***Baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala"*** **1Wakorintho 15:6**
- Yakobo: "***Baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote"*** **1 Wakorintho 15:7**
- Sauli katika njia ya kwenda Dameski: "***Na mwisho wa watu wote, alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake"*** **1 Wakorintho 15:8.**

### Mwili wake ulikuwa wa nanma gani alipofufuka?

1) **Alikuwa na mwili na mifupa**

Yesu alijionyesha kwa wanafunzi wake. "***Na walipokuwa katika kusema habari hiyo, yeye mwenyewe alisimama katikati yao, akawaambia, Amani iwe kwenu. Wakashituka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, Mbona mnafadhaika? Na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo"*** **Luka 24:36-39.**

2) **Alikula**

Alikula samaki mbele yao (**Luka 24:41-43)**

3) **Aliyabeba majeraha**

Yesu alimwambia Tomaso aiguze mikono yake na bavu. "***Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu; wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye."*** **Yohana 20:27**

**Manabii wa agano la kale waliongea kuhusu kufufuka kwa Bwana**

**Isaya 53:10 –** Aliyejeruhiwa na akafa, ***"Ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake".*** Hii inaongea kumhusu mtu aliyekufa lakini akafufuka, inazungumza kuhusu kufufuka kwa Masihi.

**Zaburi 16:10-11 –** Mtakatifu wa Mungu hataachwa nafsi yake "**Kuzimu" [**kuzimu ni mahali kwa waliokufa]; mwili wake "**hautaona uharibifu**". Andika **aya .10**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**Zaburi 68:18 –** inaogea kuhusu mtu "***aliyepaa juu".*** Hii inaongea kuhusu mtu aliyepaa. Ni maneno ya kiunabii kuhusu Yesu akipaa mbinguni.

## Kufufuka kwa Yesu kunatufundisha nini?

1. Yeye ni Mwana wa Mungu – ***"Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu"*** **Warumi 1:4**. Ufufuo ndiyo dhibitisho kwamba Yesu ni Mungu.

2. Kifo kimeshindwa – "***Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena."*** **Warumi 6:9.** Hii ni habari njema kwa wanadamu: kifo kimeshindwa.

3. Yesu Kristo ndiye mkuu juu ya wote wanaoishi – Tafadhari soma **Mathayo 28:18** na **Waefeso 1:20-23.** Vifungo hivi viwili vinatuonyesha Yesu Kristo ana mamlaka yote mbiguni na duniani, ikihusisha nguvu zote za mapepo

4. Huyu ndiye mtu aliye katika enzi ya mbinguni – "Lakini huyu, ***alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu"*** **Waebrania 10:12. '**Mkono wa kuume' inamaanisha pahali pa nguvu zote.

5. Waamini wanafanywa haki – Yesu "***alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki."*** **Warumi 4:24-25.** kwa kufa Yesu aliziondoa dhambi zetu na kwa kufufuka alitupatia maisha mapya.

6. Kunalo tumaini la kweli kwa mwanadamu kwa sababu Mungu "***Alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu"*** **1 Petro 1:3**

7. Hukumu ya milele imehakikishwa – **Matendo 17:31.** Kwa kuwa Yesu alifufuka katika wafu, ana haki ya kuhukumu "***walimwengu kwa haki".***

8. Tunaweza kujitambulisha na kufufuka kwake – **Warumi 6:5**. Tunabatizwa katika mauti yake na tunainuliwa "***kwa mfano wa kufufuka kwake"***

**Maswali:**

Kufufuka kwa Yesu Kristo kunamaanisha nini haswa? **Mathayo 28:6**

...........................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

Patiana dhibitisho tatu ya kuwa Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.

1. ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………

*Aya ya kukariri*: "***Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea mda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliouhusu ufalme wa Mungu" Matendo 1:3***

**SOMO LA KUMI NA NANE**

# KUFUFULIWA WAFU {Sehemu ya pili}

Jambo kuu la kwanza katika kufufuliwa wafu ni kufufuka kwaYesu Kristo. Kwa maana Yesu Kristo alifufuka katika wafu, amefanya iwezekane kwa watu waliozaliwa mara ya pili. Kutokana na kufufuka kwa Yesu Kristo tunaweza kupokea kufufuliwa kiroho.

## KUFUFULIWA KIROHO KWA WAUMINI

Kufufuliwa kwa waumini huanza kwa kuzaliwa upya. Wakati tunapokea msamaha wa dhambi zetu, tunapata uzima wa Mungu katika Kristo.

- Tumehuishwa – "***Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu."*** **Waefeso 2:1.** Hapo mwanzo tulikuwa tumekufa kiroho kwa sababu ya makosa yetu, lakini kwa imani ndani ya Yesu Kristo alituhuisha.

- Tumeinuliwa juu katika ulimwengu wa roho. "***Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; (yaani, mmeokolewa kwa neema). Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"*** **Waefeso 2:5-6.** Huku ni kufufuliwa kiroho.

- Kupitia ubatizo tunakuja kuishi na Kristo – "***Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye"*** **Warumi 6:8.** Ubatizo ni kifo, kuzikwa na kufufuka; ni mtindo ambao Mungu anatupitishia wakati tumebatizwa.

- Dhambi zetu zote zinasamehewa – ***"Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makossa yote"*** **wakolosai 2:13**.

- Kristo anaishi ndani yangu – "***Maana mimi kwa njia ya sheria niliifia sheria ili nimwishie Mungu. Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena; bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu"*** **Wagaratia 2:19-20.** Kristo anaishi ndani yetu kwa njia ya kiroho na uhakika huu unakua tunapokua katika imani**.**

### Mungu alifanya uweza wa nguvu katika Kristo alipomfufua katika wafu.

1. Mungu anataka kila mwamini azijue nguvu hizo – "***Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho"*** **Waefeso 1:19-20**

2. Nguvu zile zile zinafanya kazi ndani yetu, "***Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu"*** **Waefeso** ***3:20***

### Waliokufa kiroho hupokea uzima wakati wanasikia neno kuhusu Yesu Kristo

Yesu alisema: "***Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai"*** **Yohana 5:25.** Hii inazungumzia wenye dhambi wakija katika uhai wasikiapo neno la Mungu – wanazaliwa mara ya pili.

### Kutakuwa na mambo ya kuonekana ya maisha ya kufufuka katika maisha ya waumini.

- Nia ya imani inaimarishwa na kudumishwa – **Warumi 6:11**
- Maisha mapya yanadhihirika **– Warumi 6:4**
- Bwana mpya anatumikiwa - **2 Wakorintho 5:15**
- Kusudi la maisha mapya linakusudiwa – **Wakolosai 3:1-2**

## KUFUFULIWA KWA KILA MTU ALIYEKUFA

Jambo la tatu la kufufuliwa wafu ni uhakika wa mwisho kwamba wote waliokufa watafufuliwa.

### Wote walio makaburini

**"*Saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu"*** **Yohana 5:28-29**

### Wenye haki na wasio haki

***"Nina tumaini kwa Mungu, ambalo hata hao nao wanalitazamia, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia"*** **Matendo 24:15**

### Ufufuo wa waumini utafanyika lini?

- **"Siku ya mwisho" Yohana 6:39, 40, 44, 54**

- Wakati tunamwamini Yesu. Kuna hali ya kweli ambayo tunaanza kuijua ya maisha ya kufufuliwa wakati kwanza tunamwani Yesu **Yohana 11:25-26**

- Wakati tunabatizwa: Tunabatizwa katika ufufuo wa Yesu Kristo **1Petro 3: 21**

- **"*Walio wake Kristo atakapokuja"*** **1Wakorintho 15:23,** hii inazungumzia kufufuliwa kwa miili ya waumini ambao tayari wemekufa.

- Wafu katika Kristo watafufuliwa wakati ***"Bwana mwenyewe"*** atashuka kutoka mbinguni; hivyo ni, ajapo **1 Wathesalonike 4:16.**

### Ufufuo utafika lini wa wale ambao sio wa Kristo?

***"Saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya wema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu"*** **Yohana 5:28-29**

**Ufunuo 20:12-15:** kifungu hiki kunazungumza wakati ambapo "***kiti cha enzi, kikubwa, cheupe'*** kilionekana, na wale wote waliokufa wakaletwa mbele kwa hukumu. Haya ni maono ya hukumu ya mwisho. Kumbuka maono hayastahili kueleweka kwa njia ya kikawaida.

**Ni nani awafufuaye wafu?**

**1. Wakorintho 6: 14** – Mungu hutufufua ***"kwa nguvu zake"***
**2.Wakorintho 1:9** – "***Mungu awafufuaye wafu"***
**2.Wakorintho 4: 14 – "*Yeye aliyemfufua Bwana Yesu*".**

**Mitume wa kwanza walihubiri kufufuliwa wafu**

**Matendo 4: 2 –** Petro na Yohana **"*Walihubiri katika Yesu ufufuo wa wafu"***
**Matendo 17:18 –** Paulo alihubiri "***Habari za Yesu na ufufuo"***

**Waumini watakuwa na miili ya namna gani?**

**1 Wakorintho 15: 42-49**

- Hufufuliwa katika kutokuharibika (**aya.42)**
- Hufufuliwa katika fahari **(aya. 43)**
- Hufufuliwa katika nguvu **(aya. 43)**
- Hufufuliwa mwili wa roho **(aya. 44)**
- Tutachukua sura yake yeye aliye wa mbinguni (**aya.49)**

**Yesu ataigeuza miili yetu**

***"Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake"*** **Wafilipi 3:21**

**"*Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo"*** **1Yohana 3:2**

**Swali:**

Ni mambo yapi matano ya ufufuo wa kiroho wa waumini?
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

*Aya ya kukariri*: "***Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai" Yohana 5:25.***

## SOMA LA KUMI NA TISA

# HUKUMU YA MILELE

**Kuelewa hatima ya umilele: kuishi milele katika ufalme wa mbinguni na Mungu;** au **kuishi milele kuzimu – kutengwa na Mungu milele.**

Maandiko yanatuambia kuna dhawabu ya wenye haki mbinguni yenye msingi katika huduma na utiifu kwa Bwana wakati wa maisha yao.

Maandiko pia yanatuambia kuna hukumu kuzimu kuhusu vile mtu alikaa na Yesu na ndugu zake.

Yesu anaonya vikundi viwili vya watu:

- "***wale ambao, hawakuwalisha wenye njaa, kuwanywesha wenye kiu, hawakuwakaribisha wageni, hawakuwavika waliokuwa uchi, hawakwenda kuwatazama walio vifungoni"*** **Mathayo** ***25:41-46***
- ***"Wale ambao waliona na kusikia lakini hawakutubu"*** **Mathayo 11: 20-24**

### Ni nani anayehukumiwa

Katika **Yohana 3:16-21** Yesu alisema: "***Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu"*** **aya.8**

***"Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake"*** **Yuda 14-15.**

### Ni nani hatahukumiwa?

Katika **Yohana 5:24** Yesu alisema "***Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni."***

Imani huelekeza uhuru wa hukumu, na hii huleta uzima badala ya kifo. "***Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu ya walio katika Kristo Yesu, wasiotembea katika mwili, bali katika Roho."*** **Warumi 8:1**

### Kuelewa hukumu

#### Waumini

Waumini wanahukumiwa kulingana na "***mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya".*** Maandiko yanasema, ***"kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha kristo"*** **2 Wakorintho 5:10.**

***"Kwa hivyo, tena, ikiwapo tupo hapa, au ikiwa hatupo hapa, twajitahidi kumpendeza yeye"*** **2 Wakorintho 5:9.** Kama waumini tunatakiwa kuishi maisha yetu, tukijua kwamba kuna hukumu ya mwisho ya kutoa hesabu ya jinsi tulihudumu kama waumini.

#### Wasioamini

Wasioamini wamekwisha kuhukumiwa kwa kutokuamini Yesu Kristo. Biblia inaongea juu ya hukumu kuu ambapo wafu wote watahukumiwa na Mungu. Yohana alisema, "***Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa."*** **Ufunuo 20:11-12**

## Jawabu ni gani

Waumini wote watapokea hukumu ya mwisho, lakini jambo lililo la muhimu ni kwamba mara tu tunapokuja katika imani ndani ya Yesu Kristo tunakombolewa kutokana na hukumu, kwa maana Yesu alizichukua dhambi zetu msalabani. Ndiposa lazima tuhubiri injili.

Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu **(Warumi 3:23).** Wote wamevunja sheria ya Mungu. Mshahara wa dhambi ni mauti **(Warumi 6:23):** kifo cha kiroho na cha kimwili kikileta kifo cha kiroho milele.

Tukimwamini Yesu Kristo na tukubali msamaha wa dhambi zetu kupitia dhabihu yake msalabani, tunaokolewa kutoka kwa mauti hadi uzimani. Tunakombolewa kutokana na hukumu ambayo yatufaa.

## Kuna hukumu na dhawabu ya waumini

1. **Uzima wa milele – "*Wenye haki watakwenda katika uzima wa milele"* Mathayo 25:46. *"Ili kila mtu amwaminiye (Yesu Kristo) asipotee, bali awe na uzima wa milele)***

2. **Kutoa hesabu – "*Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu"* Warumi 14:12.** Hatupaswi kuhukumiana mmoja na mwingine, lakini tufahamu kwamba kila mtu anahesabika kwa Mungu.

3. **Mambo yaliyotendwa katika mwili –** "***Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya" 2*** **Wakorintho 5:10.**

4. **Taji ya haki – "*Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufufunuliwa kwake" 2* Timotheo 4:8**

## Kazi za wakristo zitahukumiwa

"***Kazi ya mtu aliyoijenga juu yake ikikaa, atapata dhwabu"*** **1Wakorintho** ***3:14.***

***"Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto" 1*** **Wakorinto 3:15**

## Mbinguni iko namna gani?

- Mungu yuko Mbinguni; mbinguni kumejaa uwepo wake – **Mathayo 6:9**
- Ni enzi ya Mungu; mapenzi ya Mungu hutendeka kikamilifu mbinguni – **Isaya 66: 1**
- Mbigu inatawala dunia -**Danieli 4:26**; mapenzi ya Mungu yanatakiwa kutendeka duniani kama ilivyo mbinguni **– Mathayo 6:10**
- Maisha ya mbinguni ni uzima wa milele – **Yohana 6:51**
- Yesu alikuja kutoka mbinguni **– Yohana 6:51**
- Mbinguni ni mahali pa haki, amani na furaha ndani ya Roho Mtakatifu; tunaweza kujua tabia hizi za mbinguni kwa kuzaliwa tena katika ufalme wa Mungu hapa duniani – **Warumi 14:17**

- Hakuna maumivu, kilio, kifo au huzuni kwa kuwa Mungu yupo na anawaangalia watu wake kikamilifu; hivi ndivyo Yohana anaeleza itakavyokuwa wakati Mungu atakaa duniani na watu wake: mbingu itakuja duniani **– Ufunuoa 21:3-4**

*Ufalme wa Mungu na ufalme wa mbinguni zote zinazungumzia mbinguni. Kwa hivyo maadiko kuhusu ufalme wa mbinguni na kuhusu ufalme wa Mungu zinatusaidia kuelewa jinsi mbinguni ilivyo. Ni kusudi la Mungu mbingu ipate kujulikana duniani. Hii ndiyo injili ya ufalme na ujuzi wetu wa ufalme wa mbinguni unaanza tunapozaliwa tena.*

### Mungu huhukumu aje?

- Kulingana na nuru ambayo watu wamepokea – **Warumi 2:12**
- Kulingana na kweli – **Warumi 2:1-2**
- Kulingana na matendo – **1 Petro 1:17, Ufunuo 20:12**
- Mungu hana upendeleo – **Warumi 2:11**
- Yeye huangalia mioyo – **1Samuei 16:7**
- Katika haki – **Matendo 17:31**
- Kulingana na utiifu wetu katika injili – **2 Wathesalonike 1:8**
- Anawahukumu ambao wanaiharibu nchi **Ufunuo 11:18.**

### Kuzimu kuko namna gani?

- Hukumu ya milele – **Mathayo 25:46**
- Maangamizi ya milele kutengwa na uso wa Bwana – **2 Wathesalonike 1:8-9**
- Ziwa la moto – **Ufunuo 20:15**
- Moto usiozimika na funza wao hafi – **Mariko 9:43-48**
- Mahali ambapo hapana utoshelevu – **Mithali 27:20**
- Mahali pa mauti na uovu – **Zaburi 55:15**
- Mahali pa mateso – **Luka 16:23-24**
- Maisha ya ubinafsi ni mlango wa kuzimu **– Luka 16:25**
- Mahali pa kutengwa na mambo yote mema **– Luka 16:26**
- Mahali pa huzuni **– Zaburi 18:5**
- Upumbazu unaelekeza kuzimu **– Mithali 9:18**
- Mahali pa hukumu **– Mathayo 23:33**

### Dawa ya hukumu ni rehema

Tunatakiwa kuhubiri rehema za Mungu kuu za kuokoa na kusamehe sasa! rehema za Mungu ni kwamba **"*hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafilikie toba*" 2 Petro 3:9.** Watu wanaweza kuokolewa kwa kuja katika maarifa ya kweli (**1Timotheo 2:4).** Tunaweza kuwafikia wengine na ushuhuda wa Yesu, kwanza kupitia maombi na pili kupitia kuhubiri.

*Aya ya kukalili*: ***"Baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake" 2*** **Timotheo 4:8**

**Maswali:**

Andika **Yohana 3:16**……………………………………………………………………..

…………………………………………………………..........................................................

………………………………………………………………………………………………

Aya hii inatufundisha nini kuhusu hukumu ya milele?..............................................................

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

Yesu alieleza kuzimu kwa jinsi gani katika **Mariko 9:43-48**
………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

Ni taji ipi iliyoahidiwa katika **2 Timotheo 4:8**?.......................................................................

**Warumi 14:17** inatuambia aje kuhusu ufalme wa mbinguni?
………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

**SOMO LA ISHIRINI**

# TUKAZE MWENDO ILI TUUFIKILIE UTIMILIFU (Sehemu ya kwanza)

***"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele"*** **Waebrania 6:1-2**

Mara tu misingi inapowekwa, tunatakiwa kuenenda katika utimilifu, hivyo ni, ukomavu kamili. Tunatakiwa kuchukuwa hatua za maandiko kama ilivyowekwa katika fundisho hili, ili tuenende katika ukomavu.

**Kuzitubia kazi zisizo na uhai**
**Imani kwa Mungu**
**Mafundisho ya mabatizo**
**Kuwekea mikono**
**Kufufuliwa wafu**
**Hukumu ya milele**
**Kuenenda katika utimilifu …**

**"*Na hayo tutafanya Mungu akitujalia"*** **Waebrania 6:3**

- **i)** Lazima tuwe watiifu kwa neno la Mungu kutubu na kubatizwa kwa maji;
- **ii)** Tunatakiwa kutembea katika imani, na kufahamu na kutambua uhakika wa kuzaliwa mara ya pili kupitia Roho Mtakatifu.
- **iii)** Tunapokua, tunakuja kutambua uhakika wa ufufuo wa wafu na wa uzima wa milele, tukielewa kuwa uhakika huu huadhili maisha yetu ya kila siku.

### Tumekusudiwa kuwa nini?

Mara tunapoimarishwa katika elimu ya msingi ya mafundisho ya Kristo, tunaandaliwa kukua hata utimilifu. Mungu anasema: ***"Natufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu"*** **Mwanzo 1:26**

Kupitia dhambi mwanadamu ameanguka kutoka kwa mpango wa kwanza wa kusudi la Mungu. Lakini Mungu hajabadirisha kusudi lake. Kwa maana Mungu anatupenda na upendo wa milele, anataka kutuhusisha katika mpango wake wa milele:

- Tumeitwa kulingana na kusudi lake – **Warumi 8:28**
- Tumewekewa hatima tufananishwe na mfano wa Mwana Wake – **Warumi 8:29**
- Tumefanywa haki kupitia kufa na kufufuka kwa Yesu - **Warumi 4:25**
- Tumetukuzwa kupitia kufufuka kwake na kwa kupokea damu yake ya gharama mbiguni na kuiweka katika kiti cha rehema – **Waebrania 9: 11-12, 24**

Mara misingi inapowekwa katika maisha yetu, tunaendelea kubadirishwa kwa mfano wake. Yesu alisema: "***Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba wenu wa mbinguni alivyo mkamilifu"*** **Mathayo 5:48**

**ANDIKO LA KUELEKEZA KATIKA MAISHA MATIMILIFU – Warumi 12:9-21**

Katika kifungu hiki katika **Warumi**, Paulo mtume anatufundisha namna ya kuishi kama wakristo. Anatupa maagizo yenye nguvu katika tabia za imani. Tunafanya vyema kutafakari kuhusu aya hizi na kumuomba Mungu aachilie neema katika maisha yetu ili tuweze kuishi kama wakristo.

1. "***pendo na lisiwe na unafiki"*** **aya 9*:*** upendo ni neno *agape* na ina maana 'hisia ya upendo/ukalimu na kutenda wema.' Ni upendo wa kiungu na ndio upendo ambao tunastahili kuonyesha mmoja na mwingine; ni upendo mkomavu.
   **Yakobo 3:17** inatuambia hekima itokayo juu haina unafiki. Mnafiki ni anayejifanya.

2. ***'Lichukie lililo ovu"*** **aya 9.** Kuchukia ni 'kutopenda kabisa'. Inamaanisha 'kuliogopa jambo'. Hii inahusisha maovu, ambayo yanakidhili kwa runinga, na mitandao. Makinika kwa unacho kitazama

3. **"*Ambatana na lililo njema"* aya 9.** Mke na mme wanapswa kuambatana katika ndoa. Tunapaswa kuambatana na lililo njema kwa uzito ule ule.

4. ***"Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi"*** **aya 10.** Katika agano la kale Mungu alijulikana kwa ukalimu wake na rehema zake nyingi kwetu – ndiye yule hata leo. Katika **2Petro 1:2-11**, Petro anatuambia hatua za ukomavu – kuishi kwa 'nia ya ukalimu' (KJV). Upendano wa ndugu ndiyo hatua ya mwisho kabla uanze kufanya kazi katika upendo wa kweli wa ukristo.

5. ***"Kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu"*** **aya 10.** Paulo anatuambia katika **Wafilipi** "***kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko yeye"*** na ***"kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe"*** **(2:3-4**). Tunatakiwa **"*Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi"*** **1Wakorintho 12:23.**

6. ***"Kwa bidii si walegevu"*** **aya 11 *[***KJV] – "***mkiwa na bidii katika roho zenu"].*** Tunatakiwa "***jitahidini kujionyesha kuwa mmekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli"*** **2 Timotheo 2:15.** Una uhusiano wa kujipatiana kwa neno la Mungu? Ni chakula chako cha muhimu cha kila siku?
   Waamini wanatakiwa kuwa na kazi za kawaida: "***ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula"*** **2 Wathesalonike 3:10.** Inatupasa kufanya kazi na mikono yetu "***akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kitu cha kumgawia mhitaji"*** **Waefeso 4:28**

7. ***"Mkiwa na bidii katika roho zenu"*** **aya 11.** Bidii inazungumzia kujitoa. Wakati mwingine juhudi zetu zaweza kuwa zatoka kwa nafsi na zinaelekeza kufadhaika. Juhudi zetu zatakiwa kuwa jitihada katika roho zetu. Ni neno la Mungu ambalo hugawanya nafsi na roho **(Waebrania 4:12)**

8. ***"Mkimtumikia Bwana"*** **aya 11.** Paulo alisema "***Ni mwabuduye kwa roho yangu katika injili ya Mwana wake"*** **Warumi 1:9.** Kama wana **"*basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi?"*** **Waebrania 12:9.** Maisha ya ukristo huanza kwa kuzaliwa upya na Roho wa Mungu akituwezesha kumpokea Yesu. Tunazaliwa upya tuhudumu.

**9.** ***"Kwa tumaini mkifurahia"* aya 12.** Wengi hufanya makosa ya kuyatumaini mambo ya mda mfupi na wakati ambapo kila wanakitumaini kimekosa matumaini, wanavunjika moyo, tumaini la kweli ni la mambo ya milele, mambo ya ufalme wa Mungu na tumaini la kweli, "***tumaini halitahayarishi" (*Warumi 5:5).** Kama tumaini letu liko katika neno la Mungu, ni kama "***Nanga ya roho"* Waebrania 3:6.** Ni tumaini hili linalotushika ambalo linatuimarisha katika mahali petu katika nyumba ya Mungu **(Waebrania 3:6)**

**10.** ***"Mkifurahi, katika dhiki"* aya 12.** Neno 'dhiki' linamaanisha msukumo. Nina amini ya kwamba mnajua msukumo na changamoto ya maisha lakini pengine hamjui kwamba mambo kama hayo ni dhiki ambayo biblia inazungumzia. Mungu anatupa neema kupitia imani ndani ya Yesu ya "***Ila na tufurahi katika dhiki pia; tukijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini, na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu"* Warumi 5:3-5**. Tambua Pahali pa tumaini na tambua ni nini huleta tumaini.

**11.** ***"Katika kusali, mkidumu"* aya 12.** Maombi yanapaswa kuendeleshwa kama yule mjane aliyefuatilia (**Luka 18:1-8),** ni yule anayefuata kwa kujipatiana ambaye hujibiwa na Mungu. Kuna kuhimizwa kwingi kwa maombi katika agano la kale na lile jipya. je maisha yako yanaambatana na maombi ya kufuatilia.

**12.** ***"Kwa mahitaji ya watakatifu"* aya 13**. Tunatakiwa kufuatilia ukarimu, hata pasina kusahau "***Wakiuza mali yao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote, kama kila mtu alivyokuwa na haja"* Matendo 2:45.** Kila mmoja wetu anatakiwa kuwa na kazi ya kulipwa ili "***apate kitu cha kumgawia mhitaji"* Waefeso 4:28**

**13.** *"**Mkifuata ukarimu"*** **aya 13.** Tunapaswa kufuata ukarimu, hata pasina kusahau "***msisahau kufadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua"* Waebrania 13:2.** Tunapata kutambua kwamba katika nyumbani kwetu na katika kituo chetu cha mafundisho, tukiwa na vyakula vya pamoja katika ushirika ni ya muhimu sana katika kujenga uhusiano katika mwili na kuwajulisha 'wageni' katika shule.

**14a** ***"Wabarikini wanaowaudhi"* aya 14 Yesu alisema, *"Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi"* Mathayo 5:11**

**b**. "***Barikini, wala msilaani"* aya 14. *Yesu alisema, "wabarikini wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi"* Luka 6:28**

**15a** "***Furahini nao wafurahio"* aya 15.** Wakati kiungo cha mwili kikitukuzwa ***"Viungo vyote hufurahi pamoja nacho"* 1 Wakorintho 12:26.**

**b**. "***lieni pamoja nao waliao"* aya 15.** Wakati kiungo cha mwili kinaumia, "***viungo vyote huumia nacho"* 1Wakorintho 12:26**

**16.** ***"Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi"* aya 16.** Tunapo tembea katika utimilifu, "***Natuwaze hayo" …na tuenende katika lilo hilo*" Wafilipi 3:15-16.** kuna mawazo yaliyo komaa - nia ya mawazo- ambayo tunatakiwa kuwa nayo. Tunatakiwa kuwa sawa na mawazo yenye nidhamu, sio kubadirika siku baada ya siku.

17. ***"Msinie yaliyo makuu"* aya 16.** Lakini mmujie Yesu aliye "***Mpole na mnyenyekevu wa moyo" (*Mathayo 11:29).** Tunapaswa kuangusha kila 'kijiinuacho' na ngome ziliomo katika mawazo yetu, na tunatakiwa "***Natukiteka nyara kila fikira, ipate kumtii Kristo"* 2 Wakorintho 10:4-5**

18. ***"mkubali kushughulishwa na mambo manyonge"* aya 16.** Yakobo anatuonya kwamba Mungu "***Alichagua masikini wa dunia, wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidi wampendao"* Yakobo 2:5.** Tunatakiwa kushirikiana na wale ambao Mungu amewachagua. "***Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu alichagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili awaaibishe wenye hekima" 1* Wakorintho 1:26-27.**

19. "***Msiwe watu wa kujivunia akili"* aya 16.** Hekima hutoka juu, na haitegemei uweza wetu, usomi wetu ama jambo letu (**Yakobo 3: 17).** Mungu atapatiana ukarimu kwa wengi kwake atakayeomba kwa imani **Yakobo 1:5-6**

20. ***"Msilipe mtu ovu kwa ovu"* aya 17.** Inasemekana juu ya Yesu "***Yeye alipotukanwa, Yeye hakurudisha matukano"* 1Petro 2:23**

21. **"*Angalieni yaliyo mema machoni pa watu wote"* aya 17.** Paulo anatuagiza kutafakari juu ya "***Mambo yote yaliyo ya kweli… staha … haki…. safi …kupendeza… yo yoye yaliyo ya sifa njema..."* Wafilipi 4:8**

22. **"*Mkae katika amani na watu wote"* aya 18.** Mithali inasema "***Njia za mtu zikimpendeza BWANA, Hata adui zake huwapatanisha naye"* Mithali 16: 7**

23. **a. "*Msijilipishie kisasi"*** kwa nini? Kwa sababu hukumu inaweza kuwa baya na unaweza kuadhibu yule mtu hafai

**23.b** "***Bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitailipa asema Bwana"* aya 19.** Mungu huhukumu kwa haki; anajua moyo wa kila mtu. Ghadhabu upande wetu ni kutafuta kisasi. Mungu anasema "***mwe na hasira ila msitende dhambi"* Waefeso 4:26.** Mungu anatuita kuonyesha rehema na kusamehe, tukimkabidhi aliyetujeruhi kwa haki ya Mungu – **atalipisha**

24. **"*Lakini, adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe; maaana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake"* aya 20.** Tabia kama hii ni kinyume na mtu wa kawaida. Hatutaki kumlisha adui wetu; hatutaki kumnywesha! Lakini Mungu anasema tukifanya hayo ukarimu wetu utaleta hukumu kwa adu wetu asipotubu.

25. ***"Ushishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema"* aya 21.** Yesu "***Kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa"* Waebrania 2:14-15.** Kwa kuwa Yesu ameharibu nguvu za ibilisi **(1Yohana 3:8b),** sisi pia tunaweza kuushida uovu. Mtazamo mdogo twatakiwa kufuata ni: wakati mtu anakuja

kwako na njia ya ukali (nji ya uovu, mjibu kwa njia ya upole. "***Jawabu ya upole hugeuza hasira"*** **Mithali 15:1.**
Yohana anasema "***Kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu"*** na ***"huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu- hiyo imani yetu"*** **1Yohana 5:4.**

*Jadirianeni pamoja maagizo haya na mshiriki ujuzi wenu na changamoto zenu katika kuishi kama waumini wa kweli.*

**Swali:**
Unaweza kusema ya kwamba misingi imewekwa katika maisha yako? Tafadhali elezea:

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

Kuna eneo katika kifungu katika Warumi ambayo inakupa changamoto? Andika ombi, ukimuuliza Mungu akusaidie. Kisha utafurahia wakati utahisi msaada wa Mungu.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**SOMO LA ISHIRINI NA MOJA**

# TUKAZE MWENDO ILI TUFIKILIE UTIMILIFU (Sehemu ya pili)

Kuna vifungu vingi katika agano jipya vinahusisha tabia na njia ya maisha ya waumini wa kweli. Katika somo lililopita tumejifundisha **Warumi 12:9-21** na tukaona magizo mengi ya utendaji jinsi ya kuishi.

Katika kifungu tutakacho soma katika **Wakolosai,** mazingira ni ya kiroho. Unahusisha 'mtu wa kale', ambayo ni asili ya kale ambayo ilitawala maisha yetu kabla ya tuokoke. Na 'mtu mpya' ambayo ni asili mpya ya maisha ya Kristo sasa akiishi ndani Yetu na akiyabadirisha maisha yetu.

## MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO – Wakolosai 3:1-17

Katika njia tofauti na maagizo katika **Warumi**, Paulo anatufundisha katika **Wakolosai 3** jinsi ya kuishi kama wakristo. Anatuambia:

- Yatafutenu yaliyo juu, "***Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu"*** **aya 1.** Kwa njia ya kweli mkisto anatakiwa kukaa akiwa na mtazamo, akiwa na Kriso kama mtazamo kwa maisha Yetu katika kila tutendalo.
  Yesu alituambia kuyafanya hayo "***kwa kuutafuta kwanza ufalme wake, na haki yake"*** **Mathayo 6:33.**

- ***"Yafikirini yaliyo juu"*** **aya 2*;*** hatupaswi kutazama yaliyo ya dunia ambayo hayampi Kristo heshima. **Wafilipi 4:8** inatuambia mambo ya kufikiri.

- ***"Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu"*** **aya 3*;*** tuna maisha ya kiroho ya ndani sasa ambayo ni hakika, ikituwezesha kuishi tofauti. Kama tutakuwa waaminifu kuyatenda haya kuna dhawabu: "***Kristo atakapofunuliwa aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja na yeye katika utukufu"*** **Wakolosai 3:4**

- Hatupaswi tena kuhusika na dhambi za mwili kama: ***Uwasherati, uchafu, tamaa baya, mawazo mabaya, na kutamani"*** **aya 5*.*** ***"kwa ajli ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu"*** **aya 6.** Haya yalikuwa ndiyo maisha yetu, lakini haipo tena.

- **Vua mtu wa kale** – mambo kama hasira, ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu na uongo **aya 8-9.** Mambo kama haya yanaonyesha tabia tulizokuwa nazo bila Kristo. Tunapaswa kuyavua mambo kama hayo sasa na kufuata ***"haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi"*** **2 Timotheo 2:*22.***

- **Vaeni utu upya** – aliyefanywa upya katika ufahamu, moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana na kusameheana **aya 10-13.** Haya ndiyo matendo ya mtu mpya. Tunastahili kuyatenda. Katika asiri yanasikika kama hayawezekani, lakini tukiwa na Kristo akidumu ndani Yetu inawezekana.

- ***“Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndiyo kifungo cha ukamilifu”* aya 14.** Upendo ndio wa muhimu. Upendo ni wa Mungu, “***Kwa maana Mungu ni upendo”* 1 Yohana 4:8.**

- ***“Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu”* aya 15.** Amani hii ni amani ya kiungu ambayo inapita mawazo na hisia. Amani hii inapatikana na *“**kwa kutojisubua kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu”*** **Wafilipi 4:6-7.**

- ***“Ndiyo mlioitiwa katika mwili mmoja”* aya 15.** Mwito wetu ni wa pamoja. Sisi ni sehemu ya mwili na nitunapo fanya kazi katika mwili ambapo viungo vyote vinaweza kufaidiana, ikiwezesha mmoja na mwingine kutembea katika amani.

- ***“Tena iweni watu wa shukrani”* aya 15.** Kuwa na shukrani ni jambo lenye umuhimu sana katika maisha ya ushindi ya ukristo. Kuwa watu wenye shukrani ni neema ambayo inaachiliwa na Roho Mtakatifu. [ona **Waefeso 5:18-21,** zingatia **aya 20].**

- ***“Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu”* aya 16.** Neno la Mungu hufanya kazi ndani yetu kwa nguvu, likituwezesha kufundisha na kuonyana mmoja na mwingine katika Bwana. Hata yanafanyika kupitia kushiriki neno, lakini katika aya hii, kushiriki neno katika “***zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni”.*** Uimbaji wa kiroho ni tabia muhimu sana ya mkristo aliyejazwa na roho [ona tena **Waefeso 5:19]**

- ***“Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, Mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye”* aya 17.** Tuna mawazo tofauti sasa: tunamwishia Mungu, sio kwa ajili yetu.

## MAFUNDISHO YA KWELI

Baada ya maagizo ya **aya 1-17** katika **Wakolosai 3**, Paulo anaendelea kutoa maagizo ya kutenda ya mafundisho ya kweli kwa wake, waume, watoto, akina baba, watumwa [Waajiriwa] na akina bwana [matajiri au waanjiri].

1. **Wake: “*Watiini waume zenu, kama ipendezavyo katika Bwana”* aya 18.** Utiifu wa mke ni katika Bwana; haipo bila masharti; ni ***“katika Bwana”.*** Hii inamaanisha kwamba kama mme anauliza mambo yasiyo ya kiungu kwa mke wake ama anatoa vitisho kwa njia ya ukali na ugumu [kwa vita au maneno], sio sawa yeye kutii kwa vitisho kama hizo.

2. **Waume: “*Nanyi waume, wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao”* aya 19.** Mme anatakiwa kumpenda mkewe “***Kama Kristo naye alivyolipenda kanisa” (*Waefeso 5:25**). Hii inamaanisha kwamba mme anatakiwa kunyenyenyekea na kujipatiana katika kumuinua mkewe, “***Nakumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu”* (1Petro 3:7**). Mme atamkasirikia mkewe tu akiwa na matarajio yasio mema kwake.

3. **Watoto: “*Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana”* aya 20.** Amri kumi zote ni za muhimu, lakini amri moja ina ahadi, na amri hiyo ni “***Mheshimu baba yako na mama yako”.*** Ahadi ni “***Siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako”* (Kutoka 20:12*).***

Hii amri ni ya maisha yetu yote, lakini ina zungumzia watoto wanaokuwa katika jamii – wanatakiwa kufundishwa kuwatii wazazi.
*Kutii*, katika kiyunani agano jipya, inazungumzia 'jinsi ya kusikia'. Wazazi ni lazima wapatiane maagizo kwa watoto na kuweka mipaka inayoeleweka kwao.

4. **Akina Baba:** ***"msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tamaa"*** **aya 21.** Akina baba wengi wana matarajio ya juu sana kwa watoto wao. Wakati mambo yako hivyo, hali huwa ni kuwa wakali wakati watoto hawawezi kuweka viwango vilivyowekwa.
Pia katika nidhamu ya watoto, wazazi hawatakiwi kupatiana nidhamu kwa hasira lakini ifanyike katika upendo. Wakati adhabu inatakikana lazima ipimwe kulingana na kutotii.

5. **Watumwa: "*Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana"* aya 22.** Mtumwa inamaanisha muajiriwa ama mtumishi katika mazingira ya wakati huu. Tunatakiwa kufanya kila kitu kama ni kwa Bwana **(aya 23)*, "mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi, Mnamtumikia Bwana Kristo"* (aya 24).** Wakati tunapokuwa na kutotii kwa mabwana wetu, ni Kristo analipishia, "***Wala hakuna upendeleo*" (aya 25).**

6. **Akina bwana; "*Wapeni watumwa wenu yaliyo haki na ya adili, mkijua ya kuwa ninyi nanyi mna Bwana mbinguni"* Wakolosai 4:1.** Bwana mzuri ni mtu ambaye anamtumikia Bwana Yesu Kristo katika soko, akimtendea mtumishi wake haki na adili.

### Kuendelea kutembea katika utimilifu

Katika **2 Petro,** Petro anatupa ufahamu mwingine na njia ya kukua na kuwa na mazao katika imani. **Aya 5-7**, anatupa hatua saba ambazo tunatakiwa kuchukua tunapokua katika Kristo. Hatutajifundisha hayo sasa, lakini tunapendekeza usome vifungo hizi kwa makini.

Petro anasema: "***Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani"* 2 Petro1:9.** Mambo ambayo tumejifundisha katika sehemu hii ni mambo ambayo tunatakiwa kufanya kama wakristo wa kweli katika Kristo Yesu. Tunatakiwa kulitenda neno la Mungu; tunatakiwa kuishi kulingana na neno la Mungu. Kama sivyo kukiri kwetu kwa wokovu ni bure.

"***Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo"* 2 Petro 1:10-11.** Hebu tuendelee kutenda mambo tuliyosoma katika maandiko. Ushindi wetu ni katika Imani. Tunapoendelea kuamini katika Yesu Kristo, atatupa neema ya kuishi maisha ya ushindi na kubadilisha maisha ya kale na mambo yaliyo kinyume ya maisha Yetu.

## TUKAZE MWENDO ILI TUUFIKILIE UTIMILIFU!

**SOMO LA ISHIRINI NA MBILI**

# KAZI ZA KWANZA ZA KANISA

Katika siku ya pentekosti Petro alipokuwa akihubiri kuhusu Yesu Kristo, kufa kwake, kuzikwa na kufufuka na kuinuliwa katika enzi ya Mungu, wengi wa wale waliokuwa wakisikiza "***wakachomwa mioyo* yao" (Matendo 2:37),** wakiisha kushawishika ya kwamba walikuwa wamemsulibisha Masihi wao. Petro aliwaelekeza jinsi yao kuokolewa. Mwitikio aliotarajia ulikuwa wapate kubatizwa.

"***Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu"* Matendo 2:41.** Ni wale waliopokea neno walitamani kubadilika na kuitikia jinsi walitakikana. Tambua kwamba ubatizo haukuwa chaguo; ubatizo haukuwa kitu cha kufanya baadaye; ubatizo ulikuwa ni jambo la muhimu.

"***Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"* Matendo 2:42.** Kuna mambo matano ya muhimu katika aya hii.

i) **Wakawa wakidumu:** hii inazungumzia kujipatiana kwao katika maisha ya ukristo; hii inaonyesha walibadilisha mambo yao na maisha yao.

ii) **Katika fundisho la mitume:** hii inaongea kuhusu fundisho la mitume; mitume waliendelea kufundisha "***Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (*Mathayo 28:20).**

iii) **Na katika ushirika:** Hii inaongea kuhusu asili ya jamii ya wakristo ambayo ilijiunga siku ya Pentekosti. Waumini **"*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika*" (Matendo 2:44)**

iv) **Katika kuumega mkate:** hii inazungumzia meza ya Bwana, ambayo sasa inaitwa ushirika siku hizi; na pia chakula cha Bwana.

v) **Na katika kusali:** maombi ni ya msingi katika maisha ya mkristo. Maombi ni mawasiliano yetu na Mungu na inatakiwa kufanyika kwa mtu binafsi na kwa mikutano ya maombi.

Mambo haya matano ya maisha ya mkristo inaweka tabia ya msingi ya kanisa la kikristo. Tukijipatiana kwa njia ya kujitoa kwa mafundisho ya kitume, ambayo ni mafundisho ya neno la Mungu, kwa ushirika wa waumini, kwa kushiriki katika meza ya Bwana mara kwa mara na katika maombi, tutajua upendo na uhakika wa Bwana Yesu Kristo kati yetu.

Kwa hivyo fundisho la kitume kwa muktasari ni yale mambo umekuwa ukijifundisha tangu wakati ulianza kukisoma kitabu hiki cha uwanafuzi. Katika sehemu hii tutaangalia kwa kifupi katika asiri ya **ushirika.** Katika sehemu ifuatayo tutafanya utangulizi katika **kuumega mkate** na tena kutakuwa na sehemu katika **kusali.**

## Kudumu katika USHIRIKA

*Ushirika inatoka kwa neno la Kiyunani 'koinonia' SC#2842.*
*Inamaanisha: kugawanya, umoja, ushirikiano wa karibu, kuwa na sehemu pamoja, jumuia ya, ushirika, kuwa na sehemu katita ugamvi, undugu.*

***'Koinonia'***

- *Umoja unaoletwa na Roho Mtakatiofu;*
- *Mtu binafsi anashiriki kwa pamoja umoja wa undani wa ushirika pamoja na wengine katika jamii ya wakristo*
- *Unawashikamanisha waumini kwa Bwana Yesu na mmoja na mwingine*

## Asiri ya ushirika

### Fundisho la mitume

Waumini wa kwanza ***"walikuwa wakidumu katika ushirika"*** wa **fundisho la mitume.** Ni kwa makubaliano ya fundisho la mitume ambayo ilikuwa chanzo kuu ya mabadiliko ya maisha yao. Sote twahitajika kujipatiana katika kudumu katika kusoma na kujifundisha neno la Mungu na haswa kufundisha fundisho la mitume.

Sehemu kubwa ya kanisa la sasa hawajapokea 'fundisho la mitume'. Matokeo ni kwamba fundisho katika makanisa mengi haileti ushirika unaotoshana na ule uliokuwa na kanisa la kwanza.

Ushirika ambao matokeo yake wapendwa wanapokea fundisho la mitume ni **ushirika wa ufunuo na ufahamu wa mapenzi ya Mungu.** Matokeo ni uhusiano wa ndani na wenye dhawabu kwa Mungu na waumini wengine.

### Kuumega mkate

Waumini wa kwanza "***wakawa wakidumu katika ushirika"*** wa **kuumega mkate.** Walishirikiana mara kwa mara katika kuumega mkate, hata kila siku, "***na sikuzote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakiumega mkate nyumba kwa nyumba" (Matendo 2:46).*** Vile vile wakishiriki katika meza ya Bwana, walikula chakula chao pamoja. Katika kanisa la kwanza meza ya Bwana ilishirikishwa katika mazingira ya chakula cha ushirika cha waumini pamoja.

Kukuja pamoja katika kushiriki meza ya Bwana mara kwa mara inawezesha ushirika wa wapendwa kuwa wa karibu na wazi. Mtume Yohana anatuambia, "***bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" 1 Yohana 1:7.***

Tunaposhiriki meza pamoja, ni nafasi ya kuondoa katika mioyo yetu kila nia ya dhambi kwa wengine. Kuumega mkate inahakikisha ushirika wazi kati ya waumini.

### Kusali

Waumini wa kwanza "***Walikuwa wakidumu katika ushirika"*** wa **kusali.** Kanisa la kwanza mara kwa mara walisali pamoja. Tunazoezi la kufanya maombi ya pamoja mara kwa mara katika huduma yetu na ushirika.

Kuna mengi ya kujifundisha katika ushirika wa maombi, hivyo ni kujifundisha kuomba pamoja katika njia yenye maana na yenye nguvu ukiongozwa na Roho Mtakatifu.

Wakati tunajifundisha kuwa wanaofaulu katika maombi yalioshirikishwa, tunaona Mungu akitupa dhawabu wazi. Ushirika wa maombi ni kiungo chenye nguvu sana katika maisha ya kanisa, na unahitaji zoezi na kuendeleshwa.

- **Kuangaliana na kushirikiana**

***"Na wote walioamimi walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja"* Matendo 2:44-45.**

Kanisa la kwanza walikuwa na jamii yenye nguvu ambapo kila mshiriki alikuwa anashughulikiwa na washiriki wengine, asiri ya ushirika ilikuwa ni katika kiwango cha ndani katika **kuangalia** na **kushirikiana.** Mahitaji ya kila mshirika yalikutanwa nayo na washirika wengine wa jamii ya wakristo.

### Ugamvi wa pesa unasimamiwa na mitume

Msaada wa ugamvi wa fedha ulisimamiwa na mitume ambao walikuwa ni viongozi wa kanisa, wakiwa wamechaguliwa na Yesu. "***Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa, wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji"* Matendo 4:34-35**

### Wajane waliangaliwa

Katika **Matendo 6,** tunasoma kwamba kanisa la kwanza lilihusika sana katika maisha ya kawaida: kulikuwa na ugamvi wa kila siku wa vyakula kwa wajane **(Matendo 6:1).** Mitume walijipatiana kwa shughuli hii na kwa sababu huduma hii ilikuwa kubwa sana, walichagua viongozi wengine saba kuangalia shughuli hiyo **(Matendo 6:2-6).**

### Fungu la kumi na sadaka

Sehemu ya muhimu katika ushirika ni mchango wa pesa wa washirika wa kanisa. Wengine wanaongozwa na Roho Mtakatifu kuuza nyumba na mali zao na kutoa mali yao kwa mitume ili waumini wapate kugawiwa **(Matendo 2:45; 4:34).**
Hata hivyo jia ya kibiblia ni kuchanga kwa sababu ya kushughulikia mahitaji na kusimamia mahitaji ya jamii ya wakristo, kuhakikisha kwamba kazi ya huduma inaendelea, ni kupitia **<u>kila mshiriki akileta mchango wake wa fungu la kumi</u>** ya pato lao.

## Fungu la kumi

Tabia ya fungu la kumi imetajwa kwa biblia katika **Mwanzo 14:18-20** ambapo Ibrahimu baba wa imani, alitoa fungu la kumi kwa Melkizedeki. Melkizedeki alikuwa ni mfano aliyetokea Ibrahamu, akimwakilisha Yesu Kristo.

Fungu la kumi lilihitajika chini ya sheria ya Musa lakini sisi kama wakristo hatuko chini ya sheria kwa njia hiyo.

### Mungu aliahidi kubariki

**Malaki 3:10-12** inaongea kuhusu fungu katika msingi wa kujitoa, Mungu anatoa changamoto kwetu "***Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo…mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la"* aya 10.**

### Fungu ni kwa imani

Fungu la kumi kwa waumini ni jambo la imani: mara tumepokea ufunuo wa Yesu Kristo, tunaitikia kwake kama Mungu kwa njia ya kumtolea fungu la kumi ya yote tunayopokea. [ Zaka ni Fungu la kumu, chochote tunachopokea tunatolea Mungu sehemu ya kumi ya kwanza].

**Ghala**

Tunatoa fungu la kumi kwa wale wahuduma ambao wanatuongoza na kutuelekeza katika kutembea kwetu na kutulisha neno la Mungu.

**Sadaka**

Sadaka ni kwa hiari na inatolewa kwa kujitoa kulingana na uamuzi wa mwenye kupeana. Katika makanisa mengine ama huduma, msukumo inafanywa kwa watu kutoa hata zaidi ya uweza wao na wakati mwingine kunakuwa na ahadi za uongo kwa mwenye kutoa, iwe makini kwa tabia hizo zisizo takikana.

Kama umeshawahi kushurutishwa kutoa, unaweza kuhakikishiwa kwamba hilo halijatoka kwa Bwana, lakini linatokana na watu ambao wanataka pesa yako.

*Aya ya kukariri: "**Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali" Matendo 2:42.***

**SOMO LA ISHIRINI NA TATU**

# KUUMEGA MKATE

- Kuumega mkate inazungumzia **Meza ya Bwana**
- Pia inaitwa **chakula cha Bwana**
- Katika kanisa la sasa inaitwa **ushirika mtakatifu**

## Chakula cha pasaka

### Ilipeanwa usiku ambao Yesu alisalitiwa

Yesu Kristo alitupa chakula cha Bwana usiku ambao alisalitiwa na Yuda iskariote; huo ni usiku kabla yake kwenda msalabani. Yesu alikuwa amekusanyika na wanafunzi wake kwa chakula cha pasaka.

### Chakula cha kumbukumbu

Pasaka ilikuwa ni chakula cha kumbukumbu ambacho Wayahudi, kama watu wa Mungu, walikuwa wawe wanakumbuka kila mwaka katika kukumbuka ukombozi wao kutoka Misri. Baba zao walikuwa watumwa katika nchi ya Msiri na Mungu akamtuma Musa kuwaongoza kutoka. Ukombozi wa kweli wa Waisrseli ulilетwa na Mungu akileta njia ya ukombozi kupitia kumwagwa damu ya mwana kondoo. Tukio la kihistoria lililonakiliwa katika **Kutoka 12.** Chukua mda usome sura hii kuelewa hio pasaka ya kwanza.

### Kuokolewa kwa damu, kutiwa nguvu na mwili wa mwana kondoo

Kila nyumba ya Mwisiraeli ilikuwa imchukue mwana kondoo, wamwage damu yake na wazile nyama zake. Damu ilikuwa ipakwe kwenye miimo na kizingiti cha juu cha kila nyumba, na washiriki wa nyumba walikuwa wakusanyike, wakiwa wamevaa tayari kusafiri, na wale mwili wa mwana kondoo ili wapate nguvu katika safari yao. Jambo la kushangaza ilikuwa kwamba damu juu ya milango ya nyumba ililinda nyumba nzima kutokana na kifo. Kila nyumba katika Misri ambayo haikufunikwa kwa damu ilienda hasara ya wazaliwa wa kwanza.

### Yesu ndiye Mwana kondoo wa Mungu

Haya ndiyo mazingira ambayo Bwana Yesu alitupa chakula cha Bwana. Yesu alikuwa akiwaonyesha wanafunzi wake ya kuwa alikuwa awe timilizo ya pasaka ya Agano la kale.

Wakati Yohana mbatizaji alimwona Yesu, alimtambua kama "***Mwana – kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"*** **(Yohana 1:29).** Yesu ndiye Mwana kondoo aliyemwaga damu yake na akautoa mwili wake kwa uponyaji wetu na nguvu.

### Kuimarishwa kwa chakula cha Bwana

Kumenakiliwa katika:

**Mathayo 26:26-30**
**Mariko 14:22-26**
**Luka 22:14-20.**

Kunakiliwa huku katika injili tatu kunathibitishwa na mtume Paulo katiak **1Wakorintho 11: 23-26.** Paulo anapatiana maagizo zaidi kuhusu meza ya ushirika katika **aya 27-34.**

### Vitu vinavyotumika katika chakula cha Bwana

- **Mkate**

***"Bwana yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu, fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu"* 1Wakorintho 11: 23-24**

Mkate unawakilisha mwili wa Yesu. Kila mara tuulapo mwili tunatakiwa kumkumbuka Bwana Yesu.

- **Kikombe**

"***Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu"* 1 Wakorintho 11:25.**

Kikombe kinawakilisha damu ya Yesu. Damu yake inaweka muhuri agano jipya, ambayo ni makubaliano ya Mungu na mwanadamu, ambapo Mungu anatusamehe kwa sababu ya damu ya Yesu na anatuleta katika uhusiano wa maagano naye. Damu ilimwagwa ***"Kwa sababu ya ondolea la dhami"* (Mathayo26:28).**

#### Kumkumbuka Yesu.

1. Katika kila pahali palipotajwa meza ya Bwana, kuumega mkate na kukinywea kikombe zimepatianwa **kwa ukumbusho wa Yesu**
2. Mara ngapi twapaswa kumkumbuka Yesu**?** Kanisa la kwanza walimkumbuka Yesu **kila siku.** Walimega mkate **"kila siku" (Matendo 2:46)**
3. Kanisa la kwanza waliumega mkate wapi? "***Nyumba kwa nyumba*" (Matendo 2:46)**

#### Kushiriki chakula cha ushirika

Kumega mkate katika maandiko sanasana iko katika mazingira ya wanafunzi, na baadaye waumini, wakishiriki chakula cha ushirika. Yesu alitupa meza ya Bwana katika mazingira ya chakula cha pasaka, na Paulo anaelekeza katika **1Wakorintho 11** na katika mazingira ya kanisa likiumega mkate katikati ya chakula cha ushirika. Katika **Matendo 2:46**, kanisa la kwanza lilimega mkate na walikula chakula cha ushirika pamoja.

#### Tendo linalofanyika nyakati hizi

Tendo linalotendeka katika kanisa leo ni kuwa na ushirika kama chakula cha kumbukumbu kwa kunywa kutoka kikombe na kisehemu kidogo cha mkate au bisikuti kuutambua mwili na damu ya Yesu na kukumbuka sadaka yake kwetu. Sio tambia inayo patikana kuwa na ushirika/meza kama sehemu ya chakula ushirika. Hata hivyo zaidi na zaidi waumini wanaporejesha mikutano ya nyumbani, katika vikundi vidogo, inakua inaonekana kuwa na ushirika/meza katika mazingira ya chakula cha ushirika.

#### Kuja kwake

Tunatakiwa pia kukumbuka, hivyo ni, kuweka kwa mawazo yetu kuja kwake, "***Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo"* (1Wakorintho11:26).** Mara kwa mara kimakosa meza ya Bwana inaleta jambo katika mawazo ya kukumbuka dhambi zetu. Hatutakiwi kuweka mtazamo kwa dhambi zilizopita, lakini tukumbuke ushindi wa kifo cha Bwana na kufufuka na kutazama ndani ya mioyo yetu, tukiwa tayari kwa kuja kwake.

### Tunastahili kunywa kinywaji kipi?

Wakati Yesu alianzisha meza ya Bwana, alisema, "***Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu*" (Mathayo 26:29).** Uzao wa mzabibu ni kitu kama divai kwa hivyo leo wengi hutumia kinywaji cha divai. Hata hivyo vinywaji vingine vyaweza kutumika ambapo hakuna uzao wa mzabibu.

### Ni mkate upi uliokubalika?

Yesu alitumia mkate usio na chachu ambayo ni sehemu ya chakula cha pasaka. Mkate usiotiwa chachu ulitumika na waisraeli kwa nyakati spesheli kulingana na maagizo ya Mungu.
Baadhi ya makanisa wanaiweka kama sheria kutumia mkate usio na chachu katika meza ya Bwana, lakini hakika, kusudi la kuumega mkate ni kumkumbuka Yesu, sio kuzingatia baadhi ya sheria za kidini. Kwa hivyo aina yoto ya mkate au nafaka/ biskuti inakubaliwa kwa maana hitaji ya yote kumkumbuka Yesu mara kwa mara, ikiwezekana kila siku. Kwa hivyo, tunaweza kwa heshima kumkumbuka Yesu kila wakati tulapo na tunywapo.

### Ni nani anaweza kushiriki katika kuumega mkate?

Kotekote katika historia ya kanisa, watu wameweka sheria kuhusu meza ya Bwana. Nyingi ya tabia zetu imekuwa imerithiwa kutoka kwa watu na imezuia ukweli na uhakika wa kuumega mkate na heshima yake ya undani katika kutembea kwetu na Bwana Yesu.

### Watoto

Kila mwamini anakaribishwa kwa meza ya Bwana, ikihusisha watoto. Unaweza kufikiria Yesu akija kwa nyumba yako na kula na kunywa nawe na kuwafukuza watoto wako?

Wakati Mungu alitoa maagizo ya kula mwana kondoo wa pasaka katika Misri, aliwatenga watoto? Wangeenda na njaa? Kusudi la kula mwili wa mwana kondoo ilikuwa ili watiwe nguvu jamii yote katika safari.

Je watoto hawakulindwa na damu ambayo ilikuwa katika milango ya nyumba? Hakika walilindwa – hakuna mtoto wa jamii ya Waisraeli aliyekufa usiku huo.

### Waumini waliobatizwa pekee?

Je Habari ya waumini wasiobatizwa? Tena hakuna sheria katika biblia ambayo inawatenga watu kwa meza. Tunakula na kunywa kwa imani.

Zaidi, kunatakiwa kuwe na waumini wasiobatizwa tu kwa sababu hapakuwa na nafasi ya kubatizwa. Katika kitabu cha Matendo, wale walioamini walibatizwa siku hiyo hiyo, kwa hivyo hapakuwa na waumini wasiobatizwa katiktia yao.
Leo tunatakiwa kurejelea tabia ya kimaandiko ya kuwabatiza waumini wapya mara moja.

## Ni nani anaweza kuhudumu katika kuumega mkate?

### Wote ni makuhani

Jambo la kusikitisha ni kwamba kanisa imeweka na kukubari kuwe na nafasi ya wahuduma ambao wametengwa na watu wa Mungu na wameweka huduma nyingi za kiroho na za kidini kuwa wajibu wa wahuduma waliosimikwa peke yao. Hapana migawanyiko kama hiyo katika kanisa la Agano Jipya, na katika uhakika wa maandiko, sisi ni "***Wafalme na makuhani*" Ufunuo 1:6).** Kwa hivyo kila mshiriki wa mwili wa Kristo anaweza kuhudumu meza ya Bwana**.**

## Jambo kubwa ni kumkumbuka Yesu!

Tunahimiza kumega mkate kutoka nyumba kwa nyumba, kila siku, hakuna sheria ya dini. Jambo kubwa katika kumega mkate ni **kumbukumbuka Yesu Kristo, kifo chake, kufufuka kwake kwenye utukufu na ahadi ya kuja kwake!**

**Maswali:**

Ni vitu vipi viwili vya muhimu katika meza ya Bwana?.........................................................

Vitu hivi vinawakilisha nini?

1)…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..

2)…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..

Ni nini kilichonakiliwa katika maandiko cha msingi katika meza ya Bwana?

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

SOMO LA ISHIRINI NA NNE

# MAOMBI NI NINI?

## Maombi – mawasiliano na Mungu

- Maombi ndio njia ambayo Mungu amempa muumini ya **kuwasiliana** naye.
- Maombi ni **mazungumzo:** ni mawasiliano kwa njia mbili, ikihusisha kuongea na kusikiliza.
- Ni kwa kuwasiliana na Mungu ambapo muumini **anadumisha uhusiano wake** naye.
- Kupitia maombi, muumini **anayatambua mapenzi ya Mungu.**
- Ni kwa **utiifu wa mapenzi ya Mungu** ambapo muumini anasongeza ufalme wa Mungu.
- Kwa muumini, maombi yanafanyika **njia ya maisha.**

## Maombi – uhusiano na Mungu

Kujenga uhusiano na mtu, tunatakiwa kutumia mda na huyo mtu; vivyo hivyo kukua katika uhusiano na Mungu tunatakiwa kutumia mda naye katika maombi.

➢ **Yeye ni Baba yetu**

Yesu alitufundisha tuomuombe Mungu kama Baba yetu, "***Msalipo, semeni: Baba yetu uliye mbinguni"*** **Luka 11:2.**

➢ **Omba ukiamini**

Tunatakiwa kuomba tukiwa na imani ndani ya mioyo Yetu, "***Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote"*** **Yakobo 1:6.**

➢ **Kaa ndani yake**

**"*Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa"*** **Yohana 15:7.** Hii inatokana na uhusiano naye. Kama maneno yake yanakaa ndani yetu basi tunaweza kuomba neno lake; tukimkumbusha yale ambayo ameyasema katika neno lake. 'Baba, neno lako lasema…."

➢ **Tuna shukrani**

**"*Mkimshukuru Baba, aliye wastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru"*** **Wakolosai 1:12.** Maandiko yanatuhimiza tuombe bila kukoma katika mazingira ya shukrani kwa Mungu kwa yale yote ametutendea.

## Yesu ndiye mfano wetu

Yesu alijua umuhimu wa kuwa na uhusiano na Mungu. Yesu mara kwa mara aliendа falagani kumwomba Baba yake, "***ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu"*** **Luka 6:12.**

### Yesu aliyajua mapenzi ya Mungu katika maombi

Ilikuwa ni katika wakati fulani wa maombi ya ndani katika kuyatafuta mapenzi ya Baba ambapo aliwachagua wale thenashara ambao walifanyika mitume wake **(Luka 6:12-13).** Wakati unatenga mda kumtafuta Mungu, tarajia aseme nawe.

### Yesu alijiandaa kwa huduma yake katika maombi

**Mariko 1:35** inatuambia "***Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko".*** Baada ya mda huu wa maobi aliwaambia

wanafunzi wake, “***Twenendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nilitokea” (*Mariko 1:38).**

**Yesu alijiandaa katika dhiki kuu katika maombi.**

Katika shamba ya Gethisemane, Yesu “***Akaanza kuhuzunika na kusononeka” (*Mathayo 26:37).** Akaibwaga Roho yake kwa Mungu katika maombi **(aya 38-44).** Akajilainisha kwa mapenzi ya Mungu kupitia maombi ya kuendelea.
Mungu alituma malaika kutoka mbinguni amtie nguvu Yesu **(Luka 22:43).**

## Tunaomba namna gani?

### 1. Kustahimili katika maombi

Yesu alifundisha kwamba ni lazima tustahimili katika maombi, “***Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa”* Luka 18:1.** Soma mfano wa mjane ambaye hakukata tamaa kutoka **Luka 18:2-8.** Ni kwa nini mwanamke huyo ilisikizwa?

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

### 2. Omba kwa imani – ukitarajia jawabu

“***Walakini, atakapo kuja Mwana wa Adamu, je ataiona imani duniani?”* Luka 18:8.** Mungu anawatafuta watu wa imani.

**Yakobo 5:16** inatuambia “***Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana”.*** Haki yetu inatokana na kumwamini Yesu Kristo. Wakati tunaomba kwa imani tunaweza kutarajia kuona maombi yaliojibiwa.

### 3. Omba, ukiamini

“***Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote muombao mkisali, amini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu”* Mariko 11:24.** Tuombapo tunatakiwa kumuuliza Roho Mtakatifu jinsi itupasavyo kuomba, au cha kuomba. Kisha tunaweza kuomba tukiamini, kwa kuwa tunaomba kulingana na mapenzi Yake

### 4. Omba kwa jina lake

Tunatakiwa kujuwa na kufahamu nguvu za jina Lake. Jina lake ni YESU!

“***Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya”* Yohana 14:13-14.** Hakuna jina lingine ambalo twaweza kuokoka kwalo, kuponywa, kukombolewa. Tunatakiwa kukiri jina lake, jina ambalo liko juu ya kila jina.

### 5. Omba kwa mamlaka

Tunatakiwa kuyajua mamlaka ambayo tumepewa na Yesu na tuombe na uhakika wa mamlaka hayo. “***Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.”* Luka 10:19.**

**Swali:**

Andika maelezo yako ya sala/maombi

…………………………………………………………..........................................................................

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

## SOMO LA ISHIRINI NA TANO

# SALA YA BWANA {SEHEMU YA KWANZA}

Katika maandiko ya Luka kuhusu sala ya Bwana, wanafunzi waliuliza Yesu: "***Bwana tufundishe sisi kusali kama vile Yohana aliwafundisha wanafunzi wake" Luka11:1.*** Katika **Mathayo 6:9,** Yesu alisema: "***Basi ninyi salini hivi:"***

Kote katika historia, ombi hili limekaririwa na mioyo mieupe na imani kuu. Na pia imetumika kama muundo wa maombi katika maisha ya kanisa. Lakini jambo la kusikitisha, wakati mwingine imeombwa tu kutoka kwa kumbukumbu kama jambo la kidini bila kutambua nguvu za maombi.

Katika mafundisho yake, Yesu ametupa tamatisho ya mambo muhimu ambayo yanapaswa kuombwa na waumini. Haya mambo ni hakika katika maisha yetu.

Katika fundisho hili, tutatazama na kutafsiri kila aya kulingana na maandiko, ili uweze kuomba kwa mwangaza na ufahamu.

### A.) MTAZAME MUNGU, KUJA KATIKA UHUSIANO NAYE

***"Baba yetu"***

Yesu anatuvuta katika uhusiano wa kijamii na Mungu mwenye nguvu zote, muumba wa mbingu, kupitia yeye mwenyewe. Tunapaswa kumuita Mungu, "Baba yetu"

Tunapokea ***"Roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba"*** **Warumi 8:15.** Roho wa Mungu ambaye yuko ndani yetu, anamfunua Mungu kwetu.

Tunapewa uhakika wa mahali katika jamii ya Mungu. Tunapotazama uhusiano huu, tunashangaa tunapotambua urithi ambao tumepewa. "***Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu"*** **1 Yohana 3:1.**

### Mungu yuko "mbinguni".

Mungu hukaaa mbinguni, nyumbani Pake pa milele***. "Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni pahali Pangu pa kuweka miguu yangu"*** **(Isaya 66:1).** Tunamwona Mungu katika utukufu wake akiwa ameinuliwa juu, mtu huyu ndiye nitakayemwangalia na kupenda kudumu naye, mwenye roho iliyopondeka **(aya 2).**

Tunakumbuka Yesu alikuwa amefufuka tayari na ameketi katika mkono wa kuume wa Mungu katika maeneo ya mbinguni (**Waefeso1:20);** na ametufufua na ***"akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu"*** **(waefeso 2:6).**

**"*Wenyeji wetu uko mbinguni"*** **(Wafilipi 3:20)** na tunatakiwa kuyaweka mawazo yetu yakivitazama vitu vya mbinguni "***Yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu"*** **(Wakolosai 3:1-3)** na tunatakiwa kuyatoa macho yetu kwa vitu vya dunia na kutazama utawala wa Mungu wa mambo yote.

### Baadhi ya maandiko yanayoelezea mbinguni

Sio Ezekieli wala Yohana ambao wote wawili walipokea maono ya Mbinguni wangepata maneno maalum ya kuelezea mbinguni waliyoyaona katika maono yao. Wanasimulia kuhusu vitu ambavyo "ni mfano" "zikionekana kama" **(Ezekieli 1: 27-28).** ***"Kama kuonekana kwa upinde wa mvua, ulio katika mawingu siku ya mvua, ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwa mwangaza ule pande zote. Ndivyo kulivyokuwa kuonekana kwake mfano huo wa utukufu wa BWANA"*** **aya 28.**

Tumepewa picha ya pahali pa uzuri usioelezeka na tunaweza kutafakari ambayo wanaeleza:

- Wanaokaa huko huabudu bila kukoma **(Ufunuo 5:14)**
- Utukufu wa Mungu na wa Mwana kondoo hupatiana nuru **(Ufunuo 21:23)**
- Enzi ya Mungu iko kati **(Ufunuo 4:2)**
- Vijito vya maji ya uzima vinatiririka kutoka kwa enzi hii **(Ufunuo 22:1-2)**

Hapa ndipo tumewekewa tuwe tunaishi: katika enzi ya Mungu, tukiyapokea maji ya uzima kwa roho zetu. Yesu alituandalia pahali hapa alipoenda msalabani. Sasa kupitia kuzaliwa upya, ametuvuta kwake tuwe naye katika roho.

## B.) TUNAMUABUDU MUNGU KWA KULIHESHIMU JINA LAKE

***"Jina lako litukuzwe."***

Jina lake ni spesheli. Yesu anatwambia tulisifu na kuliheshimu Jina la Mungu. [***kutukuza: inamaanisha kufanya takatifu, kuonyesha heshima, kuwa takatifu, kutenga. Gk.#37SC]***

Tunazo picha nzuri sana za kuabudu mbinguni mahali ambapo viumbe mbinguni wanamtukuza Bwana. ***"Wala hawapumziki mchana wala usiku, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja!"*** **Ufunuo 4:8.**

### Jina la Mungu

Mungu alimwambia Musa jina lake ni "**MIMI NIKO AMBAYE NIKO" (Kutoka 3:14).** Kutoka wakati huo Mungu amejifunua kwa jina lake kwa njia nyingi katika hali nyingi. Jina lake linafunua asili yake na tabia yake.

### Majina kadha ya Mungu:

- **YEHOVA – Yire:** BWANA anipeaye **(Mwanzo 22:14)**
- **YEHOVA – Rophe:** BWANA aniponyaye **(Kutoka 15:26)**
- **YEHOVA – Nisi:** BWANA bendera yangu **(kutoka 17:15)**
- **YEHOVA - M'Kaddesh:** Mimi ni BWANA nikutakasaye **(Mambo ya walawi 20:8)**
- **YEHOVA – Shalom:** BWANA ni amani **(Waamuzi 6:24)**
- **YEHOVA - Tsidkenu:** BWANA haki yetu **(Yeremia 23:6)**
- **YEHOVA - Rohi:** BWANA ni mchungaji wangu (**Zaburi 23:1)**
- **YEHOVA – Shammah:** BWANA yupo, yuko nasi (**Ezekieli 48:35)**

### Jina la Yesu

**"N*aye itaitwa jina lake mshauri, wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani" (*Isaya 9:6).**

**"*Bikira atachukuwa mimba, atamzaa mtoto mwanamume, naye atamuita jina lake Imanueli"* (1saya 7:14).** Mungu ako pamoja nasi.

#### Wadhifa kamili aliopewa Yesu

**Bwana –** aliye mkuu katika mamlaka, mwelekezi, mkubwa
**Yesu –** Yehova ni wokovu
**Kristo –** Masihi, aliyeahidiwa

Jina lake linapotabuliwa hakika Baba anatukuzwa, kwa sababu jina la Yesu ni jina la Bwana katika agano jipya.

### Jina lililo juu ya majina yote

**"*Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ikiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba"* (Wafilipi 2:9-11).**

Katika Yesu, Mungu ametimiza yale yote alifunua katika Agano la kale. Katika kweli, Bwana Yesu amefanyika anayenipa, mponyaji, bendera yangu, haki yangu, amani yangu, anitakasaye, mchungaji wangu, kila kitu changu.

Yesu ametutangazia jina la Baba **(Yohana 17:26),** ambayo kwa hakika ni Jina lililopewa Mwana.

Yesu aliomba kwamba Baba atuweke(kutulinda) kwa Jina lake **(Yohana 17:11).**
Kuna usalama na ukombozi kupitia kwa Jina lake. "***Jina la BWANA ni ngome imara; Mwenye haki huikimbilia, akawa salama"*** **(Mithali 18:10)**

Tunapoliinua jina lake juu, yesu atawavuta watu wote kwake (**Yohana 12:32).** Tunapomsifu Mungu na kulitukuza jina lake tunawapatia wengine nafasi ya kumsikia na hivyo nafasi ya kumjua.

## C.) TUNAOMBA UFALME WAKE UJE

### "*Ufalme Wako Uje"*

Tunaomba ufalme ambao utaonyesha maandili yote ya Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana **(Ufunuo19:16).** Ni mfalme huyu pekee aliye na haki kuuliza kuabudiwa kwa kiungu. Yohana mbatizaji aliwaandaa watu kwa kuja kwa Yesu akiwaonya kwamba "***Ufalme wa mbinguni umekaribia" (*****Mathayo 3:2).** Yesu alianza huduma yake kwa kuhubiri toba "***Kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia" (*****Mathayo 4:17).** Kwa njia nyingine ufalme uje (ulifunuliwa) katika Yesu, aliye mfalme.

Tunaomba utawala na mamlaka ya Mungu zidhihirishwe duniani. Ufalme wa Mungu ni wa milele lakini kupitia Yesu, ufalme umeimarishwa duniani katika uhakika na inayohisiwa. Lazima tuzaliwe mara ya pili kuona na kuingia ufalme na kuyaishi maisha yetu katika utawala wa Mungu.

## D.) TUNAOMBA MAPENZI YAKE YATIMIZWE

### "*Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni"*

Tunatambua jinsi mapenzi ya Mungu yalivyo kupitia neno lake- Biblia. Neno la Mungu linatugeuza mawazo yetu ili "***Mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kupendeza, na ukamilifu"*** **(Warumi 12:2).**

Tunatakiwa kuelewa **"*ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana"* (Waefeso 5:17).** Tunapo pokea ufunuo kupitia kwa neno la Mungu, tunazidi kufanyika zaidi kama Yesu, na mapenzi ya Mungu yanafanyika duniani.

Neno la Mungu linadhihirisha mapenzi yake kwa:

- Walio katika mamlaka: ni mapenzi ya Mungu wapate kuokolewa **(1Timotheo 2:1-6)**
- Wote wapate kuokolewa (**1Timotheo 2:4, 2 Petro 3:9).**
- Wafuasi wake wapate "***Kuenenda na kufanya mataifa wote kuwa wanafunzi" (*****Mathayo 28:19-20)**
- Waumini waishi katika ushindi **(1Yohana 5:4-5)**
- Haki na amani zifunike dunia **(Warumi 14:17)**
- waumini "***Kufanikiwa katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo"*** **3 Yohana 2. [afya** inazungumzia kuwa na mafundisho mema, kuwa na neno lisilogoshiwa, imani isiochanganywa.]

**Shiriki ufahamu wako wa ombi la Bwana mpaka hapo:**

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

**SOMO LA ISHIRINI NA SITA**

# SALA LA BWANA {SEHEMU YA PILI}

### E.) TUNAMUOBA BWANA RIZIKI YETU

"***Utupe leo riziki yetu".***

Riziki yetu ya kila siku ni nini? Yesu anatuambia tusijisumbue kwa jambo lolote kuhusu mahitaji yetu ya mda mfupi katika **Mathayo 6:25- 32.** Tafadhari soma na utaona ni mara ngapi ambayo Yesu amatuambia **tusijisumbue**

Ni mambo gani ambayo hatupaswi kusumbukia?

..............................................................................................................................................

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Yesu anatuahidi kwamba tukitafuta kwanza ufalme Wake, kisha haya yote mengine tutaongezewa (**Mathayo 6:33).**

Mungu anatamani watu wote wawe watu wake na wafurahie kushughulikiwa naye. Katika **Mathayo 6:25-32,** Yesu anaweka wazi ya kwamba Mungu anataka wote wapate kulishwa na kuvikwa na kuwa na makao. Katika ulimwengu wa leo, tunaweza kumuomba Mungu kwa elimu ya msingi ya watoto wetu kwa maana wote wanatakiwa kuwa na uweza wa kusoma. Hii ni ya muhimu: kila mkristo anaweza kuomba, Mungu kwa ujasiri, zikiweko shukrani, kwa mahitaji yao ya kila siku ya riziki, mavazi, makao, na hata masomo kwa watoto wetu.

### Mkate wa kweli wa uzima ni mtu

**"*Kwa maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima"* Yohana 6:33.** Yesu ndiye mkate wa uzima. Tunatakiwa kula na kunywa uzima wake.

Soma **Yohana 6:50-56,** na unakili mambo ya muhimu ambayo Yesu anasema kuhusu uzima.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Yesu alisema: "***Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima" (*Yohana 6:63).**

Pamoja na kumwomba Mungu kwa imani kwa sababu ya mahitaji yetu, tunahitaji pia kumuomba Mungu kwa mahitaji yetu ya kiroho ya kila siku. Neno lake ni chakula cha kujenga roho zetu na nafsi zetu.

Tafadhali andika **Mathayo 4:4**

………………………………………………………………………………………….........

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

### F.) TUNATAFUTA MSAMAHA

**"*Utusamehe deni zetu, kama sisi tuwasamehevyo wadeni wetu"***

Matumishi ya neno 'wadeni' ni neno lenye umuhimu la zamani; maana yake ni zaidi ya mtu kuwa na deni yako; inazungumzia watu kukoseana mmoja na mwingine.

**Wasamehe wengine kwanza**

Tunahitaji kutambua ya kwamba kuwasamehe wengine ina umhimu mkubwa kwetu kupokea msamaha wenyewe. Yesu anahimiza katika **Matahayo 6:14-15,** baada ya kutufundisha ombi la Bwana. Anaongea tena kuhusu umuhimu wa kusameheana: ***"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."*** *Hii inathibitishwa katika* **Mariko 11:25-26.**

Yesu anapeana mfano wa mtumishi ambaye hakusamehe, baada ya kumuagiza Petro ya kwamba tunapaswa kuwa na nia ya kusamehe ndugu "***hata saba mara sabini"*** **(Mathayo 18:22).** Tafadhali soma mithali iliyoelezwa katika **Mathayo 18:23-35.**

**Msamaha huachilia uponyaji**

Wakati mwingi uponyaji na ukombozi huja wakati mtu anasamehe wale ambao wamemuuthi, ama mtu ambaye wanajihisi ni mdeni wao. Kuna wakati ambapo mathara/kidoda ama dhuruma ni kubwa sana tunahitaji neema spesheli kutoka kwa Mungu ili tuweze kusamehe. Tunapochagua kusamehe, Mungu anatupa neema ya kutuwezesha kutoa msamaha wa kweli.
Msamahe haumaanishi kukubaliana na makosa yaliyofanywa, Mungu huchukia dhambi, lakini huwasamehe wenye dhambi. Kwa hivyo kwa neema ya Mungu tunaweza kumsamehe mtu aliyetukosea.

Tutazamapo msalabani, tunaona kwamba Yesu alikufa kwa dhambi za ulimwengu wote. Hii inahusisha dhambi tulizotendewa. "***Kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi"*** **(Warumi 5:8).** Kupitia neema ya Mungu, tumsamehepo mtu, uchungu na jeraha zinanza kuondoka kutoka kwa kumbukumbu.

### G.) TUNAOMBA KUELEKEZWA

**"*Na usitutie majaribuni".***

Mungu hua hatujaribu, tusijitie kwenye njia ya majaribu. "***Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia" (*****1Yohana 2:16).** Ni lazima tujifundishe kujizuia mambo yale ambayo yangetusongeza bali na Yesu Kristo.

Huwa tunajaribiwa namna gani? **Yakobo 1:14**

……………………………………….......................................................................................

……………………………………………………………………………………………

Ni mashauri yapi ambayo Paulo anampa Timotheo? **2 Timotheo 2:22**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

Ni nini ambacho Mungu atatufanyia tukijaribiwa? **1 Wakorintho 10:13**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

### H.) TUNAOMBA USITUTIE KWENYE MAJARIBU

**"*Lakini utuokoe na yule mwovu"***

Yesu aliomba kwa ajiri ya ulinzi wetu: ***"Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu, bali uwalinde na yule mwovu"*** **Yohana 17:15.**

Tunapoona yale ambayo Yesu ametutendea tunamtazama, tukitambua nguvu zake kuu ya kukomboa na kuokoa kutoka kwa yule mwovu. Pale msalabani Yesu alipokea ushindi kamili juu ya shetani na juu ya yote yaliyo maovu. Sasa kupitia imani kwa jina lake, tunaweza kutembea katika ushindi.

**Yakobo anatufundisha jinsi ya kumshinda yule muovu.**

Tunafanya nini? **Yakobo 4:6-8**

i. Nyenyekea upokee neema **(aya 6)**

ii. Mtii Mungu, mpingeni shetani (**aya 7)**

iii. Mkaribieni Mungu, itakaseni mikono yenu, safisheni mioyo yenu**"** **(aya 8)**

**Paulo anatuambia jinsi ya kumshinda shetani**

- Tunatumia silaha ambazo Mungu ametupa, kwa maana zina "***Uweza katika Mungu hata kuangusha ngome"*** **(2 Wakorintho 10:4).**
- Tunateka ***"Nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"*** **(2 Wakorintho 10:5*)*.**
- Tunatumia "***Upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu"*** **(Waefeso 6:17)**
- ***"Uushinde ubaya kwa wema"*** **(Warumi 12:21)**

## I) TUNATAMATISHA KWA KUABUDU

***"Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina."***

Tulianza maombi na kuhusiana na Mungu kibinafsi kama Baba yetu, na sasa baada ya wakati wa maombi.

- Tunamtazama Bwana Mungu, tukitambua ya kuwa ufalme wa Mungu ni hakika na unatufaa katika maisha yetu; yakuwa mamlaka yote ni Yake (**Mathayo 28:18)**

- Tunatambua ya kuwa nguvu zilizo katika kazi kwa maisha yetu sasa ni nguvu za Mungu, zikihuishwa katika mtu wetu wa ndani na Roho Mtakatifu (**Waefeso 3:16)**
- Tunampa Mungu utukufu wote, tukijua kwamba kila kitu chema chatoka kwake **(Yakobo1:17);** na mapenzi yake kwetu ni "***Mema, ya kupendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2).***

## Zoezi la mtu binafsi

*Enenda mahali penye utulivu, andika ombi la Bwana ukiacha nafasi katika kila aya. Katika nafasi hiyo andika mawazo yako, mambo ya kuombea, maandiko na kitu kingine chochote kinachokujia. Sema na Mungu unapofanya zoezi la ombi. Kumbuka, maombi ni mawasiliano na Mungu, watu wawili wakisemesana. Muombe Mungu akuzungumzie na akuelekeze.*

**SOMO LA ISHIRINI NA SABA**

# ROHO MTAKATIFU NI NANI?
## {SEHEMU YA KWANZA}

“***Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watapokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa”*** **Yohana 7:37:39.**

Katika andiko hili Yesu anathibitisha na kuendelesha yaliyonakiliwa katika agano la kale kuhusu maji na mito [na mvua] kama ishara ya Roho Mtakatifu ndani ya na kupitia maisha ya watu. Huduma ya Roho Mtakatifu huleta neno la Mungu kutoka kwa roho ya kiroho ya muamini.

## AHADI YA BABA

- **Matendo 1:4** Yesu alisema wangonje hile “***Ahadi ya Baba”:*** Baba alikuwa ameahidi Roho Mtakatifu.

- **Luka 24:49 “*Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakimi kaeni humu mjini, hata mvikwe uweza utokao juu”***

- **Yohana 14:26 “*Lakini huyu msaidizi, huyu Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia”***

### Roho mtakatifu ni ahadi ya Baba

Baadhi ya maandiko katika Agano la kale yanayoonyesha ahadi ya Roho:

- **Yoeli 2:28** Mungu anasema “***Hata itakuwa, baada ya hao, ya kwamba nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili”.*** Katika **Matendo 2:17-21** Petro ananukuu kutoka kwa Yoeli.

Petro anasema nini katika **Matendo 2:16?** ..........................................................................................

………………………………………………………………………………………………………

- **Ezekieli 36:26-27 “*Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda”.***

- **Yeremia 31:31-34** anaonyesha kuhusu Agano Jipya. Mungu ataandika sheria zake ndani ya mioyo yetu na kuziweka katika mawazo yetu. Mungu hufanya haya kwa kumtuma Roho Mtakatifu kudumu ndani yetu mara tunapompokea Yesu. [aya hizi zimenukuriwa katika **Waebrania 8:8-12, 10:16].**

- **Zakaria 4:6 “*Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu”* ‘**Uwezo’ unaongea kuhusu nguvu za kibinadamu, haswa silaha za majeshi; ‘nguvu’ inaonyesha uweza wa mwanadamu.

- **Isaya 43:19b** inaahidi "*Mito katika jangwa" [*linganisha na **Yohana 7:38].** Ni Roho Mtakatifu ambaye huyaleta maisha mapya ambayo yanatoka kwa Mungu. Anafananishwa na mito jangwani.

- **Isaya 12:3 "*Basi, kwa furaha, mtateka maji katika visima vya wokovu"***, ikiongea kuhusu maji ya uzima. Visima vya wokovu vimo ndani ya moyo wa kiroho wa muamini.

## ROHO MTAKATIFU ULIMWENGUNI

Roho Mtakatifu alikuwa kazini katika uumbaji, "***Nayo, nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza ilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho wa Mungu akatulia juu ya uso wa maji"*** **Mwanzo 1:2**

Roho Mtakatifu alifanya kazi nchini kabla ya kuja kwa Yesu; lakini inabainisha kwamba hakuwa amefunuliwa kikamilifu wala hangeweza kulileta kusudi la Mungu kutimilika mpaka Mwana wa Mungu kuachilia ukombozi wa ulimwengu.

Roho hakuwa amekuja katika utimilifu wa vile Mungu alikusudiwa kwa sababu hukuwa umewadia wakati. **Yohana 7:39** tunajua kwamba **hangekuja mpaka wakati ambapo Yesu angetukuzwa**; hii inamaanisha hangekuja mpaka wakati Yesu angekufa kwa dhambi zetu msalabani na alejee mbinguni na utukufu.

### Roho Mtakatifu kazini katika Agano la Kale

Tunapo tazama baadhi ya mifano katika agano la kale tunaona matendo ya Mungu kupitia Roho wake Mtakatifu kabla hajaja Yesu:

- **Waamuzi 6:34 "*Lakini roho wa BWANA akaja juu yake Gidioni; naye akapiga tarumbeta."***

- **Waamuzi 14:6** ikizungumzia Samsoni: "***Roho ya BWANA ikamjliia kwa nguvu, naye akampasua mwana-simba kana kwamba anampasua mwana mbuzi"*** na **aya 19** "***Na Roho ya BWANA ikamjilia juu yake kwa nguvu, naye…akawapiga watu thelathini"***

- **Roho Mtakatifu "*akawajilia"* watu hao na kuwatia nguvu** kutenda kazi za ajabu, akiwapa uweza na ujasiri ambao hawakuwa nao kikawaida.

- Wakati Yesu alikuja alisema kutakuwa "***mito ya maji ya uzima yaliyo hai itatoka ndani yake," (Yohana 7:38),*** kama matokeo ya kazi yake ya ukombozi. Roho Mtakatifu **'angekuja ndani ya'** kila muumini, akitupa nguvu na ujasiri ambao hatunao kikawaida.

Tambua mabadiriko: katika Agano la Kale Roho Mtakatifu '**alikuja juu'** ya baadhi ya waliochaguliwa kuwawezesha kutenda kazi ya Mungu; Katika nyakati za Agano jipya Roho Mtakatifu **'hukaa ndani'** ya kila muumini, akimuwezesha kila muumini kuwa nabii, kuhani na mfalme!

## YESU NA ROHO MTAKATIFU

- Yohana alimtambua Yesu kupitia kuja na kudhihirishwa kwa Roho Mtakatifu, (**Yohana 1:32-34).** Baba alikuwa amemwambia Yohana atakachokitazama: "***Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyu ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu" (aya 33).***

- Yesu alipokea Roho Mtakatifu kwa njia ya udhihirisho wakati wa kubatizwa kwake **(Mathayo 3:16).**
- Yesu alipokea **"*Roho bila kipimo" (*Yohana 3:34).**
- Yesu aliongozwa na Roho Mtakatifu jangwani akajaribiwe na shetani **(Luka 4:1)**
- Yesu alitoka jangwani kwa nguvu za Roho Mtakatifu **(Luka 4:14).**
- Yesu alipakwa na Roho Mtakatifu kwa sababu ya huduma yake na tume duniani: " ***Roho wa BWANA yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta…" (Luka 4:18).***

***Yesu hakuanza huduma yake ya hadhara mpaka alipojazwa na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu.***

## ROHO MTAKATIFU NI NANI?

Yesu aliongea wazi kuhusu Roho Mtakatifu kama:

- **Mtu,** kama yeye mwenyewe (**Yohana 14:16)**
- **Mfariji,** anayetembea pamoja nawe, ajaye kukusaidia (**Yohana 14:16, 15:26)**
- **Mwalimu,** atakayetufunza mambo yote na kutukumbusha ambayo Yesu alisema (**Yohana 14:26, Luka 12:12)**
- **Mwelekezi**, atakaye tuelekeza katika kweli yote **(Yohana 16:13)**
- **Roho wa kweli,** atakayedumu ndani yetu **(Yohana 14:17, 15:26)**

***Roho Mtakatifu ndiye yule Roho kamili wa Mungu mwenyewe.***
***Yesu ni Mungu akidhihirishwa katika mwili***
***Sasa Mungu huja kwetu kwa njia ya Roho wake***
***Yesu Kristo anajulikana kwetu kupitia Roho Mtakatifu***

Aya ya kukariri: "***Roho wa BWANA yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri mataifa habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kuwatangazia mwaka wa Bwana uliokubaliwa"***
**Luka 18:19**

## Maswali:

**Ahadi ya Baba in gani?**...........................................................................................................

Ni mabadiriko yapi yaliopo kutoka Agano la kale na Agano jipya jinsi Roho Mtakatifu alivyokuja?
………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………..

Ni udhihirisho upi ambao Baba alikuwa amemwambia Yohana kutazama ili aweze kumtambua Yesu? Andika **Yohana 1:33.**

...........................................................................................................................................

...........................................................................................................................................

...........................................................................................................................................

....................................................................................................................................

**SOMO LA ISHIRINI NA NANE**

# ROHO MTAKATIFU NI NANI

## (SEHEMU YA PILI)

### YESU ALIONGEA KUHUSU KUJA KWA ROHO MTAKATIFU NA HUDUMA YAKE

***“Nami nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele”*** **Yohana 14:16**

Neno la Kiyunani la ‘Msaidizi’ ni *‘parakletos’ SC.#3875:* neno hili linaonyesha muombezi, mfariji, msaidizi, wakili, mshauri. Katika masomo yasio ya kibiblia *‘Parakletos’* ilikuwa na maana ya kiujuzi ikimaanisha mwakilishi anayeonekana kotini kwa niaba ya mwingine. Roho Mtakatifu huongoza muumini katika ufahamu mkuu wa ukweli wa injili. Katika kuzidisha kwa msaada wa kijumla na muelekezi, anapatiana nguvu za kustahimili vita/changamoto za mitindo ya ulimwengu.

Neno la Kiyunani la ‘Mmwingine’ ni ‘allos’ SC. #243. Inamaanisha aliye kando, mwingine wa kufanana. Yesu anatumia ‘allos’ kwa kumtuma mfariji mwingine ***“****ambaye yuko kando yangu na pamoja/kuongezea nami lakini ni kama mimi. Atatenda wakati sipo kila ambacho ningefanya kama ningekuwapo binafsi nanyi.”* Kwa njia nyingine Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba atakuja kwa Roho wake kuwa pamoja nao.

i. **Atakaa ndani yenu.**
Yeye ni Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kupokea, ***“bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu”*** **Yohana 14:17.** Hii ni lugha ya kupendeza sana: Ni nani alikuwa akikaa na wanafunzi? Ni Yesu! Lakini Yesu anapotuma Roho, hiyo itamuwezesha Yesu kukaa ndani ya kila mmoja wetu.

ii. **Atawakumbusha mambo yote**
Ametumwa na Baba na ndiye msaidizi, mwalimu na yule “***atakayewakumbusha yote niliyowaambia”*** **Yohana 14:26.**

iii. **Anamshuhudia Yesu**
Ni Roho atokaye kwa Baba na anamshuhudia Yesu (**Yohana 15:26).**

iv. **Hengekuja hadi Yesu arudi mbinguni**
Hakuwa na uweza wa kuja hadi Yesu arudi mbinguni, “***Yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo msaidizi hatakuja kwenu, bali mimi nikieda zangu, nitampeleka kwenu.”*** **Yohana16:7**

v. **Atawashawishi watu wa ulimwengu**
Yeye ndiye Roho atakayewashawishi ulimwengu kuhusu dhambi na kwa haki na hukumu. **Yohana 16:8-11.**

vi. **Atawaelekeza wanafunzi katika kweli yote**
Yeye ni Roho ambaye “***Atawaongoza awatie katika kweli yote, kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake”*** **Yoh 16:13.**

**vii. Atayafunua mambo ya Yesu**

Roho Mtakatifu atamtukuza Yesu pia, "***Kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari,*** **Yohana 16:14** ***"Na yote aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo alisema atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasheni habari"*** **Yohana 16:15.**

- Roho mtakatifu ametoka kwa Mungu;
- Roho Mtakatifu ametumwa na Mwana wakati arirudi **"katika kifua cha Baba" Yohana 1:18**
- Roho Mtakatifu anakuja kumfanya Baba ajulikane kwetu na kulisema neno lake kwetu.

## AGANO JIPYA

Mungu alikuwa na mpango wa kumrejesha mwanadamu kwake; ni kwa njia ya **kuzaliwa upya** na Roho Mtakatifu **(Yohana 3:5-6),** akituleta katika ushirika na ushirikiano na Mungu mwenyewe

Mungu aliahidi kwa kupitia manabii ya kuwa atafanya Agano jipya na watu wote. Agano jipya liko "**ndani ya Roho' "*Mungu ni Roho, nao wamwbuduo yeye inawapasa kuabudu katika Roho na kweli"*** **Yohana 4:24.**

Kupitia Agano jipya Mungu angefunuliwa kwa watu wake katika njia ambayo watakatifu wa Agano waliona maono na kutabiri.

### Binadamu alianguka katika mwili, katika uadui na Mungu

Roho Mtakatifu ndiye jawabu ya shida za binadamu.

- "***Enendeni kwa Roho, wala hamutatimiza kamwe tamaa za mwili" Wagalatia5:16***
- ***"Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zinapingana, hata hamuwezi kufanya yale mnayotaka" aya. 17***
- ***"Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria" aya. 18***
- "***watu watendao mambo ya jinsi hiyo*** [matendo ya mwili **aya 19-21**] ***hawatarithi ufalme wa Mungu" aya. 21b***

Tunahitaji Roho Mtakatifu ndani yetu atufundishe neno la Mungu na anene mioyoni mwetu na mawazo. Pasina yeye itakuwa vingumu kushinda ulimwengu.

### Agano jipya katika Roho

Mungu aliahidi Roho kwa watu wake (**Ezekieli 36:26-27)** na akaahidi Agano bora, Agano jipya ambapo Roho angekuja na kukaa katika maisha ya watu wa Mungu.
Ilihitaji kifo cha mwokozi, Yesu, kuwakomboa wanadamu, damu yake ikituosha kutokana na dhambi zetu, ili tuweze kumpokea Roho wa Mungu.

#### Ahadi!

Tunapoitikia kwa injili tunapokea ahadi ya Roho Mtakatifu**. "*Tumbuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** Ahadi ni kwa ***"ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali"*** **Mdo 2:38**

#### Tubu dhambi kwanza

Hatuwezi kupokea Roho wa Bwana katika maisha yetu tusipotubu dhambi zetu na kupokea masamaha kupitia kifo cha Kristo msalabani.

**Amini na ubatizwe katika jina la Yesu.**

Katika **Matendo 19:1-6,** wanafunzi ambao Paulo alikuta Efeso walikuwa hawajasikia habari za Roho Mtakatifu; walikuwa tu wamepokea mafundisho ya Yohana mbatizaji. Iliwapasa kumwamini Yesu na kubatizwa katika jina lake kabla ya kupokea Roho.

- Eliwa iliwabidi kubatizwa tena kwa maana ubatizo wa wakristo unafanya kazi tu kwa sababu ya msalaba – kumwagwa kwa damu - na ubatizo wa Yohana haukutoshana na ubatizo wa wakristo.

Elezea kubatizwa tena kwa wanafunzi **Matendo 19:1-6**

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

## UHUSIANO WETU NA ROHO MTAKATIFU

**1)** Roho Mtakatifu anaweza **kuhuzunishwa.** kuhuzunika ni kuitikia zile hisia za ndani. Paulo anabinafsisha Roho Mtakatifu katika **Waefeso 4:30 "*Msimuhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi".*** Kumbuka Roho Mtakatifu ni mtu wa Mungu, anayedhihirika duniani.

**2)** Roho Mtakatifu anapeanwa kwetu kama **muhuri wa ukombozi wetu (Waefeso 1:13-14)** kuonyesha umilikiji wa Mungu kwetu- tulinunuliwa kwa dhamana.

**3)** Roho Mtakatifu anatushugulikia na **kututakasa** (**Warumi 15:16)**

**4)** Tunaweza kuwa na **ushirika** na Roho Mtakatifu **(2 Wakorintho 13:14):** tunaweza kushiriki, kuongea na kupokea kutoka kwa Roho Mtakatifu na kufurahia uwepo wake maishani mwetu. Analeta uwepo wa Mungu katika maisha yetu.

**5)** Roho Mtakatifu anaweza **kuzimwa.** Kama tukikata kile Roho Mtakatifu anatupa binafsi au kwa pamoja, "**tunamzimisha yeye" (1Wathesalonike 5:19).** Ni vyema kukuwa katika hali ya kuwa wasikivu kwa mwelekeo na msukumo wa Roho Mtakatifu, tukithamini kipawa cha upako katika maisha yetu na kujifundisha kuongozwa na Roho katika mikutano na mahusiano.

**6)** Tunatayarishwa na **kuwezeshwa** na Roho Mtakatifu kuwa wahuduma wa Agano Jipya

- Ninyi ni barua ya Kristo **(2 Kor 3:3)**
- Iliyo katibiwa na Roho wa Mungu aishiye **(2 Kor 3:3)**
- Sio katika vibao vya mawe bali katika mioyo yetu **(2 Kor 3:3)**
- Ametufanya wahuduma wa Agano Jipya kwa Roho **(2 Kor 3:6)**
- Roho hupatiana uzima (**2 Wakorintho 3:6)**

**7)** Tunaweza kuomba tu kwa jinsi iliyofaa **kwa [katika] Roho; "*kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho"*** **Waefeso 6:18**

**8)** Ni kwa Roho Mtakatifu ambapo **tunaabudu, “*tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana aliye Roho”* (2 Kor 3:18)**

**9)** Mungu anatamani tuwe na Roho wake ndani ya maisha yetu, **tuishi** na **tutembee na Roho (Wagalatia 5:25).** Bila yeye hatuwezi kujua na kuyaishi maisha ya kikristo

**10)** Tunahitaji Roho katika maisha yetu ili tuweze kufurahia **tunda lake** katika maisha yetu, upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi (**Wagaratia 5:22-23)**

**11)** Tunahitaji Roho Mtakatifu kwa maisha yetu kwa maana anapatiana karama kwetu kuujenga mwili wa Kristo (**1Wakorintho12:7-11)**

***Mungu anatazamia sisi tupokee na tuongozwe na roho wake***

**SOMO LA ISHIRINI NA KENDA**

# ROHO MTAKATIFU KUJA

## JINSI YA KUJAZWA

Kabla Yesu hajapaa mbinguni Alipeana ahadi kwa wanafunzi wake, ***"Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu"*** **Luka 24:49.** Kupokea Roho Mtakatifu ingekuwa ni ujuzi wa kupokea nguvu za kiungu kutoka kwa Mungu.

Katika **Matendo 1:4** Yesu alisema wangoje ambacho Baba alikuwa ameahidi: alisema "***Bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache"*** **aya 5.** Katika mazingira yale yale alisema "***lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata miisho ya nchi"*** **Matendo 1:8.** Nguvu za Roho mtakatifu zinapatianwa kwa muumini pakiwa na kusudi la kushuhudia: kuwaambia wengine ukweli wa Yesu Kristo.

- **Yesu aliwaambia wanafunzi wake watarajie kupokea Roho Mtakatifu**
- **Ahadi ya Baba ni Roho Mtakatifu**
- **Walikuwa watiwe nguvu na Roho Mtakatifu**
- **Kutiwa nguvu ni kwa kumshudia Yesu**

### ROHO MTAKATIFU ALIKUJA KWA NJIA GANI?

Katika Matendo 2 tunaona kutimizwa kwa kwanza kwa ahadi ya Roho Mtakatifu kuja. Roho Mtakatifu alikuja siku ya pentekosti.

### Alikuja kwa nguvu, ishara za kiungu na karama.

Alikuja kwa uvumi kama wa upepo, kukatokea ndimi zilizogawanyika kama ndimi za moto, zikaonekana juu ya wanafunzi; na "***wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyigine"*** **Matendo 2:2-8**

### Kunene kwa lugha ambazo hawakuzijua

Kule kudhihirishwa kwa Roho katika waumini ilikuwa 'kusema kwa lugha [zingine]': "***Kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe"*** **(Matendo 2:6).** Wasikizaji wakasema, "***tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu"*** **(Matendo 2:11)**.

Wanafunzi walikuwa wakisema kwa lugha za watu. Kulikuwa na lugha za mataifa kumi na sita katika siku hiyo, na wote wakasikia injili ikihubiriwa kwa lugha zao wenyewe.

### Kuhubiri injili kwa ujasiri

Kama matokeo ya kujazwa na Roho Mtakatifu, Petro aliweza kuhubiri kwa ujasiri kuhusu Yesu. Petro alileta picha yenye nguvu ya Yesu kama mtu, "***aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara";*** Yesu: "***ninyi mkamsulibisha, ambaye Mungu alimfufua"*** **(Matendo 2:22-24*);*** kisha akazungumza habari ya Bwana aliyepaa ambaye anatawala na kutamalaki juu ya adui zake **(matendo 2:33-35).** Kisha akatangaza "***Basi nyumba yote ya Israeli***

***na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya huyo Yesu mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo"* (Matendo 2:36).**

Katika **Matendo 2:37** wasikizaji walishawishiwa na neno lililojaa nguvu za Roho. Wale waliolipokea neno walibatizwa **(aya 41). "*Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume"* aya 43.**

Matokeo ya Roho Mtakatifu kuja:

- **Ishara na ajabu**
- **Kuhubiri injili ya Yesu kwa kushawishi** kwenye nguvu, matokea yakiwa ni ubatizo wa wengi

## NITAMPOKEA ROHO MTAKATIFU KWA NJIA GANI?

1. **Kwa kuomba:** "***Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao!"* Luka 11:13.**

   Baba wa mbinguni ameahidi kutupa sisi Roho Mtakatifu. Yesu alisema twapaswa kumuuliza Mungu Roho Mtakatifu.

2. **Kwa kuziweka amri za Yesu:** yesu alisema, "***Mkinipenda, mtazishika amri zangu. Nami nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele"* Yohana 14:15-16.**

   Kupokea Roho Mtakatifu inakuja kama matokeo ya kumwamini Yesu na kutaka kujipatiana kikamilifu kwake. Tunahitaji Roho Mtakatifu ili tuweze kumuishia Yesu**.**

3. **Kwa kufahamu kwamba Roho anakaa ndani yenu:** tunakuja kwa imani ndani ya Yesu kwa utendaji kazi wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Yesu alisema, akiongea kuhusu Roho Mtakatifu, "***Bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu"* Yohana 14:17b**

   Wakati huo yesu alikuwa anakaa na wanafunzi, lakini hangekaa ndani yao kwa kuwa alikuwa amekuja duniani kwa mfano wa mwanadamu. Hata hivyo alikuwa ni udhihirisho kamili wa Mungu na alikuwa akingojea wanafunzi waelewe kwamba Roho akija, itakuwa ni Yesu amekuja, sasa akiwa na uweza wa kukaa ndani yao.

4. **Kwa kutubu na kubatizwa katika jina la Yesu:** kwa hivyo tunapokea msamaha wa dhambi na tunaweza kupokea karama ya Roho Mtakatifu **(Matendo 2:38).**

   Kuja kwa Roho Mtakatifu katika maisha ya kila muumini inatakiwa kutendeka wakati wa ubatizo. Katika maandiko, waumini wapya walipokea Roho Mtakatifu katika mazingira ya kutubu na kuamini Yesu. Na kubatizwa kwa jina lake.

5. **Kwa kuwekewa mikono:** Mara unapoamini Yesu na kubatizwa, wale wanao kubatiza wanatakiwa kukuwekea mikono ili upokee Roho Mtakatifu.

   ***"Ila wamebatizwa kwa njina lake Bwana Yesu, ndipo wakaweka mikono yao juu yao wakampokea Roho Mtakatifu"*** (**Matendo 8:16-17).** Wakati Paulo alikutana na baadhi ya wanafunzi kule Efeso, alitambua kwamba walikuwa hawajajazwa na Roho Mtakatifu. Paulo akawauliza habari ya ubatizo wao na akaona kwamba hawa wanafunzi walihitaji kumwamini Yesu na kubatizwa kwa jina lake. Kisha Paulo akaweka mikono yake juu yao ili wapokee Roho Mtakatifu **(Matendo 19:1-6).**

6. **Kwa kuliamini neno lililohubiriwa kuhusu Yesu**: watu wa mataifa katika nyumba ya Kornelio walipokea Roho Mtakatifu walipokuwa wakisikiza mara ya kwanza mahubiri ya Yesu Kristo. Roho aliwashukia **(Matendo 10:44-45).**

   Haya yanatendeka hata leo: wakati mwingine muumini anapokea Roho Mtakatifu kwa ukuu wanapomtafuta Bwana.

## ABATIZAYE KWA ROHO MTAKATIFU

Yesu kwa wazi ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu:

- ***"Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakaifu na kwa moto" (*Mathayo 3:11)**
- ***"Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu" (Mariko 1:8)***
- ***"Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto"* (Luka 3:16)**
- ***Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyu ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu"*** (**Yohana 1:33)**
- ***"Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu" (*Luka 24:49)**

Tunatakiwa kumtafuta Yesu ili tujazwe na Roho Mtakatifu.

### Kujazwa Roho Mtakatifu ni ujuzi unaoendelea

Tunahitaji kujazwa na RohoMtakatifu kila siku. Tunawaona katika kitabu cha Matendo baadhi ya wanafunzi ambao walipokea Roho Mtakatifu siku ya pentekosti walijazwa tena kuwawezesha kufanya kazi ya huduma.

Kwa mfano: "***Petro akijaa Roho Mtakatifu"*** akaanza kushuhudia mbele ya wakubwa wa watu na wazee wa Israeli **(Matendo 4:8);** kikundi kikubwa cha wanafunzi walipoomba**: "*Wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri"* Matendo 4:31**

### Huduma yenye mazao hutokana na kujazwa na Roho Mtakatifu

Wakati kazi ya huduma ilizidi na pakawa na mahitaji ya wahuduma wengine kuchaguliwa, walichaguliwa kulingana na msingi kwamba walikuwa "***Wamejawa na Roho Mtakatifu na hekima"* (Mdo 6:1-4*)***

### Baada ya kuokoka tungali tunahitaji kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu

Wengi waliitikia injili iliyo hubiriwa Samaria; waliokoka na kubatizwa, lakini wangali walikuwa wanahitaji kujazwa Roho Mtakatifu. Haya yalifanyika wakati mitume walikuja na kuwawekea mikono **(Mdo 8:12-18).**

Sauli alipata ujuzi wa wokovu akiwa njiani kuelekea Dameski. Kama matokeo ya huo ujuzi, alihitaji uponyaji wa macho yake; alihitaji kujazwa na Roho Mtakatifu; na kubatizwa kwa maji. Alipokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono **(Mdo 9:17-18).**

### Roho anatuwezesha kuishi na kutembea kama Wakristo

***"Tena msilewe na mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho*" (Waefeso 5:18).** Wakati tunajazwa na Roho Mtakatifu kila siku, tutadhihirisha maisha na furaha ya Roho, katika maisha yetu na mwelekeo. Tutaimba "***Zaburi na tenzi na nyimbo za Rohoni'* aya 19*;*** tutakuwa wenye shukrani katika kila hali **(aya 20);** na tutakuwa ***"tukinyenyekeana katika kicho cha Kristo"* (aya 20).**

## KUNENA KWA LUGHA MPYA

Katika siku ya Pentekosti, wanafunzi walisema kwa lugha mpya walipopokea kipawa cha Roho Mtakatifu: "***wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyo wajalia kutamka"*** **Matendo 2:4**

Paulo mtume alitangaza katika **1 Kor 14:18:** ***"Nashukuru Mungu ya kuwa na nena na lugha Zaidi ya ninyi nyote".*** Tunaweza kukisia Paulo alipokea karama ya kusema kwa lugha alipojazwa na Roho Mtakatifu katika mwanzo wa kutembea kwake kama mkristo (**Mdo 9:17).**

Kunena au kuomba kwa lugha, au kwa lugha zizizoeleweka, ni udhihirisho unaojulikana wa kujazwa na Roho Mtakatifu katika maandiko. Katika nyumba ya Kornelio, Petro na wale waumini waliotahiliwa walitambua kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amekuja wakati watu wa mataifa walianza kusema kwa lugha wakimtukuza Mungu (**Mdo 10:44-46).**

Wakati wanafunzi wa Yohana mbatizaji walimwamini Yesu, walibatizwa tena, "***Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri."*** **Mdo 19:16.** Moja wapo wa ishara ya kwanza kwamba watu hawa walikuwa wamepokea Roho ilikuwa kwamba waliongea kwa lugha.

Wakiti mwingine wapendwa wanauliza: 'Nilazima niseme kwa lugha?' Jawabu ni: Hakuna sheria! Hata hivyo, Roho Mtakatifu ameahidiwa kwa kila muumini na anataka kumpa kila muumini neema ya ajabu ya karama ya ndimi. Karama hii inainua na kutajirisha maisha ya muumini ya maombi, ikimwezesha muumini kusongea karibu na Mungu kupitia karama ambayo Roho Mtakatifu amepeana.

## Swali:

Ni naweza aje kujazwa na Roho Mtakatifu? Andika njia sita ambazo maandiko yanatupa ili kupokea Roho Mtakatifu:

1) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
2) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
3) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
4) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
5) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
6) ………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

### ***Baadhi ya himizo:***

*Ubatizo lazima uhudumiwe na matarajio ya maandiko ya kuwa muumini mpya akibatizwa vyema atapokea karama ya Roho mtakatifu. Kama ni wewe unashugulika na ubatizo, ni ya muhimu uhubiri kwa njia ambayo yule anayebatizwa atapata ubatizo akitarajia atatokea akiwa kiumbe kipya, akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu.*

*Endapo wewe ni muumini na tayari umekwisha kubatizwa lakini haujapokea karama ya Roho Mtakatifu, tuna kuomba ujifunze somo hili kwa umakini, ukiruhusu imani kujengwa ndani ya moyo wako unapo amini neno la Mungu. Jisikie huru kumuuliza kiongozi wako wa uwanafunzi na wengine ambao wamejazwa na Roho Mtakatifu kukuwekea mikono. Kama hautapokea bado basi mtafute Bwana wewe mwenyewe, ukijua kwamba ameahidi kukupa wewe Roho Mtakatifu na kukutia nguvu uwe shahidi.*

**SOMO LA THELATHINI**

# MUNGU HUELEKEZA KWA JINSI GANI?

Mwelekeo wa Mungu ni wa muhimu sana katika maisha ya kila muumini. Sisi wote tunataka kujua na kuwa na uhakika kwamba tunatembea katika mapenzi ya Mungu.
Tunapofanya mipango katika maisha yetu, hatupaswi kuifanya kwa uhuru pasipokuwa na Mungu, kwa maana "***Hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka".*** Badala ya kuwa na mawazo yetu sisi wenyewe, tunapaswa kusema, "***Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi"*** **Yakobo 4:14-15.**

### Tunaweza kujua namna gani tuko katika mapenzi ya Mungu?

Kuna mambo matatu muhimu ambayo tunahitaji kuzingatia ili kujua tuko katika mapenzi ya Mungu:

1. Tunapokea mwelekeo wa Mungu kupitia biblia ambayo ni **neno la Mungu**
2. Tunapata uhakikisho wa mwelekeo wa Mungu kupitia neno la Mungu kwa **Roho Mtakatifu akishuhudia** na akitupa amani ya ndani ambayo haiwezi kuzimwa
3. Tunaweza kuendelea na katika mapenzi ya Mungu wakati **Milango inafunguka,** hivyo ni, hali zinatuwezesha kufanya yale tunayoamini ndiyo mapenzi ya Mungu yaliyo thibitishwa

## 1. BIBLIA - NENO LA MUNGU

Biblia ni Mungu akizungumza nasi. Imeandikwa na watu ambao waliwezeshwa na Roho wa Mungu.

"***Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo njema"*** **2 Timoteo 3:16**

**Warumi 15:4** inasema kwamba kila kitu kimeandikwa katika biblia ni letu tujifunzwe **"*ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tunaini:"***

**a) Neno la Mungu hutuelekeza**

**"*Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu" Zaburi 119:105*.** Mungu ameahidi kulitia neno lake katika mioyo yetu na sheria zake katika mioyo yetu **Yeremia 31:33**

**b) Ni mwelekeo wa mapenzi yake**

Mungu ametoa mwelekeo wa mapenzi yake katika neno lake. Hatuhitaji maagizo mengine ya jinsi ya kuenenda katika maeneo mengi katika maisha. Kwa mfano **Wagalatia 5:19-21** inapatiana mwelekeo wa maisha na inaonya adhabu ya kutotii.

**c) Ni barua ya Mungu kwa mwanadamu**

Biblia inanakili matendo ya Mungu na mwanadamu. Inaitwa "**neno la Mungu"** kwa maana imeandika njia tofauti ambazo Mungu amenena na mwanadamu.
Kuanzia mwanzo katika kitabu cha **Mwanzo** tunamwona Mungu akimtafuta mtu (Adamu) apate kunena naye **(Mwanzo 3:9)**

Mungu alitoa maagizo yakipekee kwa Nuhu ***"aliyekwenda pamoja na Mungu"*** **(Mwanzo 6:9-22).**
Mungu aliongea na Ibrahamu katika matukio mengi, akitabiri kuhusu uzao wa Ibrahamu katika siku za usoni **(Mwanzo 12-22)**

**d) Inadhihirisha asiri ya Mungu**
Hii ni ya muhimu kwa maana ni kutokana na kufahamu kwetu jinsi Mungu alivyo tunaweza kuzileta tabia zetu katika mpangilio wa asiri yake. Katika **Wakolosai 3:10-15** maandiko yanatuambia wazi jinsi ya kuenenda kama mtu mpya, aliyeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu.

**e) Mungu anapatiana maagizo wazi**
Yapo **mawasiliano mengi kati ya Mungu na mwanadamu** yalionakiliwa katika maandiko**.** Tunasoma mambo kama ***"Mungu akasema na…"*** na "***neno la* Mungu likamjia…"** hakika kama kuwakemea Haruni na Miriamu, Bwana alisema kuhusu Musa, "***Kwake nitanena mdomo kwa mdomo, Maana, waziwazi wala si kwa mafumbo"*** **(Hesabu12:8)**

**Mifano katika maandiko** ya mawasiliano ya muhihu kati ya Mungu na mwanadamu yaliofunua mapenzi ya Mungu kwa watu hao kipekee:

- Mungu alimwonya Ibrahimu kuhusu yatakayotokea Sodoma na Gomora **(Mwanzo 18:23-32);**
- Mungu alidhihirisha utukufu wake kwa Musa, kama jawabu ya Musa alivyo omba **(Kutoka 33:12-23);**
- Mungu alimfunulia Yeremia asiri ya na maeneo ya wito wa kiunabii wa wito wa Yeremia (**Yeremia 1:4:10)**
- Bwana yesu alimuagiza Anania kuenenda kumsaidia Sauli [Paulo] ili ajengwe katika imani ya Kikristo (**Mdo 9:10-16)**

Mifano hii ni ya mawasiliano muhimu sana ambapo alikuwa akifunua mambo yenye umuhimu mkuu sana. Hata hivyo mara nyingi Mungu ataongea mambo nasi kuhusu mambo yanayo onekana madogo kutuwezesha kuyatambua mapezi yake.
Wakati Mungu anatujulisha mapenzi yake na tunatii na kufanya asemayo, mipangilio ya matukio ya shughuli zetu zitabadilika, na mapenzi ya Mungu yatatendeka.

**Mapenzi ya Mungu yanajulikana kwetu kupitia neno lililoandikwa**
Maagizo ya Mungu yako wazi. Kwa mfano, aliwaagiza wanafunzi wote "***Kuenenda na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi"*** **(Mathayo 28:19-20).**
Tabia zetu zote na kazi yetu ya huduma lazima iwe utiifu wa neno la Mungu. Mapenzi ya Mungu yanajulika tu kupitia kilichoandikwa.

## 2. <u>ROHO MTAKATIFU</u>

**Neno lililohuishwa**
Yesu alisema kwamba Roho Mtakatifu atakuwa msaidizi wetu, mshauri wetu, na mwelekezi wetu: "***Atawaongoza, awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanenena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake"*** **Yohana 16:13**
Roho Mtakatifu ndiye anayelihuisha neno lililoandikwa kwetu. Afanyapo hayo, inakuwa 'rhema' [neno lililohuishwa] hivyo ni neno lililotoka katika kinywa cha Mungu. "***Mtu hataishi***

***kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu"*** **Mathayo 4:4.** Huu ni ujuzi wa ajabu kusikia Mungu akisema katika Roho. Kuna kujua kwa ndani kwa kipekee kwa wakristo ambao wanaongozwa na Roho Mtakatifu.

**Roho mtakatifu huongea kupitia ndoto, maono na unabii**

***"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono"*** **Joel 2:28.**

Ni jambo la kawaida kwa wakristo waliozaliwa mara ya pili kupokea ndoto kutoka kwa Roho Mtakatifu; sio jambo lisilo la kawaida kwa watu waliojazwa na Roho Mtakatisu kuona maono yaliyo peanwa na Roho Mtakatifu, na wakati mwingine Roho atasema moja kwa moja kupitia neno la kiunabii.

- Yusufu mumewe Maria, alipokea ndoto kadha. Zilikuwa wazi sana na zilihitaji hatua ya utiifu mara moja. Maisha ya mtoto Yesu yalikuwa hatarini. Ona (**Matahayo 1:19-25; 2;13-15)**

  Elewa ndoto zote si za kawaida. Hakika ndoto nyingi huja kwa maneno ya mfano na maono na mara nyingi huhitaji kutafsiriwa.

- Paulo mtume alipokea maono ambapo, "***alimwona mtu wa Makedonia amesimama, akimsihi, na kumwambia, vuka uje Makedonia utusaidie, Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika kwamba Mungu ametuita tuwahubiri habari njema"*** **Mdo 16:9-10**

Ono hili lilikuwa la kawaida na lilihitaji utiifu wa ghafla. Paulo na kikundi chake walitii. Kabla ya Paulo kuyapokea maono ambayo yalimpa mwelekeo mwema, alikua akijaribu kwenda Asia, lakini "***Alikuwa amezuiliwa na Roho"*** **(aya 6).** Kisha Paulo, ***"Wakajaribu kwenda Bithinia, lakini Roho wa Yesu hakuwapa ruhusa"*** **(aya 7)**

**Hakika Roho atatuongoza katika mapenzi ya Mungu yaliyo makamilifu**

**Amani ya Roho Mtakatifu**

Roho mtakatifu anapotupa mwelekeo, ambacho kitafunuliwa huendana na maandiko na kitatuacha na amani. Mungu haleti utatanishi ama shaka kwetu. Roho Mtakatifu anatuelekeza wakati tuko na mapatano na Mungu. Anatusaidia kuona dhambi zetu na makosa, lakini hatuhukumu.

Wakati **Roho Mtakatifu** anatushawishi, **anakuwa wazi** na anatuonyesha jinsi ya kurekebisha hali. **Anarejesha amani,** ambapo hukumu inatuacha bila utulivu na hakuonekani njia ya kutoka katika hali hiyo.

Inatupasa kumtafuta Mungu katika maombi ili tujue mapenzi yake, "***msijisumbue na neno lo lote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na <u>amani ya Mungu</u>, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu"*** **Wafilipi 4:6-7**

## 3. <u>HALI</u>

**Wakati wa Mungu**

Kuna wakati ambapo **Mungu hufungua milango** na anapatiana **nafasi** kuendelea na jambo ambalo amelipatiana na anatamani tulitende. Milango hii hufunguka katika **nyakati za Mungu.**

Kwa mfano, Petro alipokea maono kutoka kwa Mungu na utafsiri wa maono yale kutoka kwa Roho wa Mungu. Udhibitisho wa maono yale punde yakaja wakati watu wamataifa walifika kumkaribisha aende nao kwa nyumba ya Kornelio. **Mlango ukafunguka wa Petro kutii** na kutimiza maono. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa injili kuwafikia watu wa mataifa. Soma yaliyoandikwa katika **Mdo 10:9-48.**

**Hali zetu zinakuja kwa mpangilio**

Wakati Mungu anafungua mlango, hali zetu zinakuja katika mpangilio wa yale Mungu ameweka ndani ya mioyo yetu tufanye.

**<u>Ushuhuda</u>**

Tulishuhudia mfano wa haya kwa nguvu katika kikundi chetu cha kitume cha SHILOH mwaka wa 2010. Dada mkomavu ambaye hajaolewa alikuwa na hali ya kutamani kwenda Zambia ambako alikuwa ametumika hapo nyuma. Aliposhiriki matamanio yake tulipatana naye kwa hayo lakini tukampa changamoto kwamba angoje wakati wa Mungu, ambayo ilimaanisha kwamba hali yake itaingiana itakuja katika mpango na mlango ufunguke.

Kwa miezi kadha dada yetu aling'ang'ana kuyajua mapenzi ya Mungu alikuwa ameazimia kwenda tarehe fulani lakini hali yake haikumruhusu.

Hata hivyo baada ya hayo, alifikia wakati wa kumtii Mungu na moyo wake ukajaa amani ya Roho Mtakatifu. Baadaye hali zake zikaanza kuingiana. Akapata nauli na msaada uliotengwa kwake wa kumwezesha kuwa nje kwa miezi kumi na miwili.

**Yesu hufungua mlango**

Yesu ndiye aliye na ufunguo wa Daudi; ni ***"yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga na hakuna afunguaye"*** **Ufunuo 3:7**

Alisema "***Tazama, nimekupa mlango uliofunguka mbele yako, ambapo hakuna awezaye kufunga*** **(aya 8).**

Yesu anapofungua mlango, tunaweza kuendelea.

### *Kuwa na uhakika kwamba tuko katika mapenzi ya Mungu yaliyo kamilifu,*

- ***Mambo haya matatu:***
- ***Neno la Mungu,***
- ***Udhibitisho ambao Roho Mtakatifu anapatiana,***
- ***Na hali zetu,***
- ✓ ***Lazima zote ziambatane,***
    - ***Zikituwezesha kufanya mapenzi ya Mungu.***

**Swali:**

Umeshawahi kuwa na ujuzi Mungu akikuongoza? Shiriki ujuzi wako.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

# NI NINI KINACHOFUATA?

Sasa kwamba umemaliza masomo haya ya msingi wa uwanafunzi, tunakuhimiza sasa ujiunge na masomo ya uwanafunzi ngazi ya juu. Kitabu cha pili kitakupeleka katika ufahamu wa ndani wa neno la Mungu

Biblia inasema: "***Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"*** **waebrania 4:12.** Hakuna jambo lingine duniani kama neno la Mungu. Kwa hivyo kuna hitaji ya jitihada kujifundisha neno la Mungu **(2Timotheo 2:15)**

Yesu alisema: "***ninyi mkikaa katika neno langu mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli, tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** **Yohana 8:31-32.** Tukilipokea neno la Mungu na kuendelea ndani yake tutatembea katika uhuru mkuu kama wanafunzi wa Yesu Kristo.

Muandishi wa Waebrania alishangaa yakuwa waumini waebrania hawakuwa wamekuwa mpaka ukomavu ambapo walikuwa na uweza wa kuwafundisha wengine. Akasema "***Kwa maana iwapasapo kuwa walimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu"***

Ni ya muhimu kama waumini tupate kuendelea kukoma, kwa maana lengo la Mungu kwetu ni tuwe waumini wakomavu ambao wana uwezo wa kuwafundisha wengine pia. "***Na mabo yale uliyoyasikia kwangu, mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine"*** **2 Timotheo 2:2.**